

Msimulizi, 1895¹

Edited and corrected by
Arvi Hurskainen
Department of World Cultures, Box 59
FIN-00014 University of Helsinki, Finland
arvi.hurskainen@helsinki.fi

Abstract

This is a corrected version of Msimulizi, the first periodical written and printed in Swahili language. The periodical was established to be an information channel between scattered mission stations of the Universities' Mission to Central Africa, and also between the supporters of the mission work in Great Britain. The periodical was originally scanned and made available by SOAS (School of Oriental and African Studies, London). Obvious scanning errors were corrected. Also, clear errors in original print text were corrected. However, nonstandard spelling was not corrected, if it was possible to assume that the writer intended to write in the way it was done.

The file follows the original pagination. A page in the original publication is a page in this file. Page numbering is continuous from year to year, and it is printed at the top of the page.

This file contains the text of year 1895.

MSIMULIZI. 1895

Imepigwa chapa Kiungani, Zanzibar,
katika "Universities' Mission to Central Africa,"

MIMI HAPA MSIMULIZI!

Ee! rafiki zangu habari gani za mwaka huu 1895? Mimi ni mzima na afya zangu sijui ninyi mhali gani? Singeuliza habari zenu, illa kwa sababu

¹ The text is issued under licence CC BY-NC

nimebaki peke yangu, sina rafiki wengi kunipasha habari zenu kama zamani zile za kwanza. Najua tabia za waana Adamu, ati wakimwona mgeni amewajia, hupenda sana kuzungumza naye, wala hawamwachi peke yake, maana ataona ukiwa mtupu. Balli akikaa nao sana, marra humkinai upesi. Nami zamani zile za kwanza, watu wakipenda mno kunijia, kuniona wala sikuwa nikitindikiwa chochote.

Siku hizi, watu wa Ulaya Ingreza, na Nyasa, na Wayao ndio wanaonipenda mno, hatta hawataki nitoke machoni pao; lakini watu wa Bonde, na watu jirani nikaaao nao, wamenikinai, na sababu sijui, mmoja kwa kumi anayecheka nami.

Kiisha watu wananiogopa burre, walla sina gharama nyingi, nami natembea mwaka mzima kwa pesa sita tu. Ati mimi kiisha Mzalia hafi na maji; zamani nikinenepe sana, lakini miaka hii nimethii mno.

Tafathali mapadre mnaokaa katika killa Upelekwa wetu, waamsheni hao wanaoleta habari zangu Msimulizi, nipate kustawi katika maongezi yangu, maana ndio chakula changu.

MSIMULIZI. 824

KIUNGANI.

Tumefurahi mno kwa sababu kama mjuavyo wengi wenu, kama Bibi Bartlett alikuwa hawezi sana, hatta daktari akamwambia aende kwao Ulaya Ingereza, akaenda. Nayo hewa ya kwao imemfaa sana, bassi mwezi wa December mwaka jana ametuasilia tena naye anakaa hapa kama kwanza.

Tena mwezi ule ule Dec. 20 amewasili bapa B. Madalito akitoka pande za Kepi.

Dec. 24 tulipamba nyumba yetu na kanisa pia tayari kwa siku kuu ya kuzaliwa Bwana wetu, jioni yake ilikuwa ibada kubwa mno pamoja na uwandamano na mahubiri.

Bassi alfajiri mapema saa kumi mzinga ulipopigwa, watoto wote waliamka wakaimba Christmas Carols, hatta kulipokuwa kweupe killa mtu akajitengeneza tayari kwa ibada kubwa ya Eukaristi Takatifu. Siku hiyo killa mtu na furaha nyingi mno moyoni mwake.

Dec. 28, Ilikuwa mkutano Mbweni, Kiungani, na Mkunazini twalikwenda, na jioni wageni wengi Wazungu walikuja ndani ya magadi, hatta jioni killa mtu akarejea katika makazi yake.

Dec. 31, Tulikuwa na safari ya kwenda Mkokotoni, tukataraja kuondoka hapa majira ya saa a kumi unusu. Bassi tukaamka saa kumi, tukaanza kujifunga-funga kwa safari, lakini mvua ikatuzuia, tusiweze kuondoka saa kumi unusu. Ilipotimu saa edashara unusu tukaondoka. Tulikuwa jumla kama watoto 35, na Mr. King na Mr. Hitchbone, tukaenda hatta ilipotimia saa a pili tukawasili Bububu tukapumzika. Tukanunuliwa

MSIMULIZI. 825

madafu tukanywa tukesha, tusikae muda mwingi marra tukaondoka na kuondoka tulikoondoka hapo tukaanza kuachana, wangine wakatangulia mbele pamoja na Mr. Hitchbone, na wangine tukabaki nyuma na Mr. King.

Bassi tulipoachana vile, sisi wa nyuma shughuli yetu ikawa kwenda hima tukapate kuwafikia wale waliotangulia.

Mwalimu Daudi akapiga mbio kwenda mbele, lakini asiwakute kwani alipotea njia akaenda karibu na Mwanda, na wale waliotangulia walipita njia ya juu isiopita Mwanda. Bassi yeye akawa akisafiri peke yake, kurudi nyuma tuliko sisi asiweze, wala wale wa mbele asiwaone. Bassi akavunja tu mashambani hatta akawasili Mkokotoni saa a saba akakaa.

Sisi tuliokuwa nyuma nasi tukafanya kupotea njia kidogo, lakini marra tuliipata njia waliopita wenzetu, marra tukamkuta Mr. Hitchbone, yee na punda wake na watoto watatu. Tukamwuliza habari, akanena ni hivi mnionavyo na hawa watoto, wangine wako wapi?, Akanena mbele. Bassi tulipokwenda kidogo tu tukawakuta.

Je! jinsi gani Mwal. Daudi mmemwona? Wakanena la, tangu kuonana Bububu hatta sasa hatujamtia machoni. Bassi tukajua amepita njia ingine. Bassi pale wazungu wakapika chayi wakanywa, na watoto wakatafuna vikate vyao, na wakatafuta madafu wakanywa. Na hapa ndipo Chichele. Bassi tulipokwisha kupumzika sana hapo tukang'oa, wakati huo tukaenda kwa umoja tena mpaka tukafika Mkokotoni, kama majira ya saa tissa. Tukamkuta Mwal.

MSIMULIZI. 826

Daudi amewasili kiasi.

Tulipokwisha kupumzika tukaanza kufikiri mchezo wa kinwani tena, kwani jua limekuwa magharibi. Lakini tulikuwa hatujamwona Mkadamo wa shamba, kwani sisi tulifikia nyumba ya kilimani naye anakaa chini. Bassi baadaye akaja. Naye ni yule yule mliyesikia jina lake kwanza, Bwana Abudu.

Bassi huyu ukatukaribisha sana. Tukamwuliza kama tutaweza kupata mchele, akasema kama lipo duka chini la Banyani. Bassi tukafuatana na huyu Msimamizi kwenda kununua mchele, tukapata mchele kadri ya pishi nne. Msimamizi akatuazima vyungu na makombe, na killa tulilohitaji akajaribu katupatia.

Bassi jioni tukasema sala tukaisha, tukala, tukalala. Assubui kulipokucha, ikawa kutawanyika tena kutembea, wengine Mwanda kutafuta samaki, wengine kuzunguka kutafuta kuku, na wengine kununua mchele, na wengine kutafuta vifao vingine vya tumboni.

Saa a sita tukakusanyika tena tukatengeneza vyakula vyetu tukala. Alasiri tukatawanyika vile vile kutembea, jioni tukarudi.

Jioni tulipokwisha kula tukaulizwa kama twataka kuondoka assubui ama mchana? Wengine wakasema tuondoke assubui na wengine mchana, ukawa mgogoro wa maneno mengi. Lakini waliosema tuondoke assubui walikuwa wengi, likasimama neno lao. Lakini ikawalazimu kupika chakula tupate kula assubui kabla ya kuondoka. Bassi ikawa shughuli ni kupika chakula, na maongezi, na machezo, hatta chakula kilipokwisha kikafunikwa tukalala.

MSIMULIZI. 827

Assubui tulipoamka tukajifunga tayari kwa safari, Mwal. Yustino alikuwa hawezi kitwa kidogo bassi akatangulia pamoja na Mwalimu Yohana Hamisi.

Sisi tukapakua vyakula tukala tukawa watu wa kuondoka.

Tukaenda wote pamoja hatta tulipofika Chichelo tukapumzika. Lakini Mr. Hitchbone alitangulia pamoja na watoto watatu. Tulipoondoka hapo tukaja zetu karibu na Bububu tukapumzika, tukanunua embe tukala. Na wangine wakatuacha pale wakatangulia mpaka Bububu.

Bububu tukawakuta wenzetu waliotangulia, Mr. Mathews akatukaribisha, tukapewa madafu fadhili. Tukakaa pale mpaka saa a tissa, tukaondoka, ndio moja kwa moja tena mpaka nyumbani kwetu Kiinua Mguu.

Jan. 3 Tumeanza kusoma tena chuoni.

Jan. 8 Padre Dale, na Mr. Roberts wamewasili Unguja pamoja na watoto watano wakitoka inchi ya Bonde hawa mabwana wamekuja kubadili hewa siku chache, lakini watoto wamekuja kusoma, nao watoto ni Henry Mdimu, Henry C. Semngindo, Alen N. Juta, Rafael Nyungu, na Predrick Ndiga, na pamoja nao pia amekuja mwalimu Basil Mhada, ajaye kusoma tena pia.

Jan. 1 Achdeacon Maples amewasili hapa pamoja na watoto wawili wajao kusoma, na watoto ni James G. Chigulu, na Mntanje.

Jan. 21 Alituwasilia Rev. Denys Sayite akitoka Dares-salaam, pamoja na Murphy Makamla.

Jan. 24-29 Tumetazamia akili (Examination).

MSIMULIZI. 828

Jan. 29 Ilikuwa arusi ya Alban Njengune akimwoa Amy Linga, na siku ile ile Rev. Denys Sayite, akaenda zake Dares-salaam.

Jan. 30 Ndugu yetu mmoja wa Chama cha Paolo Yohana Hamisi tulimsafirisha aende barra Boride kufanya kazi yake, na safari yake walifuatana Padre Key na Bibi yake, na Mr. Roberts. Na siku hii hatukusoma kwani tulipewa kucheza sababu ya kwisha Examination.

Feb. 3 Archdeacon Maples ameingia ndani ya meli ya Mfaransa, kwenda Ulaya Ingreza.

Feb. 5 Ilikuwa arusi Mbweni kati ya Amini Mvuma na Georgina Stamili. Na siku ile pia tuliambiwa marks za Examination. Waliotokea vizuri katika darasa ya kwanza 1 Arthur R. Mvenya, 2 Leonard Mattiya Kamungo, 3 Isaya Mwalinjila. Darasa ya pili 1 Cherubini Masaninga, 2 Robert H. Awali, 3 Ambrosio Mitande. Katika darasa ya tatu 1 Robert Kamaliza, 2 Rafael Nyungu, 3 Adamu Saburi. Darasa ya nne, 1 Yakobo Matozwe, 2 James Kathibeni, 3 Henry C. Semngindo.

Feb. 6 Archdeacon Jones-Bateman alienda Daressalaam kuangalia watu wa huko na Feb, 8 amerudi. Tena nimesahau kusema kama Jan. 16 Mwalimu Silwano Ngaweje na Yusuf Kasembe wameenda tazama jamaa zao kwa muda kitambo, watarudi. Mtg.

NEWALA.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu, baada ya Salamu nakuarifu habari zetu za hapa. Dec. 3 tumepatwa

MSIMULIZI. 829

na Naige, hao walikuwa wengi kuliko kwanza na juu yote, wa kwanza hawakuwahi kula chakula, walikuta kimekwisha vunwa, bali hawa kinaanza kuota, bassi wamekula chote hapana kilichobaki. Tangu Dec. 3 tulianza kuomba waondoke hawa, tena siku ya Dec. 24 tulijaribu kufunga wote tulio wamasihya kwa ajili ya hawa nzige labuda wataondoka, kweli siku ya tatu yake wote wakaruka wakaenda zao kwa sababu ulikuja upepo pamoja na mvua, bassi wote wakaenda zao. Tena watu wakapanda tena vimeota lakini pia vinaliwa na nzige hawa waliozaliwa hapa, kwani wale waliacha mayayi ingawa wamekwenda wale wakubwa, bass hawa watoto wao wanamaliza kilichopandwa sasa, mwaka huu hatuna buddi kusumbuka sana kwa njaa.

Tena Dec. 16 tulitazamia Examination ya watoto wote wa hapa wa kwanza katika darasa ya kwanza Stefano K. wa pili Atanasio Sh. na katika darasa ya pili wa kwanza Mattiya wa pili Gabriel M. ya tatu Kristopher; wa pili Gabriel L. ya nne Herbert M. Gregdrio, ya tano Isaak N. James K. ya sita Klement M Ghiwalo. Ikasemwa siku kuu ya Tomaso.

Dec. 25 Siku kuu ya Uzaliwa ilikuwa sala kubwa hapa kwa ginsi ya shangwi, watu walijaa tifu, nafasi hapana kikanisa chetu, hatta Wamasihya wangine walikaa nje wakati wa Eukaristi. Kwanza walikaa watu kwa utaratibu lakini haikuwezekana wakasonganasongana wanaume pamoja na wake, tulitumia kikanisa kwani pahali pameharibika katika lile kanisa kubwa linataka kutengenezwa, bass tulikaa kama saa tatu toka saa kwanza. Na tulipoondoka

MSIMULIZI. 830

watoto wakaenda kushindana mpira walipokwisha akawapa zawadi. Na Dec. 26 watoto wote wametoka hapa kwenda kwao kucheza kwa Juma nne. Dec. 27 Mimi na Mwalimu Luke tulikwenda Mkoo kutembea kwa siku chache. Dec. 29 walikuja watoto wa Masasi kutembea sasa wanarudi kwao, na Padre Hainsworth alikwenda Marumba kutembea alikaa siku hamstahara aliua nyama watano, sasa karejea hapa. Na Ijuma Jan. 8 walirudi watoto wote tayari kwa kuanza School Juma atatu. K. Y. M.

SAFARI TOKA MASASI HATTA UNANGU.

Tulipotoka Masasi Nov: 6, assubuhi marra baada ya kutoka Kanisani, (Kwani Padre Carnon alifanya Sakrament ya Eukarist kwa ajili yetu.) Daudi Nakaam, Isaya Nene, Samwili Sulemani, na Waalimu wawili, Barnaba Mtaula, na Gilbert Mpalila, wakatushindikiza hatta Chogawali, ilipotua safari ya watu wa Unangu.

Jumla yetu tulikuwa watu sabaa, Mattiya Sayite, Hamisi, Kumbemba, Akumawindi, na watoto wawili Cherubin na Akida (hawa ndio watakaoka pamoja nami huko Unangu.) Nikaangua madafu mengi pale Mkomahindo na mangine tukachukua hatta matuoni.

Mwenyi safari ni mwana wake Kalanje, naye pia anaitwa kwa jina la babaye Kalanje; na pamoja naye, mna wakuu hawa: Idi (ndiye atakayemrithi Kalanje) Akumitete, Che Chungu, Che Mtolela,

MSIMULIZI. 831

Che Msepala, na Akwikalawe. Na pale Masasi tulipata habari kama Wangoni wanaingojea safari hii ya Unangu waipige; bassi siku ile yule Wadi Kalanje akagawa baruti, fataki, na risasi kwa watu wake, nayo safari yenyewe ilikuwa kubwa wapata watu kama 800 waume tu wenyi bunduki; kwani watu wa Unangu hufunga safari kubwa kuliko safari zote.

Jioni nikaenda kwa Wadi Kalanje nikamwuliza, Je! safari itaondoka lini, leo ao kesho? Akajibu, "Ngoja kwanza nitamwita Jaabu akaulize kwa Waganga wenyi madawa tujuwe tutakavyojibiwa."

Marra Jaabu akarudi akinena, "Wamesema kama hapana hofu yoyote na tuondoke kesho assubuhi."

Nikastaajabu sana: kwani huyu Wadi Kalanje ni Mwiislamu, hushika sala zake zote killa siku, na kabla ya kusali hupiga ashahad.

"Ashahadu la illah illa Allah," na sasa mahali pa kumwomba Muungu, anatuma mtumwa wake kuwaendea Waganga! nilipojibiwa kama ya kesho, nikaondoka.

Assubuhi tukaondoka kusafiri tukaenda mwendo wa siku tano ya sita tukafika Rovuma, Ah! ikawa furaha yetu sana kupata maji mengi ya kuweza kunywa na kuoga: na ilikuwa furaha yetu killa siku katika siku tulizotua karibu ya Rovuma kuingia mitumbwini na kutembea huko na huko katika visiwa. Na ndege wengi wazuri wakizamia samaki nikampiga mmoja kwa bunduki mkubwa kana bata lakini shingo lake refu kupita shingo la bata; tulipompika hatukuweza kumla nyama yake mbaya, na inanuka sana tukaitupa.

MSIMULIZI. 832

Juma a pili moja ikatupitia mahali paitwapo Lukumbuli; tukapata bahati sana, kwani watu wengi wa visiwani walikuja. Tukajaribu kuwasomea kwanza amri kumi, na kuimba wimbo, na mafundisho ya kuwaeleza amri zile, watu wakasikiliza sana na zayidi wakaifurahia sana amri ya tano, (maana palikuwa na vijana, na watoto wengi.)

Tulijaribu sana kuweka tofauti kati za siku zingine, na Juma a pili kusudi yao wale watu wa safari. Kwa hiyo tukaacha kujenga kibanda cha kulala killa Juma a pili. Na tukatoka saa pili matuoni kuanza kusafiri, na safari imeisha ondoka saa edashara assubuhi. Nawashukuru sana watu wale wa safari kwani killa Juma a pili walitungojea hatta tulipokwisha sala zetu zote.

Sikuweza kufanya jambo lolote kwa watu wa safari, illa Juma a pili moja naliwasomea amri kumi jioni matuoni: Kweli za kinwa ndizo nyingi. "Hayo kweli Mwalimu."

Tulifika miji ya mwisho ya Rovuma tukanunua vyakula vingi kutosha kwa siku kumi hatta kufika Unangu, lakini watu wengi hatukupata chakula maana miji yote imeingiwa na njaa, miji yenyewe ni Makanya, Pa Charnba, Mtotela na Mpinga Wandu.

Siku ile tukakuta watu watokao Unangu Ah! ikawa furaha sana kupata habari za mjini wakatarifu kama vyombo vitatu vimekamatwa na Wazungu huko Nyasa, illa cha Sultan Kalanje. Na watu sita wa Kalanje wamenyang'anywa bunduki zao na watu wa Msumba, na Sultan Kalanje anataka mwende

MSIMULIZI. 833

zenu upesi kwani atapeleka vita kupiga miji ya Wanyasa. Bassi ndipo tulipohimiza sana mwendo wa toka Makanya ni wa siku kumi hatta Unangu, siswi baada ya kuambiwa haya, tulikuwa tukiondoka usiku saa saba, kwenda sana sana, hatta tukafika Unangu kwa siku tano toka Makanya ya mfalme Kungolonje.

Na safari yetu ilikuwa na watoto wengi, na waanake wengi, na wangine wazee.

Tuliona kibanda tulicholala na Askofu Smythies mwaka wa 1891, kwani twalijenga kwa miti mikubwa sana. Na njia yote toka Makanya hatta Unangu imejaa maua mengi mengi kwani miti ndio kwanza ichanue, meupe, mekundu na mengine rangi ya manjano, na mengi ya samawi.

Tulipofika Lisombe ikawa baridi kali sana watu wengi hawakuweza kwenda, haswa Mattiya alilala chini akitetemeka, na mkewe Idi pia, halafu wakakota moto; wakapata heri. Lisombe sasa limebaki lile jabali tu, tukastaajabu sana, kuona jabali lile lililojaa umati wa nyumba za watu; sasa limeachwa tupu, na mashamba yale yaliojaa vyakula, yamefunikizwa na magugu. Ah! ndizo habari za Afrika. Yote haya yametendwa na Che Mataka ndiye aliyewaondoa: sasa wamehama wanakaa Chitaga wameshika mguu kwa Sultan Kalanje aliyewaokoa.

Tumefika wote salama salimini. Tumewakuta wa hapa wote na afya, ndiwo Dr. Hine, Mr. Bradshaw na Mwalimu Gabriel Katoma, ndio wakaao hapa Unangu. Y. B. A.

MSIMULIZI. 834

MBWENI.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi, salaam sana, na baada ya salaam nakuarifu habari hizi.

Shamba la Mbweni. Jan. 4, Padre Key akafunga safari ya kwenda kutazama Kichelwe, palipo kazi ya Padre Denys Sayite. Na Padre Woodward akaja hapa kumshikia kwa kitambo tu.

Jan. 8, mtoto wa Aaron Amwitamo akafariki. Alipokuwa hawezi akapelekwa mjini Hospital, lakini panapo siku hii akafariki kule kule mjini, alasiri akaletwa hapa, na jioni akazikwa. R.I.P.

Jan. 13, Padre Key akarudi kutoka Kichelwe.

Jan. 16 Watoto watatu wa Shamba William Kingango, na F. Ibrahimu, na Faraji, wakatoka katika kazi ya School, wakapewa kazi. Faraji anafanya kazi ya upishi hapa, hao wawili wanafanya kazi mjini kwa Mr. Lister.

Jan. 22 Watoto wa Shamba na watoto wa Kilimani, pamoja na Padre Key na mkewe, na Miss Clutterbuck na Miss Phillips, na mimi, na mwalimu Sheldon na Edward, tukaenda kushinda Chukwani. Bwana Sayidi ndiye aliyetoa ruksa ya kuwa twaweza kushinda kule. Bassi tulitoka hapa assubui saa ya pili, tukafika kule mnamo saa tatu unuss. Tulifurahiwa sana, watoto walijifurahisha kama wawezavyo, wakiangalia killa kitu. Hatta mnamo saa a kumi Bwana mwenyewe akaja na watu wake, akampa mtu wake kuwaletea Wazungu madafu manne na barafu mabonge matatu. Naye alikaa robo saa tu, marra akaenda zake. Na sisi tukajifunga tukarudi zetu Mbweni.

MSIMULIZI. 835

Jan. 23 Akaokotwa mtoto mmoja hajui atokako wala aendako. Akasema kama kaibiwa Bagamoyo, bassi anakaa hapa Unguja na bibi yake tu, Bwana wake kafungwa mjini kwa sababu ya watumwa. Yule bibi yake hamtunzi vema, anamsumbua sana. Bassi usiku mmoja akaibiwa na mtu mmoja, akaja naye hatta mpakani mwa Shamba hili, akamweka penyi mwembe, akamwambia ngoja nikachukue samaki pwani tukiisha twende zetu. Bassi yule mtoto akalala pale asione mtu, hatta siku ya pili athuuri akamwona James Chorola akamweleza haya. Bassi tukampelekea Padre Key, naye akampeleka kwa General iMathews, bado hatujasikia habari zake.

Jan. 28 Mtoto mwingine Yusuf Kamange akapelekwa mjini kufanya kazi kwa Mr. Lister.

Jan. 30 Padre Key, na mkewe wakatoka hapa kwenda kutembea Bonde kwa mwezi mmoja, hapa anashika Padre Woodward mahali pake hatta arudi.

Mwanzo wa mwezi uliopita amekuja mtu mmoja na mkewe na watoto wake wawili anatoka Kepi, anakaa hapa, sasa watoto wake wanasoma pamoja na watoto wa Shamba. Tena tunasikitika juu ya mkewe Charles Farijalla, hawezi ugonjwa wa kupotewa akili, akapelekwa mjini Hospital Juma iliyopita, sasa twasikia hajambo kidogo, anafahamu maneno ya watu kidogo kidogo. Lakini aliyezidi ni Elizabeth Shanti, yeye ana wazimu; pengine huwa na akili kidogo, lakini sio sana.

Mwanzo wa mwezi November alikuja Padre Radford kukaa hapa na kumsayidia Padre Key, yupo hatta leo, tumesikia kama labda atarudi Mkunazini alikotoka, kwani anatakiwa kule.

MSIMULIZI. 836

Kilimani. Dec. 24 Miss Mills akawa hawezi. Bassi homa ilimshika kwa Juma nzima; asiwe hajambo; akapelekwa Kiungani kubadili hewa.

Jan. 7 Miss Clutterbuck na bibi mmoja wa Hospital wote wakawa hawawezi. Huyu bibi wa Hospital alikuja kumtunza Miss Mills, bassi akabakia hapa homa iliwashika, mwisho ikawazidi wakapelekwa kukaa pamoja na Miss Clutterbuck. Bassi wote mjini Hospital, maskini Kilimani! Watoto walikaa na waalimu wawili Sheldon na Edward Koongani kwa juma nzima; baadaye Miss Clutterbuck akawa hajambo kule Hospital, bassi akaja Kilimani, akabaki Miss Mills. Kwani Miss Mills Kiungani hapakumfaa, akapelekwa Hospital, akaonekana hana afya ijapo akikaa Hospital, bassi panapo Jan. 24 akarudi Kilimani. Hana nguvu na juu yote ana majipu machavuni. Sijui kwa nini, mahali hapa Kilimani, panawafaa watoto kuliko bibi zao. Watoto wanapata afya kuliko walipokuwa Mkunazini, wanakuwa hawawezi wengine wao, lakini sio kama Mkunazini. Ghuo chao kinachojengwa karibu kwisha sasa: kizuri sana. Twataka kiishe upesi, kwa sababu sasa watoto wa Kilimani na wa Shamba wanasoma katika Chuo hiki cha Shamba, nacho kidogo hakina nafasi; watoto wa Kilimani ni 33, na wa Shamba ni 35 bassi haifai; Darasa tatu naziweka ndani na zingine tatu naziweka nje: bassi wale wasomao nje wanacheza tu kwa kutupa macho huku na huku. Kwa kuwa nafundisha watoto hawa peke yangu (mwal. Sheldon huja ajionapo mzima, kwani yeye mwajua ni thaifu,) bassi watoto wadogo wote wasomao A. B. Ch. asubui wanakwenda Kilimani kufundishwa na Miss Clutterbuck ao Sheldon: na pengine alasiri darasa ya tatu wanafundishwa

MSIMULIZI. 837

Kilimani na Miss Clutterbuck; watoto wadogo wanafundishwa assubui tu, alasiri hawaji kusoma, inawachosha. J. B. M.

LIKOMA.

Salamu kwa Mtengenezaji wa Msimulizi. Baada ya Salamu, nakuarifu habari ndizo hizi. Panapo Oct. 8 ilikuwa harusi ya Barnaba Mtipende na Kuundani mwanafunzi tu. Oct. 9 bwana Archdeacon na Mr. Corbett walifika hapa wakitoka Unangu wakati wakurudi walipitia kwa Malinganile, na Malinganile, alipowaona alitaka kuwaua wote wasafarini kwa ajili ya mtu wake aliyemwiba Chamba, Ah! kwa shidda waliokoka mkononi mwa Malinganile. Oct. 14 bwana Corbett alikwenda Chinyanya, kuwatazama Wamasihiya wengine waliochelewa kuja Kanisani, wakati ule Chamba alikuwapo, marra hiyo bwana Corbett alirudi kuja kumwarifu bwana Archdeacon kama Chamba nimemwona; bwana Archdeacon akamwambia aende kumfunga Chamba, marra hiyo watu wa kazi wakaitwa kufutana naye Mr. Corbett, School tu ndio haikwenda. Walipofika kule bwana, marra hiyo Chamba yuko mkononi, haya lete kamba, Ah! lete kisu tukate, Ah! fungua kamba bwana, marra wakaja watu wakamwokoza Chamba; lakini ajapo walimwokoza Chamba, vijana hawakukubali kushindwa. Mahali pa Chamba walimkamata Mkabula mkubwa wake, kwani ndiye aliyejaribu kumwokoza huyu Chamba. Wakaja naye hapa wakamwuliza uliza, kwa nini umejaribu kumwokoza

MSIMULIZI. 838

Chamba? naye kaiba mtu wa Malinganile, karibu tungeuawa kwa ajili yake Chamba, tena umempiga bwana Corbett. Akamwambia kwa sababu umefanya hayo, wewe utachukua mbuzi 2, na Chamba atatupa mbuzi 5 na sisi tutachukua tukakomboe bunduki yetu, kwani walimpa Malinganile kuishika. Bassi mbuzi hizo zikaletwa pamoja Mkabula akafunguliwa, na hivyo mtwana aliyemwiba Chamba akawapa watu wa Kalanje kumpelekea Malinganile, na taka moja, mbuzi zote sabaa zikapigwa visu, nyama yake akawagawia Wamasihya na Wanafunzi wa mijini.

Oct. 23, ilikuwa harusi ya Lungunya naye ni mwanafunzi mkewe ni Mmasihya jina lake Harriet Mantilunda Oct 24 harusi ya Petro Chibwana na Kufatonja. Oct. 27 ilikuwa harusi ya Makomela na Hora Chilimbilani.

Oct. 26, alitufikia Emy Uledi akitoka Pachia alikuja kwa matembezi. Oct. 27 zalifika Gunboats, H. M. S. Adventure na H. M. S. Pioneer zikaleta khabari za huzuni, ya kuwa Mr. Mackay alikamatwa na simba, huyo simba alipigwa bunduki alipopigwa alianguka chini, lakini hakufa mzima, W. E. Mackay akamwendea, marra hiyo simba akamrukia binadam chini, mnyama juu, W.E. Mackay akamwita mtwana mmoja aliyefuatana naye ampe bunduki akampa akanyosha mkono wake mmoja, masikini bwana mkono mmoja ulishikwa na simba akampiga simba, akafa. Usiku kwa usiku tukachimba kaburi tukachimba wee mpaka saa 12 za Assubuhi ndio Oct. 28, mabaharia watupu waliomchukua kuja naye hapa tangu makeputini wao hatta baharia swafi tupu wote. Bassi pale zikanenwa sala za kuzika, Keputini

MSIMULIZI. 839

akaamrisha kupiga bunduki, marra tatu tu zikaamrisha. Ukisikia bwana kama ni bunduki moja, kumbe ni zayidi ya moja. Wote tuliochimba kaburi pamoja twalikuwa watu 15. Keputini wa H. M. S. Adventure Keputini wa H. M. S. Pioneer wakatoa ngweje kutupa tuliochimba kaburi kula mtu alipata Rs 6.

Oct. 30 ilikuwa harusi kati ya Yakobo Kabefu na Peyawa. Nov. 19 Likoma yote ilikusanyika hapa pa Chipyela kwani Mr. Nicoll aliita watu wasikie maneno yake. Kusema tangu sasa visiwa viwili Likoma na Chizumulu vimo mkononi mwa mfalme wetu Queen Victoria, hapana kunyweshana pande (mwai). Mtu akimnyweshwa mwenzake, na yule mtu akifa atafungwa miaka 5 kwa "Fort Johnston." Mtu aliyesingiziwa akisema mimi nataka kunywa pande atafungwa miezi 9 na yule aliyemsingizia mwenzake atafungwa mwaka mzima. Wala hapana kuombeza maula (kupiga bau). Juu ya watumwa alisema aliye na mtumwa hana ruhusa ya kumwuzwa mtumwa wake illa akae naye. Pembe ruhusa kununua billa watumwa marufuku kabisa. Nov. 20 alifika mwalimu Yohana Chanamila akitoka Chizumulu kuja kumwaga bwana Archdeacon. Nov. 22 alianza kugeuza visogo lakini hakuweza kwenda kwani bahari ilichafuka (Mwela) kwa hivyo hakwenda. Nov. 23 assubui ndipo alipokwenda zake Chizumulu. Siku ile ile bwana Nicoll aliingia ndani ya Wissman pamoja na askari zake aliowachukua, pamoja naye Petro Ch. Kufatonja. Yakobo K. na Peyawa mkewe, Monika Kanyopolea na watoto wake wawili kwani mumewe aliisha kutangulia kufanya Station kule, na Zoe Kusingati kwani mume wake alimwacha kule

MSIMULIZI. 840

kumpikia Mr. Sim, tena Wallace B. Chinkula aenda kumpikia Mr. Sim, na Suleman Kilimani, aenda kumpikia Mr. Nicoll. Nov. 27 ilianza kunya mvua Nov. 28 saa tissia kamili ilikuwa ubatizo wa mtoto wake Lawrence Chiluali na Neema Chiluali jina lake Richard Corbett Chiluali. Nov. 29 assubui zilipokwisha Sala za assubui ilikuwa harusi kati ya David Saba na Mantisauka naye ni mwanafunzi. Nov. 27 Mr. Butler alikwenda ng'ambo kuwatazamia watoto akili, Nov. 30 udipo aliporudi hapa, Nov. 29 alitufikia bwana Smith akitoka Chizumulu. Dec. 1 alikwenda zake Chizumulu.

Bwana Archdeacon Maples ameondoka leo hapa Dec. 6 pamoja na vijana wawili waendao kusoma, majina yao James G. Chiguru, wa pili Mntanje nduguye ni huyo Williamu B. Mpota, na bwana Archdeacon aenda zake Ulaya Ingereza. Dec. 5, mtoto wa Lawrence Chiluali kafariki, ndiye Richard Corbett Chiluali ndizo habari.

Dec. 5 C. Janson ilifika hapa, ikaleta khabari za huzuni za kufariki kwake ndugu yetu, nathani wote wa Upelekwa wetu mmemjua Clara Msichoke aliyekuwa mkewe marehemu Richard Kanyema, Ah! masikini kitoto kimesalia peke yake. Mwalimu Augustine Amapundi anakitunza. Alifia Mtengula mahali alipokuwa akifundisha, mwili wake ukachukuliwa mpaka Msumba, ndipo mahali ulipolala mwili wake. A.T.M.

CHITANGALI.

Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Baada ya salama nakuarifu habari kidogo za Chitangali. Jan. 4, Padre Wetu alifunga safari kwenda Mwiti kuwatazama jamaa pande zile akashinda mda wa jumaa mbili akitembea akiongea na watu walio karibu na Mwiti. Siku hizi watoto wa nzige wanaanza kuenea pote, wangine hatta sasa hawatoki mashambani. Jan. 26, Padre amepata santuri (musical box) imetoka kwa Askofu wa Lincoln, kazi ya Ulaya Jermani, ina sauti zayidi ya kumi na tatu watu wengi wa hapa Mlolela Waliitwa kuja kutazama kwani ni ya namna ya peke yake. Padre alitusomea taratibu ya marks za watoto waliotazamiwa kusoma.

Darasa ya kwanza 1. Gideoni Kawanga, 2. Julius Msoma, 3. Enoch S. Darasa ya pili 1. Malawi, 2. Silwano Malemla, 3. Daniel Matola. Kwa School girls 1, Mary A. Njilolaga, 2. Durham Akusauchi, 3. Dorothea Akwalachia. II Class 1. Achilaudana, 2. Selina Akusigala, 3. Blandina A.

Hatuwezi kutazamia darasa zote kwa kuwa watoto wengi wametawanyika kwa sababu mama zao wakaa mbali. Feb. 10, Ilikuwa Taratibu ya Ubatizo wa mtoto wa Andrea Sawasawa na Margaret Achiwalukonji, Feb. 11 Alituasilia mwalimu Petro H. Musa

MSIMULIZI. 842

akitoka Newala kwani alikuwa mgonjwa wa mguu ulikuwa na kidonda, bassi akapelekwa Newala kufanyiwa dawa. Siku ile ile Feb. 10, Mzee Barnaba Nakaam aliitwa kwenda Masasi kwa Mzee Machinga kuhukumu juu ya watu waliomua mwenzao kasidi Feb. 27, Juma a tano ya Majifu assubuhi baada ya sala ya assubui ulikuwa mkutano kwa Wamasihiya na Waanafunzi mashauri juu ya Kwaresima ginsi ya kufunga kwa kuwa hawawezi kufanya kawaida yao ya siku zote kwa ajili ya njaa, bassi Padre akatoa mashauri kwa watu wakakubali wote kiisha killa mtu akarejea kunako masikani yake. D. U.

NEWALA.

Mtengenezaji wa Msimulizi salamu, na baada ya salamu najaribu kukuarifu habari zangu kidogo, safari ile iliyopita nalikuambia kama wale nzige wa kwanza walioacha mayayi na yale mayayi yakatokea watoto wengi sana, bassi wale watoto ndio walioharibu sana vyakula lakini siku hizi wanapungua hawaonekani marra kwa marra wanaonekana mahali mahali si wengi sana.

Na siku hizi pana ugonjwa ulioingia wa kitwa, watu wanaugua marra kwa marra naona kwa sababu ya baridi, ao kwa sababu masika, kwani masika killa siku watu ni thaifu tu. Hatta Padre J. Hainsworth anakuwa mgonjwa siku hizi marra kwa marra kwa homa.

MSIMULIZI. 843

Panapo Feb. 2, Mzee Che Matola alikwenda Mkoo, naona utauliza Mkoo wapi? Mkoo ni walikolima watu mwaka huu karibu wote, bassi huyu Mzee Che Matola alikwenda kutembea na kutazama ginsi kulivyo, na hapa mjini watu wapo lakini si wengi, wote wako kuko huko hapa huja Juma a mosi tayari kwa Juma a pili, na Jumaa tatu, yake hurudi Mkoo ao siku ile ile.

Na Mwalimu Petro H. Musa alituasilia hapa Feb. 2, alikuja kupata dawa kwani alikuwa hawezi mguu. Bassi akachukuliwa mpaka hapa, na hapa alikaa yapata Juma unussu, na halafu yake wakaja watu wa huko Chitangali kumchukua kwani hawezi kwenda mwenyewe, hatta alipofika napa pia alichukuliwa. Panapo Feb. 3, tulipata huzuni kwani Muungu alipenda kujitwalia ndugu yetu Gideon Masapula mtoto wa Daniel Lusenga ugonjwa wa siku tatu tu tukamzika hapa Makonde katika kiwanja chetu saa kumi. R. I. P.

Na Jan. 31 alituasilia hapa Mwalimu Silwano Ngaweje, Yusuf Kasembe wanaotoka Unguja, tulifurahi sana kuonana nao. Na huyo mwal. Silwano hakukaa hapa kwa siku nyingi akaenda zake kutembea Mkoo kwa juma moja tu. Na Yusuf hakukaa hapa siku nyingi akaenda zake Masasi kwa sababu jamaa zake na mama yake wanakaa Masasi, kitambo.

Nalisema habari za Makwangwara katika Msimulizi uliopita kama walimpiga Msaka, na mtoto wake huyu Msaka wakamchukua kwao Makwangwara mpaka kwao. Bassi mwezi huu wa February ulipoandama akaambiwa aende mpaka kwa mji wa babaye

844 MSIMULIZI.

Msaka akautazame, na watu waliobaki na waliotawanyika, na waliopotea, akapewa askari ndio Makwangwara wapata 10, wapate kumlinda njiani na mtoto huyu wa Msaka jina lake Mtepa, na alipokuwa akipelekwa huko Makwangwara aliambiwa akiisha kuangalia watu arudi tena huko Makwangwarani lakini mimi naona harudi. Tena si mimi tu hatta watu huthani hivyo kama harudi, na njia aliyopitia wakati huo wa kwenda huko kwake kwenyi mji wa babaye alipita ujia ya hapa Newala pamoja na Makwangwara. K. Y. M.

MASASI.

Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Baada ya salamu nakuarifu habari chache tu. Kanisa letu limekwisha nalo zuri sana, limejengwa na Wamasihiya na Waanafunzi.

Tulitumaini kama mwaka huu tutapata chakula lakini nzige zimeharibu chakula chote, balli mtama umepona kidogo. Siku hizi chuo chetu kimejaa watoto kwa sababu kwao wanakimbia njaa tu.

Jan. 30, tumepata kucheza sababu tumesikia kama Yustino Mkandu ni Msomaji, na siku ile ile Leonard Mkwasomba alipata mtoto balli si riziki.

Tena Makwangwara wengi wamepita hapa wanaenda pande za Lilulu. Watu wa hapa walienda Ungoni, lakini walipofika huko tumesikia kama mfalme Sonjela hakupendezwa kuwaona watu wa

MSIMULIZI. 845

Masasi. Sababu amesikia kama watu wake wanapokwenda Masasi, hupata chakula cha shidda kabisa, na killa mji wanawafanyia mzaha tu. Bassi kusikia tu Sonjela amekasirika sana, na Wafalme wa hapa Masasi walipeleka chumvi lakini ameipokea kwa kinyongo. Bassi sasa iliopo ndio twatazamia vita.

Feb. 25, Padre Carnon na mimi na watoto 9 tulikwenda matembezi pande za Mapale, Mpangule; Nangololo hatta Mwitwi, Feb. 27, tukarudi zetu hapa. Feb. 28, tulienda nyuma ya mlima Mtandi pale pale mahameni petu kuwaombea roho za ndugu zetu waliofariki, maana leo haswa ilikuwa ukumbusho wa Padre wetu Taylor aliyefariki March 1, 1891. K. M.

MBWENI.

Mtengenezaji wa Msimulizi salamu, wa baada ya salamu nakuletea habari zetu za hapa nazo chache kabisa uwe rathi, nazo ni hizi.

March 1 alituasilia Bibi Key pamoja na watoto wawili wa pande za Bonde nao watoto ni hawa: Angelina Machaku, na Mhunge ni mtoto wa pande zile zile wazee wake wamefariki dunia wala hakupata mtu wa kumtuza. Ndio sababu Bibi Key amemleta hapa Mission. Angelina Machaku kaja kusudi azidi kujifunza kusoma elimu.

Narejea kwa Padre Key kwani yeye na mkewe walikuwa njia moja wakatengana njiani, Padre akashika

MSIMULIZI. 846

njia kwa Dar-es-Salaam kuangalia Wamasihiya wa kule, na pamoja na kumbatiza mtoto wa Sbemasi Denys Sayite jina la mtoto ni: Chrusostomo Henry Denys, alizaliwa Feb. 18, March akaturudia Padre Key. March 18 akatuaga Padre H. W. Woodward pamoja na Bwana G. Dale wakienda zao Magila, kwani Padre Woodward alishika kazi ya Padre Key kwa mwezi unussu. March 7 tulitoka watoto wa Mbweni na nussu ya watu wazima wa shamba kwa maziko yake ndugu yetu Mary Selina Abdallah R. I. P. Ameacha kitoto chake wa siku 4 tu! naye analewa na mama Juma Mbweni.

March 25 Siku kuu ya Kuhubiriwa Bikira Maryamu na pia ni siku wanayoshika wa Chama cha Watakatifu wote. Nao walikusanyika, saa 1 Usharika Mt. ukafanyika katika Kanisa la Bikira Maryamu kwa mathbahu kubwa na siku hii tulimtabaruku msalaba wake. Mzuri sana, mabibi watatu wa pande za Ulaya Ingereza wametupelekea. Naswi siku hii hatukushika School, alasiri tukaenda kwa "Shamba la Ulaya" kujiburudisha tu.

April 3, Tulipata hatari katika chumba chetu cha taa, bali tulitenda kwa busara ya kuuzima moto. Kwani debe zima limefunguliwa tu halijaanzwa kutumiwa mafuta yake. Mtoto akatupa ndani ya debe kile kibiriti chenye moto, ache bassi mafuta yatende kazi, zilikuwa saa tatu za usiku.

April 2, Alituasilia Bibi Boyd hapa alikaa naswi siku tatu; papo alishika kazi ya Bibi Phillips kwani yu Hospital mgonjwa. Naye April 14, ashika njia

MSIMULIZI. 847

kwa Mvita kupunga hewa.

April 4, alituasilia Archdeacon Farler, wote waliomfahamu zamani tulifurahi kumwona ndio habari. Tena tuna furaha sana sisi wa Chama chake Mchungu aliye Mwema, tumezidi kuongezeka. April 5, Miss M. A. Boyd jumla yetu 30. Na wawili wamelala katika Bwana ni E. M. Bennett na Mildridt Furahani. R. M.

KICHELWE.

Naona mtapenda kusikia habari kidogo za mahali hapa. Imekuwa mwendo wa saa nzima kutoka Dar-es-Salaam kufika hapa. Zamani hapakuwa na kanisa, illa watu walikuwa wakifanya ibada yao ndani ya ukumbi wa nyumba ya mwalimu Denys. Hatta hatimaye ikaonekana hapatoshi sababu watu huzidi killa siku kuja kufundishwa maneno ya Muungu, na wengi waliofanywa Waanafunzi na kathawakatha wamebatizwa na wachache waliotiwa mikono. Bassi ikawa watu hukusanyika nje ya mlango wa mwalimu chini ya miembe, kwa sababu ukumbi haukuwaweka.

Mwisho wa mwaka 1894, watu wenyewe wakaona kheri wajenge kanisa lao, bassi wakaenda kukata miti ya kanisa na wakalijenga likaisha. Padre Key akaenda hatta Jan. 6, 1895, likatabarukiwa, likaitwa kanisa la Epifania, zuri sana

MSIMULIZI. 848

kanisa hili balli halina Fonti wala mimbara (pulpit). Lakini hatta wamejenga hili kanisa. Vile vile watu hawatoshi kanisa laonekana dogo kwao.

Feb. 18, Rev. Denys Sayite amepata mtoto mwanamume, ndiyo furaha kubwa. March 5, Padre Key na Miss Mills na Hugh 8. Mtoka wametuasilia hapa jioni tulifurahi mno kuwaona.

March 6, Padre Key akatoka na mpagazi mmoja akaenda mahali panaitwa Mtoni, mwendo wa saa mbili kutoka hapa, na hapo wapo watu wengi waliotoka shamba la Mbweni. Watu wapata 80 walimjia kumtazama, naye akawahubiria, kiisha jioni akarudi.

March 7, assubui ilikuwa sala ya Eukaristi Takatifu, kiisha ikawa Taratibu ya Kuwafanya watu Waanafunzi, waliopewa misalaba ni watu 26. Marra ibada ikiisha, Padre Key na Miss Mills wakafunga safari ya kuja Unguja, bassi nikawa sindikiza mpaka mjini Dar-es-Salaam, wakaingia ndani ya meli ya Kidachi s.s. Kaiser tukawaaga sisi tukarudi shamba ndio Kichelwe pande za Msumbazi.

Nikastaajabu sana juu ya ibada za kanisani za assubui na jioni, kwa sababu watu hawa wamefundishwa sana kwa moyo, na wote ni watu wazima na wengi wazee lakini wamefunzwa vizuri kusema sala za kanisani, husema wote kwa sauti moja na huimba pia wala kanisa hili halina waimbaji (choirs) kwa sababu hawa watu wenyewe watosha kuwa waimbaji. Wala ukiwaona kanisani hungethani hawa ndio wale wale akina mama wa Kondeni kwa ginsi walivyojua mambo ya

MSIMULIZI. 849

dini ya Kimasihiya. Bassi hii inaonyesha kama mwalimu wao wa dini anawashughulikia kwa bidii, kwa nguvu zile apewazo na Mwenyiezi Muungu.

Tena hapa watu wamelima sana mashamba, lakini nzige zilipokuja zimeharibu mpunga, mihindi, mtama, billa mhogo na mbaazi ndizo ziliobakia. Wallakini kwa miezi hii miwili mitatu nzige hazipo, na watu wamejaribu kupanda mihindi, balli wapo wengi watoto wa nzige hawajaota mabawa, hao ndio tunawahofia.

Siku moja naliondoka hapa kwenda Mtoni pamoja na mtoto mmoja jina lake Mzee, tulipofika Temeke nikaona njia imefunikizwa na watoto wengi wa nzige, kwa kuwatazama huonekana rangi nzuri, lakini uzuri huu halafu huleta machozi. Tukavuka mto unaitwa Mtoni, na inchi yote ya pale inaitwa Mtoni, tena tukavuka mwingine, tena tukavuka mto wa tatu jina lake Mvua nguo. Bassi tukafika mahali Mtoni, nikaenda kwa mkubwa wa pale jina lake Mtawanga, nikamwambia nataka nione mahali watakapojenga kanisa lao, akanipeleka nikaona miti mingi imewekwa tayari. Nikazunguka kuwatazama watu, hatta nikaenda hatta mto wa nne jina lake Mzinga Saba. Kiisha saa nane nikarudi Kichelwe.

Sasa Mtoni wanajenga kanisa, wallakini mwalimu hapana. Tena kuna watu wengi mahali panaitwa Kisiju, mwendo wa siku moja unuss.

Tunasikitika sana juu ya mwalimu Denys sababu yu mgonjwa wa kifua, bassi hatta safari za kuzungukazunguka katika miji iliyo mbali ni shidda kwake.

Tena furaha kubwa iliyompata mwalimu ndio hii, amewaona nduguze wawili mume na mke nao ni watu

MSIMULIZI. 850

wazima; Ah! furaha bora mno hiyo! Nao wanakaa pamoja naye, amewafundisha habari za Anjili hatta wamebatizwa.

March 17, ilipigwa mbiu na wana B mkubwa Gavanori (Governor) wa Dar-es-Salaam, kunena, Mwezi wa Ramathani ukiisha, hatta ukiandama mwezi wa mfunguo mosi, hala hala Mwarabu, Baniani, Mhindi, Mgazija, Mmanga, Mswahili, Mmanyema, Mnjolinjoli, Wanyamwezi na Wazaramo, mwenyi mtoto mume ao mke, lazima ampeleke Bomani, wasomeshwe Kidachi hatta wahitimu ilimu pia. Na asiyempeleka mtoto wake maneno kwa bwana mkubwa Gavanori.

April 4, tumefurahi kumwona Padre Simpson amekuja kututazama kwa siku mbili kiisha akarudi Zanzibar.

KIUNGANI.

HABARI zetu za safari hii chache sana. Illa twashukuru kwa kuwa tu hayi wote, na tujaliwe kuwa na afya zayidi.

Feb. 17. Watoto wawili wa chuoni kwetu huku tuliwapeleka kufanya kazi mjini ni Isaak Mayunga na Martin Kaluma, wanakaa kwa Mr. Lister, Mkunazini.

Mwalimu Hugh S. Mtoka alikuwa mgonjwa sana, aliugua karibu mwezi mzima, naye akawa thaifu sana, asiwe na afya. Bassi daktari akaona heri aende mahali pa mbali punde, labuda huja akapata afya

MSIMULIZI. 851

zake tena; bassi Mar, 5 akasafiri kwenda Mrim, Dar-esSalaam, alikuwa akikaa kwa Rev. D. Sayite, Kichelwe. Akakaa huko kadri ya juma tatu nzima, hatta kunako March 26 akarudi tema. Na ndani ya meli ile ile aliyojia, walirudi pamoja naye watoto wawili Silwano Ngaweje, na Yusufu Kasembe, wao wametoka pande za Mgao Lindi walienda angalia jamaa zao.

Tena siku ile aliposafiri mwalimu Hugh Mar. 5. mtoto mmoja Yohana W. Akupata alianza kushika kazi ya upishi papa hapa.

Mar. 30 Tulifurahi sana kumwona Rev. Farler, akitoka kwao Ingreza kuja kuangalia tena pande hizi za Afrika ya Mashariki. Naona wengi sana wanamjua walio hawapo hapa leo Kiungani, kwani ndiye rafiki yetu wa zamani. Alikaa sana Kiungani zamani, akawa Bwana mkubwa wa hapa. Lakini baada ya kukaa kwa siku nyingi hapa akaenda Magila kufanya kazi kule, nako ndiko alikokaa siku nyingi, halafu akaenda zake kwao. Na kule amekaa miaka mingi, hatta amerudi, akaa hapa Kiungani, watoto wote wamekuwa wageni watupu machoni pake, labuda watu wanne wajuanao naye. Wote aliowaacha hawapo killa mmoja ana nyumba yake, na wengine wamesafiri. Lakini tumefurahi sana kumwona tena. Wengi nao mnakumbuka studies (vyumba vile vya kusomea) zile za kwanza zilizo karibu na kanisa, zilioungana kidogo na dari ile tunapowekea kuni. Na wageni tuliowakaribisha yapata marra mbili tatu kuangalia mchezo wa Vitali wanakumbuka dari ile ilipojengwa nyumba ya Vitali,

MSIMULIZI. 852

bassi pale pale kimejengwa chumba kikubwa punde, ndio chuo chao students ndio hao wanaosoma tayari kwa kazi ya Uhudumu Kanisani], chumba chenyewe kizuri, na boriti za chumba ni vyuma vitupu, nayo imejengwa upesi upesi mno, sasa wanamaliza tu.

Tena nyumba yetu hii kubwa ya kulalia, boriti zile za zamani za miti inaondolewa, na kutiwa vyuma.

April 1, Usiku ulikuwa Ubatizo hapi wa mtoto wa Mwalimu Clement Kathibeni, kwani siku za karibu karibu hapa amepata mwana, na jina lake Yohana Mikael.

April 5 Rev. Simpson amesafiri Dar-es-Salaam kwa siku chache.

MSIMULIZI. 853

MAREHEMU REV. GEORGE P. K. DuBOULAY.

April 1. Tulipata habari ya huzuni sana. Ilikuwa sim kutoka Tanga ndio kunena kama Rev. G. DuBoulay amefariki. Huyu aliingia katika "Mission" yetu mwaka juzi 1893. Amefanya kazi kwa miaka miwili. Huyu alikuwa amejua na marhemu Baba Askofu wetu tangu kwao England, kwani huko kwao alikuwa akifanya kazi chini ya Kasisi mmoja aliyejuana sana na Baba Askofu aliyefariki.

Bassi kuja kwake hapa akakaa Kiungani akimsayidia Archdeacon Jones-Bateman hapa. Alikuwa mwalimu wetu. Akapatana sana na watoto wa hapa. Naye alikuwa na bidii sana ya kujifunza Kiswahili akajua. Hatta palikuwa na wakati Bwana King aliposafiri Bombay, yeye alikuwa akifundisha watoto kuimba. Wakati mwingine Mbweni hakukuwa na Kasisi, yeye akaenda kuwa mkubwa kule Mbweni kwa muda kidogo. Alipenda sana kuongea na watu na kuuliza hali za watu, na mtu wa kusayidia sana, na rafiki wa wengi. Lakini baadaye akaamriwa aende pande za Bonde, akafanye kazi Misozwe. Na huko ndio Muungu alikomtwa katika kazi yake. Bassi kufa kwake kumekuwa huzuni kwa wengi walio rafiki zake na waliomjua. April 2, ukafanywa Eukaristi Mt. kwa ajili ya roho yake. Kwa kumtii Muungu ameacha kwao akaja kufa, "Muungu aliyemwita ampe raha na amani ya milele." R. I. P.

MARHEMU BIBI JOSEPHINE BARTLETT.

Huzuni iliotuangukia April 10, ndio kufa kwake Bibi Bartlett. Wengi sana mno tunaomjua katika upelekwa wetu, kwani waalimu wote wanaofundisha katika Stations zingine zingine za upelekwa huu karibu wote ni watu waliosoma Kiungani, na hatta watoto wangine

MSIMULIZI. 854

wa barra wanamjua, kwani killa mwaka huja wakasoma Kiungani na baadaye hurudi kwao, bassi kwa hivi wanamjua, kwani yeye maskani yake ilikuwa hapa Kiungani.

Amekaa katika "Upelekwa" huu miaka asharini. Kwanza alikuwa akikaa hapa halafu akahamia Mbweni na baadaye akaja kukaa hapa Kiungani. Alipapenda sana hapa Kiungani, (hatta safari yake ya mwisho aliyoenda kwao alienda kwa ugonjwa na hakupenda kuwaagia Watoto hapa, akasema heri twende Mkunazini huko tukamwaga, kwani tukimwaga hapa ataona ukiwa akitoka katika nyumba ya Kiungani).

Alikuwa mama kwa killa mtu aliopo nyumba ya Kiungani, tangu Waalimu wetu, hatta sisi wenyewe. Tena alikuwa rafiki mkubwa wa marhemu Baba Askofu. Wengi waliompenda sana.

Na habari zake nyingi sana zilizo njema alizotutendea. Na mojawapo ilio kubwa ndio alikuwa akiuguza watoto na kuwapa dawa. Kweli bibi huyu alikuwa mzee. Lakini kufa kwake kumetuhuzunisha sana kwa ginsi tulivyopendana naye.

April 5, Alianza kuugua, hatta keshoye akaenda Hospital kule Akakaa na ugonjwa, hatta April 10 akafariki dunia. Tulihuzunika sana kusikia habari hii. April 11 tukaamka assubuhi kwenda kuuleta mwili wake hapa Kiungani; tukafanya sala ya Eukaristi Takatifu kwa ajili ya roho yake. Hatta kama saa a tatu tukaenda kumzika. Wengi waliokuja kwa maziko yake. Tulikusanyika wote Mbweni, Mkunazini, Kiungani, hatta Wazungu wa mjini watu wengi sana. Sasa yupo analala pamoja na ndugu zetu waliotangulia.

Shukurani ziwe kwa Muungu, atupaye na aondoaye. Tuseme nini tena? Ah! Bibi mkubwa ametoweka machoni petu. Je! huzuni gani hiyo! Killa mmoja wetu tumezoea kumwita Amao, Je! sasa mama hatuna. Yeye aliyekuwa yaya bora wa hapa Kiungani, balli sasa tutampata nani?

MSIMULIZI. 855

Wazee wa upelekwa huu wanapungua, lakini faraja iliyo kubwa ndio Bwana Muungu wetu tumtegemee useme: "Mapenzi yako Ee Muungu yatimizwe duniani." "Umpe raha ya milele Ee Muungu na Nuru ya dayima iangaze juu yake." R. I. P.

HABARI ZA HERI.

Mambo mawili makubwa sana yametujia siku hizi, mambo ya kuwapasa waanadamu wote wakaa pande hizi za Afrika wajua na wasiojua wakipenda wasipende, mambo ya kuigeuza hali Afrika ndani na nje. Na mambo hayo yanatoka inchi mbali, ndio Ingereza, marra yalipofanyika habari ikaja ghafula hiyo kwa uzi ndio simu. Neno lilitoka Ingereza, likapita kwa uzi, kumbe kwa kope la juu na chini lipo hapa Unguja, tumelisikia. Bassi mambo gani?

Maaskofu yetu mawili wamepatikana, na siku yao ya kuwekwa ndio siku kuu hiyo ya Petro Mtakatifu, Mtume na Shahidi, 29 June. Maana yake tumejua sote. Mbona nieleze? tangu Wamasihiya wa kale husemwa 'Palipo askofu, ndipo Kanisa.' Hatta pasipo askofu, Kanisa halina uzima. Kazi ya askofu ni kazi ya baba katika Muungu. Tena kwa killa kazi yataka msimamizi. Bassi tumepewa baba na wasimamizi pia, sisi hapa pande za pwani na barra, nazo za Nyasa pia. Na mmoja tumemjua sana na sifa zake na kazi yake Right Revd. Chauncy Maples, Askofu wa Likoma. Miaka kumi na nane amefanya kazi hapa kwetu, wala hachoki. Hatta anazidi kujiingiza katika kubwa zayidi, hasemi bass, haya tu sikuzote. Naye wa pili, hatumjui

MSIMULIZI. 858

bado kwa uso illa sifa zake tu. Amefanya kazi ya kasisi huko Ulaya miaka zayidi ya asharini amechunga watu wengi mahali pangine pangine, amejua mahitaji yao ya rohoni. Na jina lake huyo, Right Rev. William Moore Richardson. Tuwaombe kwa furaha.

Jambo la pili kubwa pia, lakini mbali. Baraza kuu la Waingereza wameamuru kufanyika njia ya gari la moshi toka Mombasa hatta pande za Uganda, tena lifanyike upesi. Safari ya Uganda siku hizi hatta leo, fanya shauri kwanza, funga mizigo, twaa vyombo, chukua chakula, fanya maungo, shika njia, vumilia taabu zote, labuda utajaliwa kuwasili hatta Uganda kwa miezi miwili, ukashukuru. Pisha miaka mitatu mitano. Safari ya Uganda, Ah! kuaheri tu ya kuonana, jipakie garini, kaa kitako, hatta lala ovyo hatta ugonjwa, fumba macho, amka siku ya tatu. Lo! Buganda hiyo! Lakini mapesa kwanza, Bwana. Jambo kubwa burre?

UNANGU.

Tulifika hapa siku ya Nov. 29, 1894. Siku hiyo Che Kalanje na watu wake, walikuja kutulaki na bunduki zinapigwa, na watu wengi wengi wakifurahi kuwaona jamaa zao wakirudi pwani.

Unangu ni jina la mlima wenyewe, nayo imekuwa kama milima miwili pamoja, juu yake nyumba nyingi

MSIMULIZI. 859

za watu zimefunikiza; watu wengi kuliko niliowaona kwa Akwisombe. Che Kalanje ni mfalme mkuu wao wote, lakini wapo wangine; kama: Achipango, Akwikalawe, Che Nampanda, na Akumtilamanja na Che Mbalalila. Upande wa kaskazini wa Unangu kuna miji miwili, Chitagala ndio mji wa Akwisombe, na wa pili Chisindo, mfalme wake aitwa Che Chisoma. Na upande wa kusini kuna miji hii, Mtonya mfalme wake aitwa Che Chiwaula, na Mwitamwi, mfalme wake Che Katuli; na Liwinjili; mfalme wake Akwilasya ao Che Kwopotwe ndio mji ule aliokaa zamani Cardoza na hatta sasa nyumba zake zipo nasikia atarudia tena: na mji mngine Namisimu anapokaa sasa Mwenye Makanjila.

Na miji ya mashariki ni Kumwembe kwa Sultani Mataka, na mgine ni Mkuya mfalme wake aitwa Che Namalweso; zamani mfalme wa Mkuza alikuwa Che Namwela, lakini ilipokuja vita ya Kumwembe Che Namwela akahama, na sasa akaa Kumangochi karibu na mlima Chikala, anakaa juu ya kilima kiitwacho Masangano.

Na upande wa magribi wetu kuna miji hii, Malulu mji wa Nyasa, na Vinjili mji wa Kikole (ndio waliompiga Kalanje akaua watu wengi Jan: 2, 1895, lakini hakuweza kuushinda maana umejengwa juu ya mlima nao umelemaa sana) na mji mgine Chiwegulu, mfalme wake aitwa Che Maniamba; na miji hii yote ya Wayao, nayo yote imejengwa juu ya milima.

MSIMULIZI. 869

Labda baadaye tutaweka Station kule Malulu kwa Mgusa. Tulipokitoka Nyasa tulikaa kule Juma apili watu wengi walikuja kusikia mahubiri: Na tena kuna mji mgine waitwa Chiswulu, nao pia tuliposhinda kule tulikuwa na watu wengi kutusikia.

Kazi zetu hapa Unangu.

School yetu haina watoto wengi wakati huu; maana watoto wa huku husayidia sana mama na baba zao katika kazi ya kulima, labda baada ya kulima kwao tutapata wengi, sasa tunao sita tu nao ni wa nyumbani humu mwetu. Na mwalimu wa School yetu ni Gabrieli Katoma. Na kwenyi mwezi wa May tutapata mwalimu mpya na bibiye, ndiye Yakobo Kachanda labda tutamweka kule mlimani kwa Mbagalila; maana amekubali kumkaribisha.

JUU YA MAFUNDISHO YA DINI.

Juma amosi twatweka bandera kuwakumbusha watu kama kesho ni Juma apili nayo inatwekwa saa kwanza na hushushwa saa thenashara. Siku ya Juma amosi mtoto anaitwa Litambo huchukua kengele na hupanda mlimani, na baada ya nussu saa hurudi na watu wengi, lakini shidda kuwaona watu wakubwa illa vijana waume na wanaake, lakini mwezi huu watu wazima wengi wanaanza kuja. Wakija tunaimba wimbo wa 149, na halafu yake amri kumi, tena hufuata mahubiri. Juma a pili ya nne katika Kwaresima, Dr. Hine akaniambia niwaulize watu kama maneno haya yamewaelea, na wakiwa na neno waulize, nilipowauliza

MSIMULIZI. 861

mmoja akajibu akinena, "Sisi hatuyakubali maneno yenu, maana tangu kuja ninyi watu wengi wanakufa, nao si wazee walla hawana kuugua kwa siku nyingi." Tukamwuliza, "Humu mjini hamna makaburi ya watoto wachanga waliokufa kabla ya kuja sisi? Wengi wakajibu, "Ah! nyamaza."

Tena akizidi kuuliza, "Je! tukiacha hizo thambi mnazonena, huko mbinguni tutapata anasa na vyakula vitamu kama hapa duniani?" Nikamwambia Mbinguni kuna furaha na uzuri wa kupita kuo, na kula. Tena akazidi kuuliza mengi juu ya nguo zinavyofanywa, nikamwambia, naswi watu wa barra tukiwa watu wa kumwogopa Muungu sana tutapata akili hatta ya kufanyiza nguo, akakataa kabisa, akinena, "Tukijua kufanyiza nguo sisi watu wa barra, ulimwengu wote utaharibika."

Tena tuna watu waume na wake wanaokuja kufundishwa siku ya Juma a tatu na Alhamisi. Na killa siku saa kumi napanda mlimani kuongea na watu, na kurudi saa thenashara. Watu wa Pa Mtilamanja ndio wajao kufundishwa.

Feb. 14 Nalitoka hapa kwenda Kumwembe kwa Sultani Mataka (ni mwendo wa siku mbili toka hapa) kuwapeleka watu niliokuja nao hapa toka Chitangali wapate kupelekwa hatta kwao. Tulipotoka hapa tukalala karibu na Likopolwe ndio mji wa kwanza wa Mataka, huu anakaa nduguye Che Mtamila, tukala masuku mengi njiani, na tena matunda mengi ya pande hizi.

MSIMULIZI. 862

Feb. 15 Tukaondoka tukafika Mwikopolwe, lakini mfalme hatukumkuta tukaongea sana na watu wa mji, msemu wa Kiyao chao kama Wamkula, tulipoisha kula tukaondoka tukafika mahali paitwapo Mbanga tukulala.

Feb. 16 Tukaondoka tukavuka mto Bochesi ndio ni mto mkubwa tulivuka kwa ngalawa, mtoto mdogo wa kike ndiye aliyetuvusha anajua sana ginsi ya kuvusha kupita wanaume waliokuwapo pale, tukapika pale athuuri. Tukaondoka, jioni tukafika mjini penyewe, Mwembe wa zamani lilipo kaburi la Mataka wa kwanza, wenyewe hupaita Pa Msichisi. Mwendo wetu wote toka Likopolwe ni mijini tu hatta Serkalini kwenyewe. Mji huu ulikuwa na enzi zamani, sasa kaburi tu na watu wachache nao ni watu watorokao kwa bwana zao, ao kugombana wao kwa wao, ao mke na mumewe hukimbilia hapa na akitika hapa bwanawe wala mumewe hawezi kuja kumtwa, imekuwa kama ile miji sita ya kukimbilia.

Nalo kaburi lenyewe limejaa nguo za killa aina, na maji hutiwa katika mitungi mikubwa.

Killa mtu na mitungi ya pombe pia, na miti mikubwa imepandwa kuzunguka kaburi, na mlingote mrefu mwenyi bandera ya Sayidi (bandera nyekundu). Tulipofika mwenyewe hayuko, yuko Kuwela (ndio mji wake wa pili) mkewe akatufanyia heshima sana.

Asubui nikamwambia mkuu wa mjini anipeleke Kunamiswi maana ndiko uliko Mwembe mpya juu ya milima miwili Namisuwi na Lisale, tukaenda

MSIMULIZI. 863

akatuonyesha mlima wanapouawa watu na Mataka, akiwa mtu ameua ao kuloga. Tulipofika mjini tukalionga jumba lake kubwa mko Islamu wengi wamejenga Mosikiti, na kaburi la yule Mataka alimfukuza Padre Johnson limejengwa kukabili mosikiti, watu wengi wakaja kututazamia, halafu tukaenda uani kumwamkia mkewe mkubwa, naye kweli mkewe mkubwa, mnene sana sana na mfupi sana, amevaa kaniki; akasema naswi kidogo tu tena tukamwaga tukashuka mlima. Nikamwambia yule mtu nipeleke alipojenga Mzungu wa kwanza aliyefukuzwa na kunyang'anywa mali. Akanipeleka tukaona alama ya nyumba, napo mahali penyewe ni kando la kilima. Nikamwambia unaweza kuniambia habari za Mzungu huyu? akajibu ndio, Akaanza; alijenga sana hapa akaleta mali mengi na mtumishi wake alikuwa Abdallah, alikuwa hodari kwa kutega bunduki hatta siku moja aliua fisi aliyekikamata sana watu; na wakati wake Mzungu huyu watu wengi walikipata nguo; kwake anasimamisha mti uliopakwa mafuta, tena awezaye kupanda humpa nguo. Ah? watu wengi wanamlilia. Nikamaliza kwanini wakamfukuza bassi? akajibu, Alifanya shauri la kuwaua watu kwa njaa, kwani alitangaza kama limeni siku sita, na ya saba hapana kulima, bassi tukamwendea Sultani tukamwambia, "Tazama Mzungu anataka kuangamiza inchi, ndipo akaamuru afukuzwe. Nikauliza, je! wale waliouawa mwaka juzi je? Akanena, Wao walikuwa wawili walitaka kusimamisha bandera zao, lakini Sultani

MSIMULIZI. 864

hakukataa, wakafungwa mali yote yake yakatwaliwa, lakini mkubwa alikuwa na ndevu refu sana, nguvu nyingi sana, tulijaribu kumfunga hatukuweza tukawaua wote kule Namisuwi; walikwia sana kuoza sijui kwa nini?

Assubui tukaondoka kwenda Wela tukamkuta mwenyewe naye kweli Sultani. Mtu mrefu sana, yule Mohammed Thalatha yataka mkono aongezwe ndipo amfikie Sultani Mataka. Naye hupanda punda killa atembeapo na baragumu hupigwa mbele yake, na askari vijana na bunduki zao wengi naye, nyuma na mbele, na huyo nduguye atakayeingia jina baada yake naye mrefu sana, anaitwa Mkwepu. Nikamwamkia na kumweleza nilichojia. Naye ana waalimu wanne wasomao barua zake. Siku ya pili nikaongea naye sana, akaniomba msalaba niliovaa pamoja na mkufu wake; lakini kabla sijajibu, wale waalimu wakamwambia kama nguo hizi na hivi vyote alivyovaa ni vya dini si vya malidadi, bassi akanyamaza. Na Dr. Hine alinituma kama nkifika mulize kama ataka wazungu waje kujenga kwake; lakini sikuthubutu kumuliza maana anakula bangi kama huyu Kalanje, na pombe pia.

Baada ya siku kumi nikafanya safari ya kurudia kwangu Unangu, nikapita njia ya Mkuya kwani fupi; tukapitia pa Msenda tukapitia tukakaribishwa sana na jamaa zake Muchi. Siku ille tukaenda sana tukafika Mkuya tukapikia, tukatoka tukaenda na usiku pia kwani ilikuwa Juma amosi tukafanya nguvu

MSIMULIZI. 865

tufike usiku hapa, lakini kwa maana ya mvua na baridi (kwani inchi hii ni ya baridi sana) hatukuweza usiku tulipokivuka mto tukaanguka mimi na mtu niliyefuatana naye nikaumia jeraha kitwani na begani, mawili miguuni, na yule mtoto akajiumiza mkononi. Tukafika hapa saa kwanza Jumaa a pili. Nikafikia kuugua hatta ile kazi yangu ya kutembea mlimani ikazuiwa kwa madonda haya ya mguuni. Bassi tangu January nimeugua vidonda hatta mwezi March 25 nimepona, Dr. amesumbuka sana kuvitia dawa. Watu wa kule Kumwembe na wa hapa wana tofauti sana, na hukumu zao mbali. Wa Kumwembe huapa hivi: "Ku msikitini Che Nyambi! kwa sababu kaburi lake limejengwa mosikiti.

Na wa hapa huapa: "Mbamba Kumu!" ao "Amdachi!" Na hukumu za Mataka naona za haki kama Akwisombe. Kule Kumwembe alikuwa mtu mmoja Kalukupa, mtu huyu alikuwa kiongozi wetu safari ile ya 1892 ya marehemu Bishop Smythies, alikaa hapa kwanza tena akatoka akakaa Ruvuma kwa Mponda; halafu akakaa kwa Akwisombe, tena akaja akakaa hapa Unangu; tena akatoroka, sasa anakaa Kumwembe.

Mwaka huu huku Yao vita nyingi zinaanza; kwanza ya Mataka anaenda kupiga Mwitamwi, maana Katuli amepeleka ng'ombe wanne zawadi kwa Mataka nataka vita. Kalanje anafanya shauri kupiga Chiwegulu kwa sababu watu wa Chiwegulu walishariki vita ya Manjili. Tena watu wa Makanjila wanatupiga sisi na watu wa Mtonya, juzi watu wetu sita wamekamatwa,

MSIMULIZI. 866

na wawili wameuawa. Tena Kawinga anapigana na Malamia ndio chini pande za Mngochi. Na nzige wamezidi Blantyre sana siku hizi, lakini hapa hapana. Y. B. A.

CHITANGALI.

Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Ikiwa umejua kama katika miaka hii miwili tumepitiwa nzige pande za kwetu, bass tangu mwezi wa Nov. siye tunaokaa sehemu ya inchi ya Makonde tumeingiwa na njaa sana; bass tukawa tunashukia sehemu ya inchi itwayo Lukulesi huko Masasi, maana wao hatta leo wana akiba sana ya vyakula ginsi inchi ilivyo na rhotuba kununua vyakula, na wangine kufanya kibarua cha kulima na mshahara wao kupimiwa mtama. Lakini miezi hii dunia ya upande huu imetulia kidogo kwani pana mihogo mingi waliyopanda kwa umoja wakati zilipofika nzige, na wangine wana mtama ndio waliojaliwa kupanda marra ya pili. Mwiti mihindi na mtama wamepata sana isipokuwa mpunga ndio waliopungukiwa wasiweze kupanda marra ya pili.

Na ijapokuwa njaa hivi, kwenyi siku ya Pasaka tulikusanyika vilevile kama siku zote watu walishuka Jumaa tano na Alhamisi kuwa tayari kwa Ijuma kuu; na watu ilipokwisha siku kuu ya Pasaka hawakurudi mijini mwao wahadi Juma a tano kwani ilianza michezo wahadi Juma a nne saa kumi na Juma atano wakaenda zao.

MSIMULIZI. 867

Kama wangine mmepata fanuni kama Mzee Nakaam anataka kuhama Chitangali kwenda Chiwata, kweli mambo hayo lakini hajahama lakini amepeleka watu kama arobatashara kujenga nyumba zao na wakijilimia, na wangine huenda kuweka mashamba wakirudi mjini, lakini hatta sasa watu wataka sana kuhama, tena wanaisifu inchi yenyewe kwa rhotuba. Itakuwa jirani sana na Mwiti maana ni karibu sana. Na kwa Mzee Kaluwa pia.

Ap. 18, Nikaeda Newala pamoja na Mwal. Daniel Usufi. Ap. 20, Nikarudi, mwenzangu akashinda siku 4 akaenda Masasi kwa njia ya Miwa na Mwiti.

Ap. 21, Mwal. Petro Musa akatoka Mwiti wahadi Masasi. Ap. 25, Padre Cecil akatoka kwenda Mwiti awatolee Usharika Mt. Wamasihiya wa kule. Usiku uleule wakaja simba wawili wakakamata mbuzi watatu katika zizi la Mzee Maluchila maana hapana watu upande huo wameisha hama, sasa wamehama, wamebaki vijana wazichungao tu na wanaake wawili.

Ap. 27, Mwal. Daniel akawasili Chitangali akitoka Masasi na usiku uleule wakaja simba tena wakajaribu kupasua zizi Msokosela lakini watu wakawadiriki upesi wakakimbia.

May 2, Nikangoa kwenda Masasi, nikamkuta Padre njiani kwani ndio aliokusudia kurudi. Nikashinda siku Mwiti kwa Mwal. Gilbert, May 4, Nikaenda Masasi. Nikashinda siku 3, ikawa shughuli yangu kuzunguka milima kuangalia jamaa na jioni kurudi kulala.

MSIMULIZI. 868

May 8, Nikatoka pamoja na Barnaba Mtaula mwalimu wa Masasi tukalala Mwiti, assubui miye nikashika njia ya Miwa na mwenzangu Chitangali May 10, Nikafika Chitangali, na Padre Carnon akafika naye kunako saa 10 pamoja na watu wengi wengine wakimchukua kwenda Lindi, wengine wakichukua nta kuuza Lindi. Padre Carnon alikwenda kutengeneza maneno ya watu wa Masasi waliokosa kusikiana na mtu wa Lindi, bassi yakawa dawa kwa Gavanori wa Lindi, Assubui yake akang'oa kwenda Lindi.

May 14, Barnaba Mtaula akang'oa kutangulia kwenda Lindi pamoja na watu waliochukua nta. Na assubui yake nikatoka mimi pamoja na safari ya Newala tukaenda mwendo wa siku mbili mahala pa kuenda siku tatu; kwani tukizidi sana kujilawa hatta wakina mwal. Barnaba tukawashika njiani. Tukafika Lindi Ijumaa May 17, Jumaa mosi assubui yake Padre Carnon akawa anafunganya kurudi kwani nimeisha waambieni kama ameshuka Lindi. Tukashinda siku mbili Lindi, siku ya pili yake jioni tukaabiri mnamo Wismann. Assubui siku ya tatu tukang'oa wahadi Kilwa kama saa kumi unuss, tukalala palepale na ussubuhi lising'oe wahadi saa kama alasiri. Tukaenda usiku kucha saa ya kwanza tukafika Dar-es-Salaam saa sita tukang'oa wahadi Bagamoyo tukalala pale tukauthika sana kwa mvua usiku ule; ussubuhi saa ya pili tukang'oa tukaingia mji wa Unguja kama saa tano haswa. Na safari yetu tulikuwa jamii kubwa, maana watoto wa Newala na Masasi na mimi wote tulikuwa mnamo stima moja. A. K.

MSIMULIZI. 869

MAGILA.

Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Tangu siku mbili tatu tumeacha kucheka nawe, bassi tukaona kama ni vema tukugeukie tena kwani wewe wawafurahisha watu wote, bassi afathali naswi tuwe washariki wa furaha hiyo hiyo. March 25, ilikuwa siku ya Kuhubiriwa Bikira Maryamu. Bassi siku ile tulipokwisha kutoka Kanisani kama saa ya pili, Padre Griffin akawaita waalimu akawaambia, kama wakiweza wawachukue watoto mlimani, kwani mwalimu wetu mkubwa, Mr. C. W. Roberts hakuwapo, kwani huenda killa Juma a pili huko Msalaka apate kuwahubiria na kusalisha; kwani hapana kasisi. Bassi tukawapeleka watoto huko mlimani, tukakaa kule, bassi marra wakaja watoto wawili wakasema kama Mr. C. W. Roberts amewasili lakini hatapumzika anakwenda Kwamkului, ndipo mahali akaapo mwalimu Gramville. Bassi wakaenda watoto wale aliowaita. Hatta alasili kasiri akawasili Rev Samwili Sehoza pamoja naye waalimu wawili Alfred Juma na John L. Mwaimu, wakatuzungumza halafu wakaenda zao. Hatta saa yetu ilipotimia tukarudi. Mwalimu Ackworth Machaku hawezi macho tangu mwanzo wa March hatta sasa. Siku hizi tumepata jambo tulilolitaka mno ndiyo mvua, kwani ilikawia sana mwaka huu, bassi sasa watu wanafurahi sana kuipata. Tena njaa katika inchi hii imezidi mno. Kwa sababu hii nzige za kwanza hazikula mihogo wala kunde, bassi watu wapakonea mihogo na kunde, lakini hizi za

MSIMULIZI. 870

mwisho zikala mihogo na kunde, bassi watu wasiwe na akili ya kutenda.

Nathani ni wengi waliosikia habari ya njia ya gadi la moshi, bassi siku hizi imeendelea mno; mjue kama njia hiyo imeendelea sana, watu wa Magila waendapo Tanga huenda kwa miguu mwendo wa saa mbili unusu marra wamefikia gadi. Sisi watu weusi hulipa robo tu, Wazungu ndio rupia mbili. Bassi usikie ginsi kazi hiyo ilivyo ngumu kuchimba; kutwa na kiboko mkononi nyuma yao, na kazi yenyewe kwa kuwa ngumu watu wa Tanga hawakuiweza kuifanya wala Mswahili yoyote wala Mbondei. Bassi Wadoicha wakaleta watu wa huko ndani, kabila mbili Wamakua na Wanyamwezi. Kwa hao kazi hiyo hutendeka. Wakati huu wa Kwaresima tumepata kupigiwa chapa vitabu vidogo vinavyoitwa njia ya msalaba vyenyi sanamu ya Bwana wetu tangu kituo cha kwanza hatta kituo cha kumi na nne.

Mwezi huu uliopita tumepata Bibi mwalimu kwa chuo cha watoto wanaake wa hapa jina lake Miss Dunford, pamoja naye Mzungu mmoja jina lake Mr. Brent, akaa Mkuzi.

March 13, tulipata habari kama meli ya pili baada ya hii baba Padre H. W. Woodward atawasili hapa, bassi siku hiyo tulipohakikisha kujua tukapeleka punda na mmoja kumngojea kwenyi Station ya Ngomei, Lakini gadi lilipowasili hakuwamo, akarudi yule mtu na punda, kumbe wamepitia njia ya Pangani yeye na Padre Dale, akawasili hapa Juma apili alasiri March 31.

MSIMULIZI. 871

Apr. 14, Walituasilia hapa Mr. Roberts na Dr. Ley, Mr. Chilvers waliokuwa wamekwenda kubadili hewa, na pamoja na bibi mmoja anayekuja kumsayidia Miss Dunford kazi ya kuwafundisha watoto wanaake. Lakini katika hawa niliowataja Mr. Roberts hakwenda kubadili hewa, lakini alimpeleka Bibi mmoja aliyekuwa hawezi jina lake Miss Southward.

Jumaa Kuu Kanisa letu likajaa watu tele, lakini walikuwa mapadre wawili tu kwa saa zote, tangu saa sita hatta saa kenda, walikuwa Padre Woodward na Padre Petro, kwani Padre Griffin na Padre Palmer walikuwa hawawezi.

Siku kuu ya Pasaka, sala kuu ya Pasaka ilianza Juma a mosi jioni, asubuhi ya Pasaka saa thenashara, ulikuwa Usharika Mtakatifu mahali pawili, kwenyi mathbahu ndogo ndio kwa waalimu walio waimbaji na watoto waimbaji, illi wawe na nafasi ya kuwa tayari kwa nyimbo zote wakati wa sala kuu ya Usharika Mtakatifu. Baada ya sala hii ilikuwa saa thenashara unussu.

Baada ya haya zikaanza kulia kengele nyingi watu wakajaa Kanisani isivyo na kifani wake kwa waume; na walioshariki wengi mno, na aliyehubiri ndiye Padre Palmer.

Siku moja ilituasilia safari kubwa; twauliza kuna nini? Twaambiwa Duke anakuja, marra tukatoka wote tukitazama huko chini michungwani twajionea myavuli mitupu kwani ilikuwa mvua kidogo, wakaingia aliyetangulia ni mwenyewe Duke na mkewe, na nyuma

MSIMULIZI. 872

yake Baron Von St. Paul, tena nyuma yao Bwana wa fortha ya Tanga, na tena Bwana mganga, wangine wawili na bibi mmoja. Nyuma yao waana wa Kiafrikani Wanubi, wajionea nyuso kama wamefunikwa kanikini. Walilala hapa hatta assubuhi wakaenda huko mlimani kutembea. Hatta April 17 jioni wakarudi hapa hapa, usiku wakalala, assubui wakaenda zao. Ujue kama safari hiyo ina ufakhari mwingi, Wazungu wote sita walipanda nyumbu na mkewe Duke ndiye aliyepanda frasi; na mtumishi wa Duke amepanda punda tu yeye peke yake, wote nyumbu.

Apr 26, waliwasili watoto watokao Kiungani pamoja na mwalimu Paul Y. Dezu, na majina ya watoto ni hawa James Mkumbano, Francis Mzituba, John Mbaruku, Harry Kidungwe, Nataniel Bungulu, walikwenda Kiungani muda wa mwaka sasa wamepewa mwezi mmoja kutazama jamaa zao.

Apr. 27, Alituasilia baba yetu wa kwanza aliyekwenda Ulaya yapata sasa miaka mitano, bassi tulipoambiwa atakuja, killa mtu aliona kama ndoto isiyowezezana kwani ni siku nyingi ati. Bassi Juma a pili akataka kupokea Usharika Mtakatifu kwa waanawe mwenyewe, bassi Padre Petro akatoa Usharika na Rev. Samuel alimsayidia kwa kushika kikombe, ilikuwa vizuri mno, naye mwenyewe vilimpendeza bassi watu wote tukamshukuru Muungu aliyeyaendeleza mambo haya kuwa hivyo yalivyo sasa.

Bassi alipotoka Kanisani watu wengi wamejaa wakingojea kumwamkia. Bassi siku hizi killa saa wanamjia

MSIMULIZI. 973

watu kumwamkia rafiki zake wa zamani, bassi hapa nimewafanya kama nimewafumba maana nimesema baba yetu wa kwanza, wengine watauliza ni yupi? Siye huyo Rev. J. P. Farler aliyekuwa Archdeacon wa Magila.

Apr. 27, Tulikaa raha mustarehe hatuna habari, marra tulistushwa kama moshi mawinguni, tukitazama ni nzige wanarudi tena, ah! killa mtu amevunjika moyo kwani watu wamepanda mihindi mingi tukitumaini huona njaa.

April 29, Waliondoka hapa Bwana Daktari na Miss Dunford wakimchukua Miss Derby aliyekuwa hawezi sana kwani aliugua kama muda wa juma tatu, marra mbili ao zayidi kufanyiwa Usharika wake wa mwisho. Tena afathali sana Daktari alikuwapo usiku kucha, alikuwa halali ndio maana ikawa heri kidogo.: April 28, Alituasilia Padre Gr. Dale akitoka kwake Mkuzi, ametuambia kama huko Mkuzi amezika watu wanne wamekufa kwa njaa.

Wengine wengi wanajua kama karibu ya Mission pana duka la Mhindi aliye Mmasihiya jina lake James Moses Meta. Bassi amejenga kibanda kusudi watu wauzie biashara zao. Bassi panapo April 30 tukapewa habari kama pale kibandani pa James Meta amekufa mzee mmoja kwa njaa, watu walio Wamasihiya wakamzika.

May 2, tumeletewa habari ya mji ulio karibu na hapa, jina lake Kiumba, kama watu wawili wanaolala nyumba moja wamekutwa asubuhi wamekufa; Ah!

MSIMULIZI. 874

ndugu, njaa hii ni nzito sana, lakini hatuwezi kusema kama makafiri wasemavyo, "Muungu hatupendi." Wamasihiya twajua ni mkono wa Muungu kwa thambi zetu.

Apr. 29, Alituasilia hapa mfalme Kinyasi, Mkilindi, kwani amesikia kama Bwana mkubwa Farler amekuja, akachukua kondoo wake akaja kumwamkia; akakaribishwa vyema sana; April 30, akaenda zake.

May 7, siku ya kukumbuka Roho ya Baba yetu Askofu aliyefariki mwezi wa May mwaka wa jana, bassi siku hii ilitimia mwaka mzima tangu kufa; Padre wetu akataka tuwe na siku ya ukumbusho, bassi assubuhi kengele tatu zikalia watu wengi wakajaa Kanisani, Archdeacon Farler akakaa pamoja na watu chini lakini Padre Griffin akaishika sala, baada ya sala watu tukatawanyika njia zetu. Tena Archdeacon Farler akaenda Misozwe watu wakamwamkia yeye na Dr. Ley, bassi hatta jioni kengele ikalia ya Kanisani tukasali. Assubuhi Archdeacon akafanyiza Missa Takatifu. Tulipokwisha tukatoka kwenda pande za Magila.

May 19, imetangazwa arusi ya mwalimu Yakobo Ghamdangwe. Bwana Archdeacon Farler alikwenda Mkuzi kwa siku tatu lakini alipatikana na homa kidogo, sasa hajambo. Padre Petro atakaa Misoswe mahali pa Padre Du Poulay. Tumehuzunika mno kusikia kama Sister Agnes amefariki huko Ulaya kwa uthaifu ule aliotoka nao hapa; na siku ya Juma nne assubuhi ilikuwa sala ya Usharika Mt. kwa ajili ya roho yake.

MSIMULIZI. 875

Padre Dale alikuwa hawezi sana sasa hajambo twatumaini atakwenda Unguja kubadili hewa.

Watoto wetu walitazamiwa kazi ya chuoni, katika darasa ya kwanza 1 Charles Mfuko, 2 Nicholas Saki. Katika darasa ya pili 1 Lamberto Semkugwe, 2 Francis Baraka, katika darasa ya tatu 1 Lesiwa, 2 Tangulu. Katika darasa ya nne 1 Semwaiko, 2 James Bakali, katika darasa ya tano 1 Sekibai, 2 Mkwacha. Katika darasa ya sita 1 Saidi, 2 Kamanga, katika darasa ya saba ni mtoto mmoja tu jina lake Jitu, Katika darasa ya nane 1 Kanju, 2 Mwenyipembe.

KUFARIKI KWAKE Dr. HERBERT LEY m.r.c.s.

Alijiunga Mission hii ya Universities kwenyi 1885, akaenda kukaa Magila, na amekana kuwa mtendaji na, mwenyi bidii kwa kazi yake. Hatta Bonde nzima ilitirika mno kwa dawa alizokarimiwa na Muungu awagange nazo. Tena akarejea Ulaya Ingreza kupumzika, tena akarudi Magila. Vile vile alikuwa mwenyi bidii na uwivu sana kwa kazi yake, asikubali kuiacha apumzike.

Tena mwaka huu ulipoandama aliumwa mguu na nyoka mkubwa, ndio mwanzo wa kuthoofika afya zake. Akaja hapa Unguja kubadili hewa, kiisha akarudi Magila.

Akapata habari kama Mdachi mmoja hawezi Mayumi, akaenda kumtwaia illi ampeleke Tanga, lakini alipofika Magila marra akashikwa na homa kali sana kwa juma moja, June 10 alifariki. Msiba huu mkubwa sana kwa Magila na sisi wote tumjuao.

"Bwana ndiye aliyetoa, Bwana ndiye aliyeondoa, Jina la Bwana libarikiwe." - R. I. P.

MSIMULIZI. 876

MKUZI.

Salamu kwa Mtengenezaji wa Msimulizi. Siku ile tulipotoka Kiungani saa thenashara unusu tukalala melini; hatta saa pili asubui siku kuu ya Marko, April 25 tukang'oa nanga, jina la meli Setos. Tulipofika Tanga ni saa tissa unusu. Hatta Ijumaa asubui tulichelewa kuingia katika gari la moshi; tukashinda pale mpaka alasiri, tukaenda uliza habari za gari tukaambiwa gari haliendi Ngomei, illa mahali panaitwa Pongwe, bassi tukalala tena pale Tanga. Assubui yake ni Jumaa mosi tukashinda hatta alasiri saa tissa kasa robo tukaingia garini pamoja na Rev. J. P. Farler; tukaenda hatta tulipofika Ngomei, ndio mji wa kwanza wa Bonde wa upande ule, ni saa kumi unusu. Tulipofika pale Mr. Farler akakutana na punda aliyeletwa kumlaki akaenda zake Magila. Mimi na wenzangu tukakawilia pale kwa sababu tulikosa wapagazi; baadaye tukawapata tukaenda lalia Umba kwani ni karibu na Umba. Ah! inchi imejaa nzige na njaa tupu, na watu wengi wamehamia pande za pwani na Tanga, njia zimejaa magugu, mashamba mengi hayakulimwa. Asubui yake tukashika njia ya kwenda Mkuzi, tulipofika hapa ndio kwanza watu wametoka Kanisani sala ya Eukaristi.

Nimefuatana na mtoto jina lake Msoke alipotea zamani sana, sasa ni miaka saba tangu kupotea, bassi tukampata huko Unguja, ndipo nikaja naye illi kumrudisha kwa babaye. Bassi tulipofika hapa babaye

MSIMULIZI. 877

alipomwona akalia kwa furaha, kwani hakuthani kama atampata tena. Na baba yule akachinja kuku juu ya yule mtoto; hatta athuuri tukapewa mbuzi kuwa kitoweo chetu.

May 4, baba yetu Rev. G. Dale akashikwa na homa, Juma a pili ussubui akatokea Padre Petro kutufanyia Eukaristi Takatifu, saa nne ikawa sala Kibondei, wakafanywa watu wawili kuwa wanafunzi, majina yao Masingano, Manyangasa. May 6, walitoka watu hawa Herbert Msembeleka, Yusufu Kilua, Charles Mwekaahangwa, na Herbert Ngaja, wakaenda Unguja kufanya kazi kwa Mr. H. Lister. May 11, Padre Dale akaenda Magila kwa ajili ya ile homa yake. Siku hiyo hiyo akafika Rev. Dr. Palmer akitoka Korogwe kutembea, tayari kurudi Unguja.

May 19, Rev. J. P. Farler akambatiza mtoto wa James Mwaimu, kwani Rev. Dr. Palmer alienda Magila kumtazama Padre Dale afya zake; na mtoto huyu aliyebatizwa jina lake Agnes Alice.

May 22, Rev. Farler akaenda zake Magila assubui na jioni Rev. Dr. Palmer akarudi toka Magila, akatuambia ya kuwa Padre Dale anaenda Unguja kutazama afya yake na mimi ntakaa hapa.

May 26, pana watoto wetu tunawasafirisha kwenda Unguja pamoja na watoto wale wa Magila waliokuja mwezi uliopita, ndio Marko Changale aenda Kiungani, pamoja na Cuthbert Mlangwa na mwenziwe, aenda Mkunazini, lakini ameshikwa na homa hii jioni, bassi sijui, vema. Lakini pana wawili tena wangekuja bali wamezuiwa

MSIMULIZI. 878

na ugonjwa, wa kwanza John D. Saidi, lakini yee hawezi sana kitandani tu huondoshwa na watu, sijui ya baadaye, wa pili Wilfred Ponda, mguuni, hawezi kwenda. A. A. S.

KOROGWE.

Mtengenezaji wa Msimulizi Salamu. Wa baada ya salamu twakuletea habari zetu chache, kwa wakati mwingi hamkupata habari za huku kwetu. Siku ya 25 ya April, kulikuwa ubatizo wa watu wazima na watoto wa chuoni. Arthur Mbezi, Petro, Kagoda, Chrstopher H. Chaba, Yohana Abdallah, William Mbelwa na twalifurahi kumwona Rev. Palmer akitoka Mkuzi pamoja na watoto wake wakija kutembea, nasi tulifurahi, na labda mmepata kusikia kama twajenga Kanisa jingine jipya la mawe kwani tulilo nalo ni dogo tu halina nafasi, haliwezi kuchukua watu 60 ao 50. Kanisa hili kubwa litachukua wakati mwingi kuisha kwani mafundi wamekwenda Unguja kwa holiday twatumaini watarudi tena kujenga. Tena nzige siku hizi wamerudi wameharibu mihindi mingi lakini mingine imepona, alitokea hapa siku, Juma a mosi Bwana mkubwa wa Mazinde aitwa Von Storck, sababu yake aliyojia ndiyo hii, alituma watu kwenda Tanga kuleta barua zake zatoka Ulaya Jermani, bassi wale wapagazi walipofika hapa Korogwe wakatua, wakaweka mizigo yao na ule mzigo wa barua una chakula ndani, na wale

MSIMULIZI. 879

wapagazi wakarudi zao mjini kutafuta maji, nyuma huku Mzigua mmoja akachukua zile barua akaenda nazo, na yule mpagazi aliporudi akatafuta barua hakuziona hatta kidogo. Bassi akaenda zake kumwarifu Bwana mkubwa kama barua zimepotea Naye. Aliposikia akafanya uchungu mwingi sana akatoka Mazinde kama saa ya sita ya usiku akawasili assubuhi mapema, acha awatolee uchungu mwana wa Kidoicha, akawakusanya watu wa mji wote, akawaambia, sharti mtafute barua zangu na kama hamtaki mji wenu nitauchoma moto. Watu wakatoka kutafuta mchana kutwa, mji ukafungwa hapana mtu kuingia ndani ya mji hatta kidogo, na ng'ombe na mbuzi zikazuiwa, watu wakatafuta hawakupata Naye. Amesema kama wasipoona ng'ombe na mbuzi zote mali yake, hatujui kama atachukua kweli. Watu wakatafuta kwa siku tatu; na sasa barua hazikuonekana na watu wamesamehewa ila watu wamehofu sana kwa ng'ombe zao walithani zitatwaliwa, nazo ng'ombe nyingi sana na mbuzi, alitaka kuwatiisha tu nao wakatetemeka kwa nguvu za mwana wa Kidoicha. Nao Wazigua wameomba rathi waachiliwe mji wao na ng'ombe zao na mbuzi pia. Sasa yule Bwana mkubwa amekwenda zake, nao wamesamehewa mali zao na mji wao pia. Sasa wamestarehe watu. Y. H.

KILIMANI.

Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Wa baada utanikaribisha, nabisha bassi nifungulie mlango

MSIMULIZI. 880

nibarizi nawe, kwani nimesikia habari zako kama wataka kulishwa sikia, bassi. April 16, tulienda kushinda kisiwa cha Makaburi, tulitoka zetu hapa saa kwanza unusu tukachapa mwendo wahadi mjini tukaingia katika mashua tatu za makasia, tukichukuliwa nazo hatta bandari yetu tukashushwa. Tukajifurahisha tuwezavyo, hatta saa a sita tukapewa chakula chetu tukashukuru. Saa kenda tukaingia katika mashua tukiletwa nazo hatta mjini tukashuka tukafika hapa petu saa thenashara unusu.

Apr. 18 Mtoto mmoja aitwa Hamadi alikuja kukaa hapa atoka shamba la Mbweni.

Apr. 20 Watoto wetu watatu walipelekwa Kiungani kukaa ndio George Uledi, Denys T. Sayite na Sila Jabu.

Apr. 25 tulipata holiday tangu assubuhi hatta jioni.

May 1 tulikusudia kufungua nyumba yetu, kwani Chuo chetu kimekwisha sasa, wallakini Bibi Mills alikuwa hawezi, siku hii iliwekwa hatta Bibi apatapo nafuu.

May 8 ilikuwa kufunguliwa nyumba yetu, siku hiyo tulipamba kwa makuti tele na bandera nyingi sana za killa namna, na Bibi aliwaita watoto wake aliowalea tangu udogo wao, killa mmojua alioko hapa Unguja kwa siku kuu hii, saa saba walikutanika wote hapa, wengi sana waliokuja, na watoto wa shamba walikaribishwa jumla wote tulikuwa 110. Saa nane ilikuwa karamu tulikula chini ja mwembe, tulipokianza

MSIMULIZI. 881

anza kula mvua ilikuja, kwa hiyo hatukuweza kukaa kwa utaratibu kama tulivyowekwa, tulitawanyika, asiyeogopa mvua alikula vile vile haithuru na baada ya kula tukapewa sharbati. Siku hiyo hiyo alituasilia mke wa Mwalimu Denys na kitoto chake, tulifurahi mno kumwona, saa kumi ilikuwa sala ya kufunguliwa nyumba, tulienda Kanisa la Yohana Mtakatifu, watu wengi walikuja kwa sala, katika hao ni Baba na Mama wa killa mtoto wa Shamba, kwani walilalikwa nao kwa siku kuu hii. Tulipokwisha kuingia tuliimba uimbo mmoja, baadaye Archdeacon alitoa hutuba kwa Baba na Mama wa killa mloto wa Shamba wawalete watoto wao wafunzwe katika chuo cba Kilimani, ilikuwa nzuri sana. Na baadaye tuliimba uimbo mmoja, tena tulitoka Kanisani tukiendelea kwa kuimba wahadi Kilimani, tukasimama mlangoni na tuliimba Shangalieni leo, na Zaburi moja. Baadaye tuliingia Chuoni na Bwana Key alisema sala ya kubariki nyumba, mwisho tuliimba wimbo wa 19 mstari wa mwisho. Baada ya kutoka watu wale walioitwa walipewa chakula na watoto wao wadogo, kiisha walienda zao killa mmoja kwake.

May 11 Bibi Mills alianza kuwa hawezi wallakini hakujipumzisha, alifanya kazi yake tu.

May 13 Tulianza kukitumia Chuo chetu.

May 19 Tulikuwa na hofu sana kwa bibi ni kumwombea tu apone ndivyo tulivyofanya.

May 20 Alipelekwa Hospital, na huko akawa hajambo.

MSIMULIZI. 882

May 21 Miss Clutterbuck alienda Hospital alikuwa hawezi kidogo na alienda apate kutunzwa kwani hapakuwa na mtu wa kumtunza. Bibi Key anatusayidia sana kwa Mabibi akisikia mmoja hawezi tu hatta ijapo usiku anakuja, wakienda Hospital anawapeleka. Mwalimu Benedict Madalito alikuja kufanya kazi mahali pa mabibi, na Miss Clutterbuck aliturudia May 25, na May 29 Bibi Mills alirudi tulifurahiwa mno kumwona yupo naswi ashika kazi yake, wallakini kufundisha chuoni bado, twasikitika kwani ashikwa na homa tangu aliporudi wallakini Miss Clutterbuck amerudi Hospital tena kujipumzisha, nathani hakuwa hajambo kabisa aliporudi, twatumaini atarudi upesi.

Hapa Kilimani yupo mtoto mmoja jina lake Hamadi, ametoka mpakani mwa shamba hili la Mbweni. Mtoto huyu ni mzalia wa Pemba, na umri, wake kama miaka mitano, mtoto wenyewe mzuri sana, na mtoto wa haya nyingi pia. Bassi hao wazee wake wale wamemleta hapa, baada ya kumleta hapa juma mbili tatu zikapita (mwezi haukuhitimu); baadaye huyu mama akaenda mjini ajitafutie vitu vya udoho-doho vya kujisetiri nafsi, marra akukamatwa! looh! amwangalie, aliyemkamata, akamtambua. Jee! Wakaapi wee mzee? (Naye baba huyu ni mzee na mvi zake). Akawa hana buddi kusema anapokaa. Jioni ileile baada ya kukamatwa huyu mzee, mama mtu akaja hapa Kilimani kumwarifu habari Bibi, na pia akaomba mno mtoto, aangaliwe sana, kwani atakuwa na

MSIMULIZI. 883

hatari ya kukamatwa.

Siku ya tatu yake. (ndio Bibi alipofanya karamu ya kubarikiwa Chuo cha hapa) twamwona yule mzee maskini, na mama mtoto na wanaake wengine wawili tena, na pamoja nao mtu yule aliyewakamata huyu mzee, nao watoka kwa Bwana Key na barua ya kusema mtoto huyu Hamadi na aende kwani wazee wake ni watumwa!" Ah! maneno yalitia huzuni sana. Bibi akaniita akaniambia ya kuwa Hamadi anatakwa aende zake, kwani barua imetoka kwa Balyozi juu ya huyu mtoto. Sikuwa na jibu illa nikamwendea yule askari kumwuliza kama huyu mtoto anatakwa sasa? Akanena "Ndio," Na nilipokuwa nikisema na askari, yule mtu aliofuatana nao (mwenyi kumkamata huyu mzee juzi) akaja karibu yangu akanitazama usoni nilipokuwa nikisema na askari. Nikamgeukia huyu mtu, kwani nalimsikia, mama mtu akisema yeye si mtumwa, mtu huyu ni mwivi tu, nikamwuliza, Hawa ni watumwa wako? kwa njia gani umewapata? (Kwani hawa wanakaa Mpakani pa shamba la Mbweni miaka mingi). Akajibu; "Mimi, si watumwa wangu hawa, lakini ni msimamizi wao, Nakoa mimi, ni hawa wametoroka utumwani Pemba, kwa siku nyingi nimewatafuta ndio nimewapata, saja sina buddi kuwachukua tena pamoja na mtoto pia. Na mtoto huyu alikuwa mbele yangu anikazia macho sana, naye humshikilia nguo mamaye, Niliokuwa nikimwangalia huyu mtoto akaanza kulia, lakini hatta mtoto mwenyewe hakujua anacholilia, illa ni kawaida

MSIMULIZI. 884

za utoto tu. Na wakati wote huu tunaosema, baba mtu anatemeka sana sana, lakini mama huyu ana furaha zake (na huzuni kwa mumewe,) Tukakaa kimya Marra! Huyo! huyo! anakimbia mkamateni." Ah! kumbe ni huyu mzee anakimbia, hatta kwa ginsi anavyokimbia ukiambiwa huyu ni mzee huamini hatta kidogo; alikimbia kwa nguvu sana sana. Askari na Nakoa wake wakamfukuza wakamkamata. Lakini kama si babaye Wm. Kingango, hawangalimpata.

Wakaja tena hapa, na maskini huyu mzee anatemeka kwa hofu, Bibi Mills akaja chini kashika barua mbili mkononi moja kwa Balyozi, na moja kwa General Mathews, zote hizi ni za kumwomba huyu mtoto akae hapa asiende utumwani. Yule mama akamwomba sana Bibi asimwache mtoto kufuatana nao, illa akae hapa. Akamsihi sana Bibi amtunze mtoto. Bibi akamwambia mama asiwe na huzuni juu ya mtoto kwani hataenda utumwani illa atakaa papa hapa. Askari akamchukua huyu mzee na mkewe, na waanake wale wangine wawili, illa mtoto hakumwacha aende nao. Na habari zao za baadaye hatta leo hatujasikia, illa walienda hukumuni.

Majibu ya barua za Bibi alizoandika akapata. Balyozi alimwambia kama atajaribu awezavyo kumpatia yule mtoto akae Kilimani. Na baadaye akaambiwa kama hana buddi kumkomboa yule mtoto. Bassi, hana buddi kwani na mtoto anamtaka sana akae hapa, akatoa Rs. 70 makombozi yake.

MSIMULIZI. 885

Mtoto wenyewe anakaa hapa Kilimani, mzuri sana, tena aonekana kuwa mtoto mwenyi akili na bidii ya kusoma anayo. B. M.

KIUNGANI.

April 13, tulipamba nyumba na kanisa tayari kwa siku ya Pasaka. Jioni ilikuwa ibada ya shangwi pamoja na kuandamana, tena lilipokwisha somo la pili ulikuwa ubatizo; walibatizwa watoto wawili ndio Archibald Mtanje na Samwili Mbongo, April 14, ilikuwa furaha kubwa ya siku kuu ya Pasaka, na sala zote zilikuwa za shangwi, tena siku ile ile waliingia watu watatu katika Chama chetu cha Paolo Mtakatifu, ndiyo hawa: Paolo Kazinde, Hilary Likwambe na Granville Ngoda, ndio furaha kubwa mno Chama chetu kinavyoendelea kuzidi. Ap. 15 Watoto wafanyao kazi ya kupiga chapa, na dobi, na wapishi walikwenda kushinda Bububu, na jioni wakarudi hapa. Ap. 17, Gavanori wa Zanzibar alitukaribisha katika shamba lake pande za Koani kupita mto Mwera, bassi walienda watoto 55 pamoja na Mr. Madan na Mr. King. Twalilala huko siku moja, balli kulikuwa na uhondo barabara chakula chetu kilikuwa fathili wali wa pilao na maji yetu ni madafu.

April 18, alasiri kasiri tukarudi zetu hapa. April 19, tukaingia chuoni, tena siku ile ile tulimsafirisha Mwalimu Paolo Dezu akaanze kazi yake kuwafundisha watu, pamoja naye walifuatana watoto sita waendao Magila kutazama jamaa zao muda wa mwezi.

MSIMULIZI. 886

April 20, Miss Mills alituletea watoto watatu kukaa hapa, ndio George Uledi, Denys T. Sayite, Sila Jabu.

April 24, Archdeacon Jones-Bateman alienda kisiwa Gereza, akalala huko siku tatu, kubadili hewa.

April 26, Archdeacon Farler alisafiri Magila pamoja na Archibald A. Semmanyi na mkewe, na Tomaso Yanikore.

May 3, Mr. Gillanders alisafiri Ulaya Ingreza, naye ni schoolmaster wetu, lakini hewa ya hapa haikumfaa, alikuwa hawezi marra kwa marra, ndipo akasafirishwa Ulaya Ingreza kwa amri ya daktari, tunamtarajia aturudie tena.

May 4, alituasilia Bishop Tucker pamoja na Rev. D. A. Hooper wakitoka Mombasa. Bwana Askofu alikuja kufunga safari ya Uganda, siku mbili tatu akarejea Mombasa. Na Mr. Hooper alikaa hapa siku tatu nne kiisha akaingia ndani ya meli, amekwenda Ulaya Ingreza kutazama jamaa zake. May 7, ndio siku ya kumkumbuka kufa kwake marehemu Askofu wetu, Usharika Mt. ulifanywa kwa ajili yake.

May 8, alituasilia mkewe mwalimu Denys Sayite akitoka Dar-es-Salaam.

May 14, Tumemsafirisha mwalimu Clement Kathibeni na mkewe, na Arthur Mvenya, Edward Kaonganya na George Mwonyeze, wakienda zao Nyasa. Pamoja nao wamesafiri Gray Feruzi na mkewe, Joseph Hapiwa na mkewe, na Filipino B. Yahom, wanaenda kufanya kazi ya kupiga chapa Zomba.

May 21, Tulipata simu ikitoka Ulaya Ingreza,

MSIMULIZI. 887

ikapasha habari za furaha, kama amepatikana Askofu mwingine wa Upelekwa huu wa Universities. Bassi jioni zilikuwa sala za kumshukuru Muungu maana ameitimiza haja yetu ndio kutupatia Askofu.

May 23, Wametuasilia Luke Chivoko, Arthur Kasembe, Barnaba Mtaula; na Leslie Namate, Mika Twanje, na mke wa Leonard Pesa, wakitoka pande za Mgao Lindi.

May 27, saa kenda unusu tulienda wote Ziwani mahali tunapocheza mpila, tulienda kujaribia mbio, na waliopita wenzao ndio waliochaguliwa kwa kesho kwenyi mashindano makuu ya kukimbia mbio, maana ndipo yalipoathimishwa kwa Siku ya kuzaliwa Kwini Victoria.

May 28, Saa saba unusu tulienda Mnazi Mmoja kwa kutazama mashindano, na kiwanja chote cha Mnazi Mmoja kilipambwa kwa bendera nyingi, tena zilisimikwa hema nne kubwa. Hatta ilipotimu saa nane unusu, Loooh! Mnazi Mmoja ilijaa sana umati wa watu, waume kwa wake, weupe kwa weusi. Bassi ndipo mashindano yakaanza ya namna nyingi, kukimbia, kuruka, kuvutana kamba, kutupa risasi, &c. na kwa kupiga mbio watoto wa hapa alishinda Luke Chivoko Hugh Alfred Mpetula na Frederick Taweni. Bassi sisi, wa Kiungani na Mkunazini na Kilimani tulikaribishwa kupiga mbio tu, lakini mashindani yote mengine yalikuwa ya Wazungu. Tena Chencheni askari wa Sultani na Masopai walipiga mbio. Siku hiyo ilikuwa furaha kubwa. Hatta jioni saa thenashara killa mmoja akarejea kwake;

MSIMULIZI. 888

mwenyi kupata amepata, na wangine wenyi kukosa wamekosa.

Siku hiyo hiyo alituasilia Archdeacon Farler na Mr. Griffin akitoka Magila; na Archdeacon Farler asikae balli baada ya saa mbili tatu akang'oa nanga kwenda Dar-es-Salaam pamoja na mpishi wake Tomaso Yanikore.

June 18, ilikuwa Kuimbato (concert) hapa, twaliwakaribisha Wazungu wa mjini pande za Shangani. Wazungu wengi waliokuja zayidi ya asharini, bassi ilianza saa mbili unusu hatta saa nne unusu, killa mgeni alifurahi. Saa tano unusu wakaenda zao ndani ya magadi ya frasi, naswi saa sita usiku tukalala.

June 19, ilikuwa tena Kuimbato ile ile hapa, twaliwakaribisha watoto wa Mkunazini na watoto wa Mbweni pia, killa mgeni alifurahi, saa tano killa mgeni akaenda zake, naswi tukaupiga usingizi.

Mwezi huu ametuasilia Padre Dale. Akijaliwa kupewa afya zake twatazamia aje akae hapa mahali pa Padre Simpson aliyesafiri Newala. Na Padre Tyrwhitt amesafiri kukaa Magila, na Archdeacon Farler ndiye ameshika Mkunazini kwa muda.

Nimesahau habari moja, ndio panapo June 15 Dobi ya Kiungani imehamia Mkunazini sasa, nyuma ya kanisa kubwa Christ Church. Mtg.

**TUMEPATA HABARI LEO JUNE 27 KAMA ASKOFU WETU
ATAFIKA UNGUJA AUGUST 30; NA ASKFU WA LIKOMA
ATAPITA UNGUJA JULY 30 KWENDA NYASA.**

Mtengenezaji wa Msimulizi salamu, baada ya salamu nakuarifu habari hizi: April 11, walitufikia wageni wetu watokao ng'ambo ndio hawa: So Songolo, Anne H. Songolo, Aruffo Tangani na Harriet Tangani, tayari kwa Juma Kuu. April 12, panapo saa sita Wamasihya wote, na Wanafunzi waliochaguliwa kwa ubatizo waliingia kanisani.

Ap. 13, Wamasihya wote waliokwisha kutiwa mikono walikusanyika tena kanisani kuitika majina yao, kusudi wapate kujua hesabu ya watu watakaokuja kushariki.

Ap. 14, Saa ya kwanza ikawa ibada kubwa ya Eukaristi Takatifu. Panapo saa tatu ikawa ubatizo wa watu 59, watoto wa School 8, mtu wa kazi mmoja, watu wazima 16, wanake 34. Sikutaji wote hao, billa

MSIMULIZI. 890

hao wa School Michael Mayupe, James Rubadili, Richard Mandoli, Tito Ntakayao, Barnaba Njeleza, Antonio Chikwemba, Cecil Dikani, Benedikto Chipenjele, mtu wa kazi Mika Nyamazi, ndio furaha yetu kuona wenzetu wameingizwa katika jamaa yake Masiya. Siku ile ile ya April 14, School ikatawanyika, wangine walivuka mpaka ng'ambo ya pili ya Ukamanga kuwatazama jamaa zao wa hali gani.

Ap. 21, Wanake 42 walifanywa Wanafunzi, panapo saa thenashara akatufikia Mr. Smith akitoka Chizumulu na siku ile ile wakafika wale vijana waliokwenda Kunkamanga.

Ap. 25, Alifika Mr. Nicoll akitoka Kotakota kwa Jumbe, kwani aliitwa na Mr. Atlay kuamua maneno ya humu. Aliingia ndani ya jahazi jina lake Shukuruni, cha pili Shaurimoja, Shaurimoja aliingia bwana Mbaruku na masuriya wake, pia mwanawe Jumbe wa zamani alifika jina lake Mzee, asema nimekaa sana Unguja, Pangani, tena asema mnara wa Chimoto naujua, mamaye yupo hapo Unguja. Mtengenezaji sikia bwana huyu Nicoll alipotoka tu chakulani aliwapeleka Wamakua wake kumchukua Pakosi, ana jina lingine anaitwa Kajanja, usiku ule ule walimleta bwana. Usiku ule ule akawaambia nendeni Kukuyu kumchukua Malokotela, wakaenda kumchukua wakaja naye. April 26, saa pili unusu hukumu ikaanzwa, jamaa zake Kajanja na jamaa zake Malokotela walikuja kusikia hukumu watakavyohukumiwa,

MSIMULIZI. 891

Wa kwanza mzee Kajanja akaulizwa, Kwanini ukanywa pande? akajibu, Mimi singekunywa, billa mtu wa ng'ambo ndiye aliyeniambia kama mimi ni mchawi ndio maana nikanywa pande. Akamwuliza kama mtu wa ng'ambo alikuambia wewe ni mchawi kwa nini hukwenda kwa Mr. Atlay kumwambia na wewe mwenyewe hukufanya nguvu ya kukataa. Safari ile ya kwanza nilipokuiteni hamkusikia maneno ya pande? wakajibu twalisikia, kama mlipata kusikia kwanini bassi mkavunja amri yangu. Tena akamwuliza ulikunywa mwenyewe ao kuku? akajibu kuku, akamwambia kwa sababu umesema kweli, kwani nilipokuuliza hukusema uwongo, illa yaliyo kweli kama jambo nimefanya kweli utakwenda kufungwa kwa mwezi mmoja kwa Fort.

Je Malokotela ulikunywa pande? Ah! Sikunywa mimi kanwani pangu. Hamwuliza kama hukunywa kanwani pako alikunywa nani? Akajibu amekunywa Shemeji yangu mke wa ndugu yangu. Akamwuliza, nani bassi aliyemnyweshwa Shemeji yako pande? Akajibu mimi hapa. Kanywa kuku, ao mtu? Mtu kanywa tena katapika nalo. Akamwambia kama angekufa nalo hilo pande na wewe pia ungesongwa kamba shingoni, kwani hii ni kama hesabu ya kuua mtu. Bassi sikiliza wewe utakwenda fungwa kwa miezi minne kamili. Ap. 27, alifika Dr. Hine akitoka Unangu siku ile ile Mr. Smith akaenda zake Chizumulu alipita ndani ya Jahazi. Ap. 30 Mr. Nicoll aling'oa

MSIMULIZI. 892

nanga, pamoja na wale wafungwa wake, lakini kapita kwanza Kunkamanga pamoja na mzee Chenyeta ao Mbaruku. May 1, alifika mwalimu Eustace, pamoja ua mkewe akitoka Pachia kwa matembezi tu alikuja, May 4 alikwenda zake. May 5, alifika Anne H. Songolo kwa maana mwanawe alikuwa hawezi.

Naona mtapenda kusikia kama Rev. Yohana B. Abdallah alikwenda Kumwembe, asema kama Che Mataka alimtendea vizuri sana, tena alipaona mahali pale alipojenga Mr. Johnson zamani, naye alilala kule siku kumi tu bassi. A. T. M.

KIUNGANI.

July 1, ilikuja simu toka Ulaya Ingereza, kusema Maaskofu wawili wetu wamekwisha kuamuriwa. Bassi siku ile tulishariki furaha hii, tukawa watu wa kucheza tu siku nzima.

July 18, ilikuwa harusi Mbweni kati ya Luke Chivoko na Joanna W. Mwatakaje, Tomaso Asuadi na Jemima N. Mwatakaje, Joseph Mabruki na Neema Chande, hatta jioni killa mmoja akaenda katika maskani yake. Luke Chivoko na mkewe walikuja kukaa hapa na harusi mbili zingine zinakaa Mkunazini.

Tena Adimeli amekuja na merikebu yake jina

MSIMULIZI. 893

lake H. M. S. St. George, manuari kubwa mno, milingoti miwili na dokhaani mbili, na ngome yake. Balli ilipokuja ilikuja peke yake tu, ilipokuwa ikiingia bandarini, ao ilipokuwa sawasawa na Kiungani, ikapiga mizinga ya kumsalimia Sultani wa Unguja, Looh! manuari hii kubwa mno. Ilipotia nanga wala haikukawia, marra hiyo ikang'oa nanga kuzifuatia manuari zingine zilioko vitani, maana siku hizi Waingereza wanapigana upande wa Mbaruku, mtoto mmoja wa Mbaruku jina lake Mbaraka ameasi, bassi hatta leo wanachapana. Akina kaka chencheni siku hizi wamo katika vita, hatta siku hizi hapa Unguja hawapo wengi. Baada ya Juma moja Adimeli amerudi pamoja na Balyozi mkubwa na Gavanori.

July 23, Examination ilianza hapa hatta July 26 ikamalizika, na zalitazamiwa darasa nne za kwanza tu.

July 24, Archdeacon Jones-Bateman alisafiri Mrima Dar-es-Salaam kumtazama Rev. Denys Sayite na Wamasihiya wa kule.

July 26, Aliwasili Miss Mills akitoka pande za Kepi, maana alienda kule kubadili hewa kwa ugonjwa wake. Siku ile ile aliturudia Archdeacon akitoka Dar-es-Salaam.

July 30, Examination ilisemwa saa kumi nao waliotangulia wenzao ni hawa; Katika darasa ya kwanza wa 1. Isaya Mwalinjila, 2 Petro Kilekwa na Francis Sapuli, 3. Leonard M. Kamungo. Darasa ya pili wa 1. Gabriel Ngalimasi, 2. Julius Mkonda, 3.

MSIMULIZI. 894

James Chigulu. Darasa ya tatu wa 1. Yakobo Matozwe, 2. James Kathbeni, 3. Barnaba Mnena. Darasa ya 'nne wa 1. Denys T. Sayite, 2. Fredrick Ndiga, 3. George Uledi.

July 31, Bishop Maples alituasilia, tulifurahi mno kumwona, na siku hiyo tulifurahi kwa kucheza siku nzima. Siku hiyo hiyo jioni aliingia ndani ya meli, hatta August 1 akang'oa nanga amesafiri Nyasa.

July 31, William Mpotu mtoto wa Kinyasa amesafiri Magila kwenda kubadili hewa maana macho yake thaifu.

Aug. 3, Luke Chivoko na mkewe, na Cecil Majula na Cherubini Masaniga, na mkewe Leonard Pesa na mkewe Filippo Chakale na Reuben Namalowe wamesafiri kwenda Newala.

Siku ile ile alisafiri Mr. King kwenda Mombasa kutembea kwa muda kidogo.

Siku hizi nyumba ya Kiungani ina kazi sana, zinatolewa boriti zote, mahali pao zinatiwa boriti za chuma.

Naona wengine mnajua kama zamani dobi ya Wazungu wetu ilikuwa hapa Kiungani, lakini sasa imehamia Mkunazini. Bassi sasa kile chumba kilichokuwa cha madobi kimetengenezwa kwa matamizi mangene, kimetiwa madirisha mawili; bassi siku hizi kimekuwa Class room ya darasa ya pili, ndiko wanakosomea sasa.

MSIMULIZI. 895

Tena August 7 wameingizwa watoto kuwa waalimu, ndio hawa: —
Theodore Mlomo, Gabriel Ngalimasi, Yustino Dodo, Fredrick,
Tawenir, Leslie Namate, Eriko Akuchigombo. Mtg.

KOROGWE.

Mtengenezaji wa Msimulizi salamu, na baada ya salamu twakuletea habari chache safari hii wala si nyingi. June 1, ilikuwa siku kuu ya Pentekote jioni yake ilikuwa ubatizo wa mtoto mmoja wa hapa jina lake Yusuf John Bamira. Siku ile ya siku kuu yenyewe hatukwenda mahali kwani ilikuwa siku ya Juma apili. June 4, tulikwenda kushinda Sigi kwenyi nyumba ya Mission, illa haina mtu wa kukaa pale, iko peke yake, hajapatikana mtu wa kukaa. Twalifurahi sana huko tukafanya michezo mingi, hatta jua liliposhuka tukarejea kwetu. Tena June 11, ndio siku kuu ya Barnaba Mt., watoto wote hawakwenda mahali ila watoto wa Darasa ya kwanza walienda mahali paitwa Magunga, na Padre Kisbey alikwenda pamoja nao, hatta jioni wakarudi hapa petu. Siku ile ile jioni yake tulipata habari kutoka Magila tukasikia ya kuwa Doctor Ley amefariki. Na assubuhi yake ndio June 12 siku ya Juma a tano ukafanywa Usharika kwa ajili ya roho yake. Twafurahi kusema

MSIMULIZI. 896

kama watu wa Korogwe siku hizi wanajaribu kushika siku ja Juma apili wanakuja na wanahubiriwa na Padre Kisbey. July 17 ilikuwa siku kuu ya mavuno, watu wakaleta sadaka zao naswi tukapamba kanisa letu kwa maua mengi. Na siku ya Jumaa nne jioni ilikuwa sala ya shangwi na mahubiri assubuhi ilikuwa Usharika saa ya kwanza. Y. H.

HABARI ZA KUWINDA.

(Habari hizi zimetoka katika Gazette ya Kiingereza.)

Mr. A. Hall yuko katika Hospital ya Mombasa anauguzwa, ameletwa huku na wapagazi, moja kwa moja akitoka Kikuyu, safari ilikuwa ya kusumbuka sana kwa mtu aliyedhoofika sana kwani amepona katika hatari mbili zilizompata. Amehadithia moja moja ginsi alivyopata majeraha mengi nayo habari ya kutiisha, nayo akiisimulia katika ugonjwa alio nao. Alipofuatana na mtoto wake mmoja alishambuliwa na "kifaru," akampiga bunduki, lakini alipata bahati mbaya, ijapokuwa alimjeruhi yule kifaru hakumpata mahali pema. Napo mahali penyewe hapakuwa pema Hatta hakuweza kuepuka, marra "kifaru" akampiga pembe pajani, pigo hili lilipompata likamthoofisha kabisa, hatta nguvu ya kusimama asiwe nayo hatta matafu yakawa yanapasuliwa. Akaanguka chini

MSIMULIZI. 897

amelala na huyu mnyama akawa anampigapiga tu akijaribu kumwua kwa kumchoma pembe yake, naye Mr. Hall alikuwa amelala kabisa chini lakini akaweza kumkomesha asizidi kumpiga. Bassi huyu mnyama akamkanyagakanyaga Mr. Hall, akaona hana buddi ndio bassi, lakini alimvunja mbavu na kumchubua sana ndipo akamwacha akaenda zake, (labda nionavyo aliradhi akidhani kama atakufa pale pale alipomwacha).

Kupona katika hatari kama hii ni bahati sana, lakini alipatikana na vita ingine tena aliopigana. Siku moja alijiwa na chui mkubwa ghafula, na chui mwenyewe alikuwa amemjeruhi, na Mr. Hall hakuwa na nafasi ya kushindilia tena, marra chui akarukia bunduki akamshika utaya wa juu. Hapo pakawa pigano kufa ao kupona, Mr. Hall akijaribu kujiokoa, mboto wake yule aliyefuatana naye akaja kwa ushujaa sana kumsayidia; mwishowe wakashinda baada ya kupigana sana lakini Mr. Hall alijeruhi sana tangu kitwa hatta mguu, alipopata majeraha haya akachukuliwa hatta Kikuyu; goti moja haswa lilipata majeraha sana. Huku aliuguzwa na Dr. Ansorge aliyekuwa akipitia Kikuyu wakati ule ule, akakaa akimuuguza mpaka alipopata nafuu. Furaha sana kwa kuwa amepona sasa, Mombasa aliuguzwa sana na Dr. MacDonld na anakaa pamoja na mwenziwe Captain Raikes naye pia anauguzwa vivyo maana amejeruhi katika vita ya Mbaruku.

MSIMULIZI. 898

MBWENI.

Mtengenezaji wa Msimulizi salaamu. Najaribu kukupa habari chache za hapa petu Mbweni.

June 2, ilikuwa siku ya Pentekote tulifurahi mno. June 3, ilikuwa harusi ya mwalimu Rose Muriezai, yule mwalimu wetu mkubwa, ilitawi sana watu wengi waliitwa mkubwa kwa mdogo, naye hakukaa hapa siku nyingi marra akaenda zake; akatoka hapa June 6 kwenda merikebuni wasafiri Masasi ndipo watakapofundisha chuoni wote wawili.

June 4, ndiyo Jumaa nne baada ya Pentekote hatukwenda mahali tulikaa hapa petu. Na alasiri yake ilikuwa sala ya Chama ya Mchungaji aliye Mwema kusudi kwa kumwaga Rose Mtaula, kwani yeye mtu wa Chama tangu July 1885.

June 6, tulikaribishwa Kiungani tukashinda mpaka jioni, kiisha tukarudi killa mtu katika maskani yake.

June 12, ndiyo siku ya kuzaliwa Mrs. Key akakaribisha watoto wadogo na wenyi aliowathaminia akawachukua shamba la bwana Amri wakafurahi sana kule, wakala sana watoto hatta mikate ya kusonga.

June 18, tulikaribishwa Kiungani kutazama mchezo na ulikuwa mzuri sana.

June 28, siku ya Alhamisi, Mr. Key alitoka hapa

MSIMULIZI. 899

kwenda Dar-es-Salaama na Kichwele, toka huko akaenda kutazama mahali paitwapo Kisiju kwani watu wa huko wametaka mwalimu. Alikuta mkuu wa mahali na watu 70 wakaja kumsikia kuhubiri, siku ya pili alirudi Kichwele, akarudi hapa July 3 Juma atano usiku.

Jumaa tukafanya kazi mahali pa Juma a mosi kwani June 29 ni siku ya Petro Mt. Tukashinda hapa petu hatta mnamo saa tatu tukaenda shamba la bibi mwalimu tukajifurahisha, jioni tukarudi.

July 2, ilikuwa siku kuu ya Kutakasika kwake Bikira Maryamu ndiyo siku ya Chama cha Watakatifu Wote, bassi walikusanyika wangine wao waliokuwa tayari wakapokea Usharika Mt. hatta saa kenda wakafanyiwa karamu, kiisha wakaenda kanisani kwa sala ya kusanyiko, na Archdn. Farler aliwahubiria.

July 9, ilikuwa siku ya Chama ya waalimu iliyoitwa Chama ya Mchungaji aliye Mwema; siku hiyo hiyo aliingizwa mwalimu Beatrice Mnyororo, assubuhi wakafanyiwa Usharika Mt. ulifanywa katika mathabahu ya Maryamu Mtakatifu iitwayo ya Mchungaji aliye Mwema. Tena alasiri kusanyiko na mahubiri; aliyehubiri ni Rev. J. Key, baadaye wote walikwenda shambani kwa Bibi mwalimu kupata chayi; na wenzetu watatu wa Chama wanaotoka barra, walikuwapo mwalimu Emma Pesa, na Louisa Mnubi na Faith Kayamba. Ch. S.

MSIMULIZI. 900

Je, rafiki zangu, "General Election" ndio kitu gani? kwa nini simu marra nyingi siku hizi imeleta habari yake? Nijaribu kueleza kidogo, kwani yatupasa sisi na watu wengi. "General Election" maana yake, baraza kubwa ya Kwini imevunjika, ngine ikafanyika, mawaziri wote wa Kwini wameondoshwa, wengine wamechaguliwa. Lakini yatupasaje? si Kwini yule yule mwenyi kutawala apendavyo? Ndio Kwini yule yule, lakini Kwini huyu si kama wafalme wote. Kwini huyu tokea hapo amewapendelea sana watu wake wote. Apendavyo yeye Kwini kutawala ni kama wapendavyo watu wake kutawaliwa. Hapendi Kwini kufanya neno kubwa, watu wengi wasipoitikia 'Ndio njema.' Afanyeje bassi apate kujua mapenzi yao? Hawezi kuwauliza mmoja mmoja, kwani watu wake wengi mno. Bassi aulize wachache ati lakini wenyi akili nyingi, tena wajuao mapenzi ya watu Waingereza wote, ndio wawe washauri, wa Kwini, mawaziri wake. Bassi hao mawaziri huitwa 'Cabinet', maana yake, wasiri wake Kwini. Vema. Siku hizi Kwini amewaondosha mawaziri wake. Kwani? Ameona hawakuwapendeza watu wake, akasema "Vema, ntachagua wengine." Marra baraza kubwa (House of Commons) ikavunjika, killa Mwingereza akaitwa aje kusema ataka kumtia nani katika baraza, wakachagua (ndio 'General Election') watu kama mia sita na hamsini, baraza ikafanyika tena, mawaziri wapya wa Kwini wakawapendeza. Bassi Kwini akafurahi, kwani sasa mawaziri wake walimpa shauri jema na kumjulisha mapenzi ya Waingereza wote. Na waziri mkubwa siku hizi ndio, 'Marquis of Salisbury.' Juu yake maneno makubwa yote. Nina mengi tena, lakini nafasi sinayo. Je? mwataka kujua yayidi? Labuda kesho. A. C. M.

NEWALA.

Mtengenezaji wa Msimulizi salamu, na baada ya salamu nataka kukuarifu habari zetu kidogo. Panapo Aug. 4, Tulimsafirisha Pridre J. Hainsworth, kwenda Ulaya kuuguzwa kwani amekuwa thaifu sana kwa mwaka huu wa leo, pamoja naye watoto tissa waendao Kiungani kusoma.

Tena Aug. 4, ile ile nalitoka hapa kwenda Marumba, kwani naliitwa na Mzee Matola kwa mashauri kidogo, nalifuatana na watu wengi sana wapata mia ao zayidi, lakini sikupita upesi Mkoo kwa sababu ya watu hawa naliwangoja nisafiri pamoja nao, bassi nalishinda siku nzima kule. Siku ya tatu yake tukaondoka tukaenda lalia Mwiti na asubuhi yake tukaenda kulala Mtawatawa, karibu na jangwa la Namkudenga. Assubuhi yake tukafika Marumba kama saa tatu, nikaenda kumwamkia Mzee, Matola akanikaribisha sana, nikakaa kule siku tatu. Nikatembea sana kuangalia visiwa, nikaona inchi nzuri sana lakini jua kali kama Unguja si kama kule kwetu Newala.

MSIMULIZI. 902

Na Mzee Matola nikamkuta mgonjwa sana kwa lile jeraha lake, baada ya siku tatu akaniruhusu kurudi, nikafika hapa siku ya 12 ya August nikawakuta wageni wa Unguja, ndio Mwal. Cherubini M. na Mwal. Emma Pesa, na mkewe Mwalimu Luke Ch. Na tena panapo siku kuu ya Bartolomayo hawakuja watu wengi kwa sababu ilikosewa kutangazwa kule Kanisani ilitangazwa juma a pili mahali pa juma a mosi; kwa hiyo wakakosa kuja waliposikia siku kuu imeisha. Na siku ile ile Aug. 24, Kunako saa nane watoto wa nyumbani na watu wazima wanaofanya kazi nyumbani humu walishindana, nao walioshinda kwa mchezo fullani wote hupewa tuzo lao kwa kadiri yake, palikuwa namna nyingi za michezo kiisha killa mtu akaenda zake. Aug. 26, Watoto wote wa nyumbani walikwenda zao kwao wakarudi Sept. 1, Na panapo Aug. 29, Bwana Hood aliwafanyia karamu watoto wake wa School za nje, nao pia wakashindana michezo mingi, jioni yake wakarudi zao kwa mama zao. K.Y.M.

MASASI.

Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Nina habari nyingi za kukuambia za vita na kisa chake. Mwaka huu panapo mwezi wa June huko Masasi walishuka Makwangwara wengi sana wapata miteen kuja kuchukua chumvi, na Mwinyi Mataka mwezi

MSIMULIZI. 903

ule ule akapeleka safari yake ya kuja pwani kwa mkono wa kijana mmoja jina lake Chibwana Che Maseke, lakini si mwana wa mfalme yee humwita hivi kwa ajili mfalme Mataka anamfanya kama mtoto wake. Bass akampa msafara kuuleta pwani, naye hajaleta msafara pwani huu ndio mwanzo wake nathani pia ndio mwisho wake. Alipokwisha fika njiani katoa amri kwa msafara wake wote, na msafara wenyewe karibu ulikuwa na watu saba mia. Bassi akasemaje, "Wa mulendo" wakajibu "kupilikanaga ambuje." akasema "Asonaga tesi likwangwara nu mbogaa." "Yakulya mkasimsuma tamlisye wa mwipanga ya Ambuje Che Nyambi." Na maana ya maneno haya ni hii, "Watu wa safari" wakajibu, twakusikia bwana, akasema "Kama mkimwona Mkwangwara tu njiani ndio kitoweo chenu." "Na chakula msinunue mtalishwa na raiya za Bwana Che Nyambi"(jina la pili la Mfalme Mataka). Bassi wakawa katika kuja zao mpaka Masasi. Bismilahi ya kwanza waona masakasa ya Makwangwara wale miteen, hapana mashauri tena amri imeisha toka tangu njiani, ikawa kuwakamata, wakakamatwa wawili, wangine mguu uniponye za mlimani. Na wale wawili mahali pale walipokamatwa palikuwa haswa mlangoni pa mzee Mkuti mfalme mkuu wa Masasi yote. Walipokamatwa yee mwenyewe hayuko. Bassi mwanawe Danieli Tambala akaenda mpaka walikotua Wayao ndio Magumuchila, kuuliza khabari gani hizi za kufanyizia jeuri wageni wake. Hakujibiwa la heri, wangine

MSIMULIZI. 904

wakataka kumwua akarudi. Bassi watu wengine wasafari wakaenda kutafuta pande za Mtandi chakula burre tu, bassi wakakuta kijiji cha mzee Akumbemba, wakaanza kung'oa mihogo, mwenyewe shamba kuuliza kabari gani hii? Hakujihiwa billa kumpiga bunduki, wakamjeruhi. Bassi kuona mzee Akumbemba habari hii akaichagisha vita na watu wasafari wale waliokuja mjini kwake, akawapiga watu watatu. Wayao wakaanza kukimbia mpaka matuoni kwao, wakawaarifu wenzio nao wakawacheka sana, kwani wamekimbia raiya zao kama walivyosema wenyewe kama ni raiya za Che Nyambi, bassi, Mzee Akumbemba, akapeleka nuss reale ya amarikano, kumwarifu kama hiyo alama ya saanda, kesho kufa kupona sisi nawe. Siku hiyo ilikuwa Aug. 23, bassi Mzee Mkuti na Mzee Akumbemba wakaalika vita. Wakampelekea mtu Chibwana che Masese kusema mambo haya yawe ya kusema isiwe vita. Yee asikubali, akasema vita, vita tu bassi, sijui maneno miye. Bass nao wakakubali. Assubui yake, siku ya Bartolomayo Mt. hapakuwa mtu Kanisani billa mapadre na waalimu na wengine wachache jumla 10 katika Wamasihya wote wa Masasi. Sala ya Ukaristi Mt. ikaanza kufanyika hatta mwisho wa sala Padre anatoa mbaraka zikalia bunduki za kutosha za Mnamataka, kwa dakika tu kama bunduki aroba mia na zayidi, bass wakaanza nao watu wa Masasi, zao sio bunduki haswa kama maji tu, bass Wayao leo mmoja mmoja wanashika

MSIMULIZI. 905

njia, wakafukuzwa mwendo wa siku nzima, watu wa safiri waliokufa hawana hesabu, watu wa Masasi mmoja, na Makwangwara watano, maana nao waliingia kuwasayidia watu wa Masasi kwa sababu walipigana kwa ajili yao. Nastaajabu hawa Amwembe walipigaje bunduki hizi hatta kuua watu wasita katika hizi aroba mia, hizi mia tatu na tissini na nne walielekeza wapi? Na mateka buriani, pembe, watumwa, tumbako, huko Masasi hapana thamani kwa vitu hivyo maana ulikuwa msafara mkubwa sana. Nalisikia mwenyewe amekimbia kwenda kwa Machemba kuomba msaada aje kuwapiga watu wa Masasi naye nasikia hakukubali. Akaenda mpaka Mikindani kushitaki kwa Bwana mkubwa wa Mikindani bass hatujasikia tena habari yake, tuthanivyo yuko huko huko Mikindani. K. Y. M.

KIUNGANI.

Katika Msimulizi wa August mlipata khabari ya kwamba July, mwezi mosi ilikuja simu kutoka Ulaya Ingreza kusema kama maaskofu wetu wawili wamepatikana, na wamekwisha kuamriwa, tukawa watu wa kufurahi sana. Bassi huu wa leo unatuambia khabari za kuja kwake Askofu wa Unguja. Bassi ikiwa tulifurahia kupatikana kwake hatuna buddi kufurahia

MSIMULIZI. 906

kuja kwake. Tulianza kumtazamia siku ya alhamisi Aug. 29th. Watu wote macho yao wakielekeza mnarani labda huenda wakaona sero, na ikitwekwa ingine yo yote huithania ni meli ya Askofu tu, ingawa walijua hakika kama Askofu ameingia katika meli Fransa, lakini siku hiyo huwafikiria watu wa mnarani kwamba wamekosea. Tena walijua hakika kama meli ya Askofu itatokea kaskazini, lakini siku hiyo hatta ikitokea kusini huifikiria kuwa ya Askofu, Lakini yote burre asitokee siku ya alhamisi. Bassi tukithani siku ya Ijuma mapema atakuwa mgeni wetu lakini isije hivyo. Tukatazamia tangu asubui mpaka zilipokoma saa a tissa tukaona sero, lakini ya kubahatisha tu. Lakini siku hiyo haijulikani ya kubahatisha tukajua kama ndio ile ile ya Askofu.

Ilipotimu saa a kumi unuss ndipo ikajulikana kuwa hakika meli Fransa. Bassi hatukuwa na mashauri mengi illa kubadili nguo na kushika njia ya mjini. Na zamani tulizokiondoka sisi nyumbani, tukitupa macho njia kuu twaona njia imejaa tele jamaa wa Mbweni wakienda kwa haraka sana, na shangwi na vigelegele. Hatta njia kuu siku hiyo watu wa Unguja wenyewe walionekana wageni maana tulijaa mno sisi. Na ginsi tulivyokuwa na furaha na haraka watu wa Unguja wakitutambua kama tuna habari kubwa. Bassi wote tukaongoza kwenda Shangani kwa Balози. Tukajaa mlangoni tele, Wazungu wakasimama juu barazani, wote macho yetu yameelekea baharini. Na meli siku

MSIMULIZI. 907

hiyo tukaiona kama mwendo wake imepunguza kasidi, ikakawia sana kutia nanga. Nasi ginsi tulivyokuwa na shauko ya kumwona, tukatamani kama ingeimkini kuingia majini na kuikaza meli kwa makamba na kuikokota ifike hima pwani, lakini haiyumkini, bassi tukawa watu wa kustahimili mpaka nakhotha alipopenda kutia nanga.

Ilipotia nanga akaondoka Balozi Cave pweke akaingia mashuani kwenda kumleta. Akakawia kama kwa nussu saa hivyo, tukamwona akija. Na kwa kuwa kiza kimeanza wakati huo watu wote wakasonga ngazini alao wamwone Askofu lakini ginsi tulivyokuwa wengi wangine hatukudiriki kumwona maana alisongwa mno na watu.

Lakini tulipokuwa tukitoka, akasimama mahali pa kuonekana, tukamwona sote. Marra tulipotoka kwa Balozi tukaenda Mkunazini kusali sala ya jioni.

Tukajaa sana kanisani, tukasali tukeshwa, mwisho Askofu akafanyiza khotuba kwa maneno machache akifasiri Arch. Jone-Bateman, tena tukaimba "Te Deum" (Twakusifu Muungu).

Khotuba yake ilikuja kama hivi:

"Ndugu wapenzi, wake kwa waume katika Bwana wetu Isa Masiya.

Leo ni siku ya furaha sana kwenu wala si kwenu tu lakini na Ulaya pia. Kwani sala zenu mlizokuwa mkiomba kwa siku nyingi zimetimizwa leo, na natumaini mtazidi kuniombea.

MSIMULIZI. 908

Nawashukuru sana ginsi mlivyokuja pwani wengi kunilaki. Moyo wangu ulijaa furaha hatta nikafahamu kama hakika nimefika kwangu. Nilipokuwa nikitoka Ulaya si watu wengi walionisindikiza hatta pwani, lakini hapa nimewakuta mia marra mia waliokuja kunilaki. Marra moyoni mwangu nikakumbuka habari ya Paolo alipokuwa pwani ya Atene na watu wengi wakija kumwaga.

Na mimi nataka sana mniombee nipate kuwa mtu wa kufaa kwa kazi hii kama maaskofu wenu waliofariki. Tena mnaona msalaba huu niliouvaa ni wa marehemu askofu wenu, bassi nami nataka kwa unyenyekevu kufuata maisha yake takatifu.

Tena pete hii niliovaa pia ni ya marehemu askofu wenu nami kwayo nataka kujiunga kwa maisha katika kazi ya upelekwa huu. Tena nataka mniombee nipate kuweza kusema nanyi kwa lugha yenu wenyewe." Sept. 2, Siku ya jumaa tatu ikapigwa amri na askofu mwenyewe kucheza killa mahali katika Mission zote.

Sept. 22, juma a pili likatokea jambo jingine kubwa sana litupasalo kufurahia sote watu wa upelekwa huu, ndilo kuongezeka ungoje katika watu weusi. Naona wangine wanakumbuka kama walikuja hapa zayidi ya miaka miwili imepita sasa waalimu Watatu Daudi M. Hugh S. M. Siprian. H. Ch. kujifanya tayari kwa kazi ya Ushemasi. Na juma a pili hii ndipo wakaamriwa daraja hii takatifu. Waliamriwa katika Christ Church, Mkunazini.

MSIMULIZI. 909

Sala zilianza kama saa pili kassorobo.

Sisi hapa Kiungani tulisali sala ya Eukarist saa thenashara urobo tulipokwisha marra tukala tukashika njia kwenda mjini. Na Mweni nao kathalika. Bassi ikitimia saa a pili tumekuwapo sote Mkunazini.

Tukaanza kujazana Kanisani kabla kengele hazijaanza. Hatta zilipopigwa kengele na kunyamaza Kanisa limejaa watu, chini, na juu darini, hatta katika vile vipengee vya juu kabisa mkajaa watu, wakionekana vitwa tu. Bassi kwanza ulikuwa uwandamano (procession). Walikuwapo makasisi sita, na mashemasi wanne. Na waimbaji zayidi ya arobaini. Walipokwisha ingia ukaimbwa uimbo, tena Archdeacon Jones-Bateman akatoa khotuba. Baada ya khotuba sala zikaendelea mpaka walipoamriwa Ushemasi na sala ya Eukaristi. Na pamoja nao aliamriwa Mr. W. Bishop aliyetoka Ulaya Ingreza siku hizi katika College ya Dorchester.

Sept. 15, Mwalimu Arthur Kasembe alifanywa Msomaji. Na asubui yake jumaa tatu wakatiwa mikono watoto kumi na moja.

Sept. 23, na 24, tulicheza kwa furaha yao mashemasi.

Sept. 24, watoto wa Kinyasa wamesafiri kwao. Mmoja wao ndio Mwalimu Michael Chikokota amepolekwa kwenda kushika kazi ya kufundisha. Lakini wengine twatumaini watarudi.

Sept. 26, Askofu amesafiri pande za bara Newala pamoja na Mashemasi wapya wote watatu.

MSIMULIZI. 910

KILIMANI.

Mtengenezaji wa Msimulizi Salamu. Katika Msimulizi uliopita mlisikia kama Bibi Mills aliugua sana, hatta akaambiwa na mganga aende pande za Kepi, bassi alienda, na hewa ya huko ikamfaa sana akarudi mwisho wa mwezi July, alionekana kuwa na afya, tukafurahi kumwona. Na mahali petu hapa tunapokaa pamezidi kutegemea zayidi kuliko palivyokuwa siku hizi za zamani kidogo; umetiwa ua wa vyuma, na matumizi yake ni kuwafungia Watoto wadogo (Day boys) wanaokuja kusoma kwa zile saa za kupumzika kusudi wasitoroke chuoni; kwanza hawakupenda walikuwa wakilia sana, lakini sasa wanapenda sana kufungiwa humo.

Tena mabibi wametengeneza bustani ya maua, na wamepanda maua yanaanza kukua vizuri. Na pia tumejitengenezea kiwanja cha kuchezea mpila na siku hizi tunaanza kukitumia. Na habari za chuoni mwetu ndio ya kuwa chuo kinaendelea sana, watoto wamezidi kujifunza zayidi, na kuendelea mno mbele kuliko zamani.

Sept. 2, Tulipata siku nzima ya kucheza kwa furaha ya kufika Bwana Askofu, na keshoye tulifurahi mno kwa kumwona kuja hapa kuangalia mahali petu; watoto wakamwimbia na kufanya "Drill."

Na siku zizi hizi tumepata watoto zayidi wa

MSIMULIZI. 911

kukaa humu. Mtoto mmoja mdogo Paolo Sudi umri wake miaka miwili unussu, Mlisho, Subeti, na Ramathani, lakini hawakuja wote siku moja illa wametanguliana siku chache chache. Na siku hizi, Sheldon Mwalimu wa humu nyumbani anakaa Shamba kupumzika kwa muda kitambo, na Mwal. Benedict Madalito anasayidia humu nyumbani mahali pa Sheldon.

Sisi tunaokaa nyumbani hapa Kilimani ni sisi wale wale tuliokuwa katika "Choir Shool" Mkunazini, billa tumehama tu, kwa kuwa kule mjini hatukuwa na afya nako sana, na wenzetu wengine waliosoma Mkunazini katika "Choir School" wameenda Kiungani wengi kusudi wazidi kusoma na wengi wao wamepata kuwa Waalimu. Bassi Sept. 19, Tulipewa siku nzima kucheza kwa ajili ya Theodore Mlomo, Gabriel Ngalimasi, na Yustino Dodo kwani walifanya vizuri sana katika Examination yao Kiungani na wameendelea sana hatta sasa wamekuwa Waalimu, tukaifurahia sana bidii yao.

Tena Waalimu Daudi Machina, Sipriani H. Chitenje, na Hugh S. Mtoka wameamriwa kazi ya Ushemasi, twalifurahia sana, na zayidi mno kwa Hugh Mtoka, kwani na yeye amesoma katika chuo kile kile cha Mkunazini tulipoelemishwa na sisi. Bassi hivi tunavyoangalia wakubwa wetu ginsi wanavyoendelea kututia moyo sana na sisi tupate kuendea mbele na kuwa kama wao. Salamu. B. M.

MSIMULIZI. 912

KOROGWE.

July 30, Akatuwasilia Padre Kisbey akitoka Magila pamoja na Mwal. Alfred Juma. Siku ile ile usiku wakatuwasilia Rev. Firminger pamoja na Mr. Chilvers na wapagazi wakitoka Mkuzi huyu Rev. Firminger amekuja tembea tu.

Aug. 1, Mwalimu Alfred Juma akaenda zake Mkuzi halafu atarudi kukaa hapa.

Aug. 8, Padre Fiminger akaenda Magila.

Aug. 13, Akutuwasilia Mwalimu Alfred Juma pamoja na mkewe wamekuja kukaa.

Aug. 15, Padre Kisbey akaenda Magila kwa kusudi la kwenda Unguja maana hawezi sikuzote hizi.

Siku ile ile alipotoka Padre alituwasilia Mwalimu Lawrence Mmaka amefuatana na Mdachi mmoja watoka pande za Msasa, wakatembea juu ya vilele vya vilima wanatafuta thahabu illa hawakupata, jina lake huyu Mr. Leamerman. Aug. 16, Mwalimu Lawrence akashika safari kurejea Magila, Mdachi akaenda Mazinde kwani huyu Mdachi alimtaka awe mkalimani wake maana hajui Kiswahili illa neno moja ndio "Nenda upesi." Bassi alihuzunika kumkosa tena kwani alifuatana naye sababu hana shughuli, ni wakati wa matembezi.

Sept. 4, Tumefurahiwa mno kumwona Padre Kisbey akiturudia mwenyi afya toka Unguja. Na akatuarifu

MSIMULIZI. 913

kama Bwana Askofu wetu amewasili Unguja.

Sept. 6, Ametuwasilia Mdachi mmoja mganga anakwenda Mazinde alikuwa na asikari wengi na wapagazi alifika hapa Kilimani kuangalia majengo na killa jawabu, tena akarejea kambini kwake kwani hema yake iko chini nje ya mji wa Korgwe. Kanisa letu jipya karibu litakwisha. A. J.

MKUZI.

Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Safari hii hatuna maneno mengi. Illa kwa mwezi huu tuna rotuba kidogo ya riziki, kwani watu wengine wamepata mihindi ya kadri, na mtu unaweza kupata mitatu kwa pesa. Na nzige shidda kuonekana sasa sijui wakati ujao mbele.

June 1, alifika hapa Elvani Kachawa kutembea katika inchi yetu ya Bonde. Na June 3, Rev. John S. alitoka hapa kwenda Unguja na siku hiyo hiyo watoto wetu walienda kushinda Kakindu ndio mahali katika njia ya Pangani.

June 6, Yakobo Chamdangwe alioa hapa, jina la mkewe ndilo Manyangasa naye ni mwanafunzi; Rev. Samwil ndie aliyemwoza. June 8, akaja Padre Woodward kutufanyia Eukaristi kwani Padre Palmer alienda Magila kwa ugonjwa Dr Ley. June 12, Mr Brent na

MSIMULIZI. 914

watoto wetu walienda Magila kwa siku kuu ya Eukaristi. Assubuhi yake akafika hapa Hugh P. K. na watoto wake wakienda Unguja kwani bibiye ni thaifu sana.

June 15, akaturudia Rev. Gerrish akitoka Cape pamoja na mafundi wajao kujenga pande hizi za Bonde.

Na panapo June 16, tukafanya siku kuu yetu ya Eukaristi hapa. June 24 Padre wetu Dr. Palmer akatoka hapa kwenda Unguja pamoja na Wilfred Ponda na Daudi Sezua wajao Kiungani kusoma, na John D. Saidi ajaye kupunga hewa kwani ameugua siku nyingi sana.

Habari ya simba na makafara.

Mmesikia wangine ginsi inchi hii ilivyoingiwa na hatari ya simba amekamata watu wengi hatari hii tujuavyo haiwezi kuondoka illa kwa kudra ya Mwenyezi tu. Na pande za magharibi za Bonde ndiko ilikoshika hatari hii. Bassi siku ya July 5, wakati wa magharibi tukaona watu wengi wake kwa waume na watoto pia wamevaa selaha zao na wamejifunikiza kwa majani na kinu kina ngozi ya mbuzi na ushanga, huenda wakiimba nyimbo za vita, na huingia killa mji kucheza na kupewa pesa. Na kafara hilo ndilo la kusema simba ataondoka asikamate watu. Na aliyetoa amri ya kafara hili ni (mgonezi) nabii, na pesa zile zitokazo killa mji humpelekea yule mgonezi. Bassi

MSIMULIZI. 915

ndugu zangu inchi imejaa kutomfahamu Muungu.

July 20, Padre Dr. Palmer na Padre Firminger wakatufikia hapa kutoka Unguja pamoja na Clement Lunguno na John D. Saidi.

July 27, tulipamba kanisa letu tayari kwa siku kuu ya mavuno. Assubui yake ni juma a pili ndio sikui kuu yenyewe watu wakaleta kadri ya mihindi na walivyopata. Juma a tatu July 20, watoto wetu tukawapeleka killa mtu kwao kukaa muda wa juma a tatu Aug. 10 Padre wetu alishikwa na homa Jumaa tatu akachukuliwa Magila kwani homa imemzidi sana.

Aug. 16, John D. Saidi ametoka hapa kwenda Magila tayari kwa safari pa Unguja kwenda kusoma tena; na Mgaya aenda Mkunazini kwa bwana H. Lister. A. A. S.

MSIMULIZI. 916

KUFARIKI ASKOFU MAPLES.

Ee Simu, Simu! Ginsi unavyoleta marra furaha, marra huzuni, nayo ya kuchomachoma moyo na kutuangusha mavumbini.

Jana tuliletewa, leo tumeondolewa!

Jina la Bwana libarikiwe.

Ee Simu, jicho la ulimwengu, kama juzi upo Blantyre, ukaona mtu anakuja toka Matope mbio, na habari anazo, anatweta, hawezi kusema, illa soma tu. Ukasoma "Askofu wa Likoma ametota majini huko Nyasa." Bassi kwa kupepesa jicho watu wa London (safari ya juma sita) wamepata khabari, washangaa, hawasadiki vema. Wakatuuliza huku Unguja kwa simu, "Ee ndugu, kweli hiyo?" Tukajibu, "Hatujasikia." Tukauliza wa Blantyre (yote hayo kwa kope la juu na chini} wakasema, "Ndio hiyo."

Ndugu, tulizane kidogo, hatuna buddi, kwa ajili ya babaye mzee huko Ulaya aliyefiwa na kipenzi chake, na ya jamaaze pia; kwa ajili ya ndugu zetu wa Nyasa, kwani juzi walitokewa na mchungaji mwema wa roho zao, baba kwa umri, baba kwa upendo, baba kwa uaskofu, leo hapana; kwa ajili yetu sote, kwani aliye peke yake kifungo cha upendano na kujuana Mission wote, ndiye aliyetwaliwa.

Habari hizi za kutisha moyo, tungoje kwa kimya tukikumbuka Muungu atendapo miujiza Kwa siri aendavyo; Hatua zake ziko baharini, Atenda aendavyo. R. I. P.

MAGILA.

Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Sept. 14, Ilikuwa siku kuu ya Msalaba Mtakatifu kwa sisi watu wa Magila inakuwa siku kuu kubwa sana, kwa maana Kanisa letu kubwa la Bonde laitwa Msalaba Mtakatifu. Bassi saa thenashara assubui ilikuwa Usharika Mt. kwa waimbaji kama ilivyo desturi yetu kwa killa siku kuu kubwa, waimbaji watangulia kupokea Usharika, walipotoka ilikuwa saa a kwanza wakaenda kunywa kahawa kwa maandazi wapate kuwa tayari

kwa Eukaristi kuu, nayo Eukaristi kuu ilikuwa saa mbili. Kanisa letu likajaa sana wake kwa waume. Padre Petro ndiye aliyehubiri, na baada ya Kanisani ikawa mchezo kwa watoto kujifurahisha wenyewe, lakini kwa kuwa ilikuwa siku ya Juma amosi haikuwezekana kufanywa karamu ikawekwa kwa Alhamisi iliyofuata, bassi siku ya Juma a tano barua ilikwenda Mkuzi kuwaita watoto wa Mkuzi waje walale hapa tayari kwa karamu, bassi siku ileile ya Juma a tano ng'ombe akachinjwa nyama ziwe tayari.

MSIMULIZI. 918

Siku ya Alhamisi, assubui ikawa Usharika Mt. baadaye ikawa mchezo wa dandalo na tinge, na mizungu, saa atano ikawa karamu, hatta alasiri, Bibi Boyd alifanya michezo na watoto wa kike kuwafurahisha alivyoweza. Saa a kumi yalikuwa mashindano ya watoto waume kwa zawadi, yalikuwa ya namna nyingi, kupiga shabaha kwa bunduki, kwa mishale, kupiga mbio, kupiga mbio kwa mguu mmoja, kudaka mpila, hatta saa thenashara machezo yakaisha.

Sept. 16, Waliondoka Rev. Gerrish na Mr. Mellor kwenda Unguja, halafu wasipopata afya zayidi kwenda Ulaya. Dr. Palmer aliwapeleka mpaka Tanga, lakini Mr. Roberts aliwapeleka mpaka 'Station' ya Mheza, ndipo linapofika gari siku hizi ndio 'Station' iliyo karibu naswi. Tukiwa na rafiki yetu tumpendaye tukisikia amefika Tanga twaenda kumngojea Mheza ndio mwendo wa saa moja urobo, tangu hapa hatta 'Station' hiyo.

Tena alasiri waliondoka mabibi wawili ndio hawa: Miss Dunford na Miss Brown kwenda Misozwe kupunga hewa na tumesikia kuwa wamefika hatta Mlinga mlima ule mrefu sana, hatta siku ya Juma atano wakarudi hapa.

Sept. 23, Tulipotoka chuoni saa nne marra tulisikia kelele za watoto, akakimbia mmoja kusema kama nyoka yule mkubwa anayelitwa chatu amekamata mbwa, bassi haenda kwa Padre haazima bunduki lakini haikuwa bunduki ya marisao; bassi tukatwaa ya

MSIMULIZI. 919

risasi, tukashuka mimi na mwalimu Samwil tulipofika amemwacha yule mbwa kwa sababu ya kelele tukarudi marra tulipofika mjini mtoto akaja akasema kama amerudi, bassi tukashuka, kufika, amemwingiza yule mbwa maguguni kando ya mto amvuta paangoni, marra tukimtazama haonekani marra kwa bahati alitoa kitwa amwume mbwa amkokote, hakudiriki ilimtoka bunduki mtu aliyekuwa tayari, kwa bahati kati kati ya kitwa risasi ikampasua, marra akaja mtu aliye hodari akachimbua, maana nussu ya mwili ilikuwa paangoni. Mtu huyo hodari aitwa Bwambwala, akalifikia akalifunga kamba akakuta nje watoto wa Mission wakamchukua mjini, Padre akamtafuta mtu kumchuna ngozi, na ngozi yake ipo hatta leo. Sept. 27, ametuaga Bwana Henry N. kwenda Unguja yeye na mkewe kubadili hewa kwani siku hizi zote alikuwa hawezi mguu hapa Magila.

Sept. 31, ametuwasilia Mr. Brockway akitoka Korogwe kwani alikwenda kubadili hewa huko kwa nussu mwezi maana alikuwa hawezi.

Sept. 31, Tulishika siku kuu ya Mikael na Malaika Zote, bassi Mr. Roberts alitangulia siku ileile ya Mikael pamoja na watoto wawili kwenda Msalaka. Bassi Juma atatu assubui sisi na watoto tukafuata na mbuzi na mchele marra tukafika Msalaka tukakaa kidogo marra gari hili. Wazungu, na Wahindi, na watu weusi, wamejaa tele marra Madoicha wakamsalimia Mr. Roberts, hilo likakimbilia Station,

MSIMULIZI. 920

marra baada ya saa moja unusu likapita tena kwenda Tanga. Tukashinda hatta jioni tukarudi majumbani mwetu.

October 1, Zimeshuka nzige zikafunikiza kipande chote cha miji ya hapa tangu milima hatta mashamba. Oct. 5, Walishikwa na homa mabibi wote Miss Boyd na Miss Dunford na Miss Brown kwa hiyo Dr. Palmer akaja kuwatazama apate kuwapa dawa.

Sasa nyumba yetu ya kilimani imeisha moja na moja bado, watoto nussu wameishahama wakaa huko huja hapa asubui na huenda jioni baada ya chakula.

Oct. 10, amepita Mdachi na safari kubwa akitoka Kilimanjaro jina lake Dr. Widemann lakini hakulala hapa amekwenda kulalia mbele karibu na njia ya gari apate kuingia linapokuja asubui. L. M.

MKUZI.

Mtengenezaji wa Msimulizi, salamu, wa baada ya salamu, leo sina habari nyingi. Panapo August 25, ndio siku kuu ya Bartolomayo walifanywa watoto wetu wawili kuwa Wanafunzi, ndio Lukuti na Nkuninga: jioni yake Padre H. W. Woodward alifika hapa pamoja naye Charles Mfuko

MSIMULIZI. 921

kwenda soma Kiungani, na James Mwaimu kutembea Unguja.

Sept. 1, Padre wetu Dr. Palmer alitoka hapa kwenda Magila illi amsindikize Rev. H. Gerrish kwenda Unguja: na mtu aliyefuatana naye aliporudi akasema Padre ameenda Unguja kumwona Askofu wetu, bassi haji huku mpaka Uzaliwa, nami nalipata barua yake ya kusema hivyo. Sept. 8, Mwalimu A. Machaku alilalia hapa tayari kwa safari ya Unguja na watu wake. Sept. 12, Padre Woodward alitufikia hapa akitoka Unguja na Mwalimu Basil, walifika hapa kama saa sita adhuuri na saa nane wakaenda zao Magila.

Panapo Sept. 18, Mr. Brent na watoto wetu walienda Magila kucheza pamoja na watoto wa huko kwa siku kuu yao iliyopita siku nne tu. Na Jumaa mosi yake wakarudi.

Katika inchi hii yote wameambiwa wasicheze ngoma ya dandaro illi nzige wasije na kuharibu mihindi: na amri hii imetoka mlima wa Mlinga na kwa mgonezi (nabii) mmoja. Bassi inchi yote imeenea watu wasicheze. Hatta Sept. 22, wakati wa jioni tukasikia kelele nyingi sana za watu waume na wake; tukatoka kuona ni nini? Tulipofika nje ya boma letu, tukauliza kunani? Wakasema ni geleta la mognezi jinale Mkundawantu asema liende killa mji mpaka likatupwe nyikani, illi kuzuia nzige.

Geleta. Geleta ndio kafara. Bassi geleta hili liliamriwa likifika killa mji, na watu wa mji killa

MSIMULIZI. 922

mwanamke afagie nyumba yake na kutia takataka zake ndani ya kikapu; nao wakiisha hutoka wakiendea mji wa pili pamoja na nyimbo zao. Na watu wa mji ule huchukua vile vile hatta mji mwingine, vivyo hivyo hatta nyikani.

Nzige na Arusi.

Pana mahali karibu na upande huu, njia ya kuendea Magila lakini kama mwendo wa saa unussu panaitwa Kileleu. Huko kuna mtu kooa, na mtu yule akasema sharti mimi arusi yangu iwe na ngoma ya dandaro, watu wakasema haifai, kwani mlinga amekataza, yeye akasema sharti iwe, nayo ikawa. Walipocheza hatta asubui yake nzige wengi wakala mihindi yote ya yule bwana arusi na bibi arusi na wazee wao pia; na ya killa mtu aliyeshuhudia arusi hiyo. Tena baadaye wakasikia sauti yatoka kati ya wale nzige ya kuwa: "Naghamba ni nkondo nitimie wanangu, hivi kumbe ni dandaro, basi inywi wapuna wangu jai mampemba yoshe." - "Nalidhani ni vita nikawasaidie watoto wangu, lakini ni dandaro, bassi nyie askari wangu kuleni mihindi yote." Na maneno yote hayo yatoka mlinga, kwani huchukiwa sana na ngoma za dandaro. Bassi ndugu zangu maneno yote hayo ni ya Washenzi wasiomjua Muungu waaminivyo. Kwa maneno hayo yaonya ya kuwa wamo gizani sana, hawajaona Nuru kama tulivyojaliwa sisi Wamasihiya. Nalisema mbele ya kwamba Padre wetu ameenda Unguja kumwona Askofu. Bassi panapo Sept. 28, alijaliwa kuturudia tena salama.

MSIMULIZI. 923

Oct. 5, madhabahu yetu tuliiondoa, na mpya ikaanzwa kujengwa ya mawe, kubwa kidogo kupita ya kwanza.

Tena alasili ya Jumaa mosi, siku hiyo hiyo ya Oct. 5, tulifanya kukutana Wamasihya wote, na wanafunzi penyi chuo chetu cha wanawake; na huko tulijaribu kusemezana na kutengeneza kidogo mambo yetu ya Umasihya, kwani twajiona tu walegevu sana siye wa Kanisa la Mkuzi juu ya kawaida zote za dini; bassi mengi tumepatana yaachwe, na mangine tumeyaweka hatta tujaliwapo kukutana tena Kanisa lote la Bonde mkuu wetu alikuwa Padre wetu na mzee Edward Semngojo.

Oct. 6, ilikuwa furaha kidogo kwetu, kwani tulipata vijana wa kike waliofanya bidii sana kwa mafundisho yao, na siku hiyo wakafanywa Wanafunzi, majina yao Malukindo, Makilua na Makiango. Hatta alasili ndipo tukapata habari zilizo nzito sana na mashaka, za kufa kwake Askofu wa Nyasa, jioni tulisema sala ya wafu kwa ajili yake, na asubui yake Juma a tatu ukatolewa Usharika Mt. — R.I.P.

CHITANGALI.

Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Jee mzee utarathi juu yangu kwa kuwa natia mkono wangu

924 MSIMULIZI.

kukuandikia karatasi hii kwako? Nathani umerathi sana. Bassi sikia habari wetu hapa Chitangali. Nathani wanginge wenu mlipata kusikia kama tutahama Chitangali kukaa mahali panginge, kwa kuwa hapa Chitangali tangu kuja watu wanajaribu kulima kama wawezavyo wallakini hawapati chakula marithawa. Bassi Mzee Barnaba alikwenda siku moja, kasikazini ya Mwiti kuwinda, bassi alipoona mahali pazuri sana, tena inchi ya rotuba sana, na alipendezwa sana napo na mahali hapa panaitwa Chiwata na mnajua maana ya jina hili? Ni inchi sawa, lakini usithanie kama na mahali hapa ni inchi sawa, la. Bassi mzee Barnaba Nakaam tangu kupaona mahali hapa roho yake haikuwa rathi. Bassi aliwaamuru watu wake wanginge kwenda kuanza kulima, bassi wengi wakaenda, hatta mwisho Chitangali ikawa tupu pasipo watu, hatta mzee Barnaba Nakaam akamwarifu Padre tuhame kwani watu wamekwisha enda zao, naye alikubali, bassi tangu Aug. 10, tukaanza kufunga mizigo na kuchukuliwa kwenda Mwiti. Hatta Aug. 23, Padre na sisi sote wa nyumbani tukang'oa kwenda Mwiti na asubui yake ikawa siku kuu ya Bartolomayo Mt. Mwaka huu siku kuu hii kwetu sisi imekuja wakati mbaya sana hatukufayidi hatta kidogo kama miaka iliyopita. Lakini siku ile tuliyotawanyika kule Chitangali, kweli twalitawanyika sana, Mwalimu Daniel alikuwa akienda Miwa kukaa kule mpaka ajapo Rev. Cypriani H. Chitenje, mimi nikaja zangu hapa Mwiti pamoja na

MSIMULIZI. 925

Padre. Bali tangu siku hiyo hatukuonana na Mwalimu Daniel U. mpaka Sept. 17, ndipo alikuja kutuangalia. Bassi ndugu zangu juweni kama sisi tangu kuhama kule Chitangali halijulikani tunalotenda tunakaa hapa Mwiti pasipo Kanisa wala nyumba, watoto wanasoma katika kibanda kidogo tu.

NEWALA.

Bwana wa Msimulizi twakusalimu. Tumeona sisi tukaa huku kama wee Bwana wanung'unika mno juu yetu, ukisema hatukulishi kama ilivyo kawaida yako, bassi urathi Bwana, wallakini nimewaambia wangine kana umekasirika, nao wanakusanya chakula cha kutosha sana kwa mwezi huu ndicho hicho:

Oct. 1, Mfalme Yohana Matola baada ya Ubatizo wake alionekana kama ni thaifu mno alao la uzima halikuwamo mwake, na akili zilimpotea husema maneno asiyo zoea kusema siku zote. Isipokuwa aliwaambia neno moja watu wake lililo zuri, akasema kama, "Sasa naona kufa kukaribu ni heri mnichukulie karibu na kanisa kwani naona baadaye mtaona vigumu nikifa kunichukua Makonde." Nao watu walimsikia wakamleta hapa akauguzwa. Oct. 5, Tukajiwa na wageni wengi ndio Bwana Askofu, Rev. Daudi M, Sipriani

MSIMULIZI. 926

H. Ch, Hugh S. Mtoka. Tulifurahi mno kwani hawa wote wakiwa wamejifunga siku hizi hizi kwa kutusaidia sisi huku. Tunamshukuru Muungu aliyetuchagulia upesi mchungwa wa roho zetu, twazidi kumwomba Muungu amjalie kwa afya. Tulienda kama mwendo wa saa nzima na bunduki zetu, zikichapwa vema, Bwana Askofu alicheka hatta upeo wa kucheka. Wallakini tulipofika mjini hatukuthubutu kupiga maana mzee Matola ugonjwa wake ulizidi. Tena siku ile ile aliwasili Dachiki akitoka Masasi, alienda kusudi kutengeneza vita ile ya mwinyi Mataka na watu wa Masasi walikuwa Wazungu wawili na askari 54, pamoja nao mwinyi Barnaba Nakaam. Panapo Oct. 8, Dachiki huyu Herr Stantzler (kwani ndilo jinale); aliondoka hapa kwenda kwa Niumansa illi kummilikisha awe jumbe mkuu juu ya Wamakonde wote, sheria, hukumu, athabu, billa asiue tu, hivi ndivyo alivyowaambia wote. Na Mwinyi Matola ni mtawala wa Ng'ambo hii ya Rovuma yote wahadi Ngomano. Bassi hawa Majumbe wakubwa jambo lolote wanaweza lihukumu billa kuua mtu hapana, hayo ni ya Ewana mkubwa Herr Stantzler.

Oct. 10, Padre Cecil Majaliwa na Mwalimu Danieli Usufu waliwasili hapa toka Mwitiki illi kuja kumsalimu Bwana Askofu. Oct. 12, Yee amerudi kwake akifuatana na Rev. Hugh Mtoka na mkewe. Oct. 13, Tumepatwa na huzuni ndio ndugu yetu aitwa Ibrahimu Limbanga amejikosea mwenyewe bunduki amekufa. - R.I.P. Alifia

MSIMULIZI. 927

Mkoo siku ile ile ilinipasa niende kumzika, nikaenda. Oct. 14, Bwana Askofu ameondoka pamoja na Rev. Daudi kwenda Miwa kuangalia. Bassi mnamo saa nne unussu mfalme Matola alikata roho. - R. I. P. Kengele ya ishara ya mauti haikupigwa maana tulikuwa na mgonjwa mwingine alikuwamo hatarini kabisa. Mnamo saa tano bunduki zilichafukiana vibaya, wakati huo ukiitwa husikii. Hii ni ishara ya kuwaita wafalme wa mbago mbago, kwani ni rahisi kutambua wao wakisikia bunduki zinavuma hivi. Tangu alipofariki mpaka leo jumla ni siku tissa zimepita bali kucha kutwa zapigwa kwani killa ajaye hupiga, kwani hii yaitwa kilio cha kiume. Oct. 15, majira ya saa saba akazikwa, amezikwa katikati ya mji wake palepale penyi baraza yake ya zamani. Tena juu yake wamejenga nyumba kubwa kwa kadri, nyumba hii imezekwa kwa nguo, kaburi lenyewe limewekwa vizuri sana. Hii ni huzuni yetu kubwa kwani tangu yee mwenyewe alipobatizwa mjini hapa wote walikuwa wakishawishwa; tena amewavuta wengine waliofanya kama kusinzia kidogo juu ya dini yao. Mzee Matola ni mfalme wa kwanza wa Newala hii yote wahadi Ngomano yachimbwako makaa. Yee ndiye aliyewakaribisha 'missionaries' kwanza kwa neno la Doctor Livingstone walipokutana huko Rovuma. Watuwengi wanamwombolezea, husema hatatokea mtawala wa amani na maarifa, na akili, na hekima, kama yee. Na mji huu sasa hutawala Matola mdogo. Dachiki kampa bandera akitweka daima.

MSIMULIZI. 928

Naye ni kweli Muungu alimfanikisha sana duniani humu kwa mambo mengi. Lakini sasa iliyopo tumshukuru Yeye aliyempa haya yote, kwani ameona vema ampumzishe katika kazi hizi alizompa. Kweli alionekana mtu mwenyi fikara na maarifa juu ya kazi yake. Tena alishika sana shauri alilopewa na marehemu Askofu aliyetuacha mwaka jana, aliambiwa yampasa sana atoe sadaka killa siku kuu kubwa, haya tumeyaona sisi wengine yanatendwa dayima. Tena alitoa sadaka sana ya kushukuru alipokwisha batizwa.

Oct. 17, Bwana Askofu amewatia mikono watoto wa humu nyumbani kama kumi na sita.

Oct. 18, Tumepata hakika hasa ya vita ya Machemba na Makwangwara, ya kuwa Makwangwara walitua karibu na mji wa huyu Machemba. Bassi nussu ya watu wa Machemba wakaondoka kuwalaki; lakini walirudi wote mbio wakaletwa wahadi kuwapitisha penyi makao yao; maana vita hii imekuwa si vita tena illa mambo tu kwa ginsi walivyo wengi mno. Bassi nyie mjuwao njia ya Lindi ati husema masakasa yameanzia mto Lukredi wahadi Ngurumamba Loo! Sijui kama wamesalia wengine kwao. Na Wangoni hawa wanasema kama sisi haturudi mpaka tuishe, kama sivyo sisi tumwishe yeye. Kwani twaona haya kwa Bambo Songea tukasemeni sisi, tumeshindwa na leo pia? Heri kumwambia tumeshindwa tumebakia sisi kenda tu, aalike vita ingine na haturudi mpaka maisha. Hizi ni khabari za vita. D. M.

MSIMULIZI. 929

Oct. 24, Edward Abdallah amewasili hapa toka Lindi, anasema Mpatila hapana hatari, balli penyi hatari ndio toka mto Lukredi mpaka Ngurumahamba, maana humu mwote Wangoni ndimo walimojazana, wamepiga mji wa Abadllah bin Ngunde, tena mji wa Nyama mwipwaye Machemba, tena kijiji cha Said bin Machemba, lakini sasa wamezuiwa na Herr Stantzler wasubiri kwanza; kwani yeye anangoja asikari toka Kilwa Kivinje na Dar-es-Salaam. Lakini Edward amesema steamer 2 zilikuja, nazo zote hizi hazina nafasi hatta kwa kukaa jinsi walivyoyapakia manjolinjoli. Lindi hapawaweke kwa wingi. Bwana mkubwa huyu Herr Stantzler alienda hatta kwa Chiwonda mtoto wa mzee Machemba bassi amekubali bandera ya Dachi, akajitoa kabisa mnamo ujamaa wa Machemba, palepale Bwana huyu aliandika barua kwa Machemba kumwambia saa za msamaha ni hizi tu ukitaka amani sema sasa hivi, naye akajibu barua ya shari, akisema labda nife kwanza ndio hawo watoto wangu waangukie miguu kwa mzungu, balli mimi mwenyewe nimpange urafiki mtu wa baharini kama samaki haiwezekani, lililopo kwangu ndilo la kusema na ailete hiyo vita nife bassi. Kukimbia! nimkimbie samaki! Si mimi huyo; Bassi bwana kuyaona haya tu akamwambia Inshallah. Akaenda zake wahadi Lindi. Lakini Chiwonda yee ameipokea bandera ya Dachi. K. E. L.

MSIMULIZI. 930

SAFARI YA BWANA ASKOFU.

Wengi wenu mwakumbuka kama ilikuwa Sept. 26 tukatoka saa sita katika meli Wissman. Kama saa nane unusu tukawasili Bagamoyo tukalala. Assubui tukatoka tukaingia Dar-es-Salama saa pili. Tukaambiwa kama meli haitoki leo, mpaka kesho saa nne, tukafurahi sana kwani tulikuwa tukitamani sana kushuka pwani kutazama jamaa wakao kule, naye Askofu alikuwa na shauku ya kumwona Bwana mkubwa wa Dar-es-Salama akashuka, lakini hakumkuta kwani alikuja bandari ya Lindi kwa mashauri yake. Bassi bwana Askofu hakukawia akarudi merikebuni. Rev. Denys alikuwa pamoja nasi toka Unguja tukashuka pamoja naye kwenda pwani, Cypriani, Hugh, na wake zao wakafuatana naye kwenda Kichelwe. Lakini mimi nikabaki mjini nikiwatafuta watoto wa Newala wakao kule, nikafurahi sana kuwaona na kuongea nao. Jioni Rev. Cypriani na Hugh wakanikuta kule kule mjini, wakaniambia kama wao na wake zao wanataka kulala pwani illi wapumzike na kulala vema kwani hawa wanaake walikuwa thaifu sana kwa bahari, bassi wikalala pwani. Lakini mimi nikarudi merikebuni, Sept. 28, Juma amosi, waliolala pwani wakapanda merikebuni kama saa ya kwanza. Saa nne tukang'oa kuja zetu Kilwa, kutoka tu mlango wa Dar-es-Salama tukakutana na steamer alimokuwa Bwana mkubwa

MSIMULIZI. 931

wa Dar-es-Salama, tukawa tukipitana tu, illa steamer yetu ikamwamkia kwa kupiga 'whistle.' Tukaenda wee mpaka jioni, na usiku kucha, tukaanza kuona ulimwengu wa Kilwa, panapo saa ya kwanza tukaingia bandarini, ndiyo siku ya Juma apili. Sept. 29, hatukuweza kufanya Usharika kwani hapana mahali pazuri, lakini tulipata nafasi ya kusali sala ya asubui katika 'Cabin' alikokuwa akilala Bwana Askofu nayo ilikuwa nafasi ya kutosha kwa wangoje tu. Wanaake hawakuweza kuja saa nne. Bwana Askofu pamoja na nahodha walishuka kwenda pwani wakarudi alasiri, jioni ikang'oa, kwani watu wa Kilwa walichelewa kushusha mizigo yao bass tulikaa sana tukiwangojea mpaka walipokwisha kushusha.

Kabla ya kutoka tukasali sala ya jioni mapema kwani hatungeweza kusali iendapo. Kwa kuwa tulikuwa dhaifu sana kwa bahari, zayidi Bwana Askofu. Assubui mapema Sept. 80, tukawasili Lindi, tukafurahi sana kwani safari yetu ya baharini imekwisha, lakini hatukupata taabu ya mawimbi makubwa, illa yalikuwa ya kadri tu.

Mimi na wenzangu, tukatangulia kushuka pamoja na mizigo yetu. Bwana Askofu, Mr. Grindrod, na Augustino walibaki merikebuni. Kufika pwani tukashusha mizigo forthani, tukapewa ruhusa kuichukua nyumbani kwetu. Tukafurahi kuwakuta watu wengi wa Chiwata, lakini wa Newala na wa Masasi walikuwa bado hawajaja. Baadaye kidogo Bwana Askofu na

MSIMULIZI. 932

Mr. Grindrod wakashuka, akabaki Augustino peke yake merikebuni akingojea mizigo baadaye akashuka.

Saa sita wakaja wapagazi wa Newala wengi tukaanza kuwagawanya mizigo, lakini hatukuweza kutoka siku ile ile kwani ulikuwa udhia kidogo forthani juu ya mizigo kwani nussu ya mizigo ya Askofu walizuwia pamoja na ya Missions zote za huku, baadaye bwana Askofu alikwenda kusema na mkuu wa fortha, akapata mizigo yake lakini ya Mission aliiacha, tukalala. Lakini ilikuwa taabu sana kwetu kwani Lindi pana njaa sana hatukuweza kupata chakula illa kidogo tu, nacho kikapatikana kwa taabu. Oct. 1, Juma a nne, tukatoka, Askofu, Mr. Grindrod, na mimi, tukapita njia ya mashua mpaka kwa Silim pamoja na wapagazi wachache. Lakini Silim mwenyewe hatukumkuta kwani tulipitana njiani akienda Lindi lakini hatukumwona. Nokoa wake akatukaribisha sana, tukakaa hatta saa nane tukatoka tukaanza safari yetu. Saa a kumi tukafika kwa Mbaruku, tukawakuta wapagazi wengi wakitoka Masasi kuja kuchukua mizigo yao, kukaa kidogo tukawaona wapagazi wetu waliopita njia ya juu wakija, pamoja nao Revs. Cyprian na Hugh. Lakini tukaambiwa wapagazi wengi wachukua mizigo ya Newala wamebaki Lindi kwani hawajapewa mizigo bado, jioni tukakutana Wamasihiya wote na Wanafunzi kusema sala ya jioni.

Saa a sita za usiku wakafika wapagazi waliobaki Lindi na mizigo yao. Assubui Oct. 2, Juma atano

MSIMULIZI. 933

tukatoka mpaka Lilonga. Nikasikitika sana kuona kama hatukuleta wavu wa kumchukulia Askofu, wala wapagazi waliotoka Newala kuja kumchukua hawakuleta, kwa kuwa Sim iliyotoka Unguja haikuagiza wavu hivyo wakathani watu wa Unguja wataleta. Na wakati huu Bwana Askofu, alikuwa amechoka sana kwa mwendo, hatta Mr. Grindrod pia alichoka sana kwani yeye alikuwa na homa kidogo. Kwa bahati tu nikaona taka zima la merikano katika mzigo mmoja, nikatatua nikawapa wapagazi watengeneze machela mahali pa wavu. Wakafunga imara sana, baada ya chakula cha athuuri tukaanza kusafiri. Bwana Askofu aliogopa kwanza kuchukuliwa katika machela kwani aliogopa kama atalewa na kutapika kama merikebuni. Bassi akamwambia Mr. Grindrod aanze illi amtazame. Akaingia akachukuliwa vizuri sana. Baada ya nusu saa akashuka akaingia Askofu wakamchukua vema sana mpaka mto Ukeredi, tulipolala kule tukakutana na wapagazi wangine wa Newala wakienda Lindi kupeleka barua ziendazo Unguja pamoja nao F. Reuben Namalowe akienda Kiungani kusoma baada ya 'holiday' yake ya mwezi. Alhamisi, Oct. 3, asubui tukatoka, mabwana wote wawili walichukuliwa zamu kwa zamu katika machela, tukafika Likolombe, tukapika chakula chetu kula mapema kwani ndio mwanzo wa kuingia jangwa la Mpatila, baada ya chakula tukafanya shauri la kuchukua maji ya kupikia chakula cha mabwana Mpatila. Lakini nikaambiwa

MSIMULIZI. 934

kama tuliagizwa Newala tulipotoka kupatana na Wamakone wa Simba walete maji tukutane nao Mpatila, lakini naliogopa kuacha maji sisi wenyewe kwani sikuamini kama watatuletea maji. Bassi tulikuwa na ndoo mbili tukajaza maji nikawapa wapagazi waliokuwa wakichukua machela wachukue zamu kwa zamu. Tukatoka Likolombe tukaanza kupanda kilima cha kupandia Mpatila. Bwana Askofu ana dira nzuri sana na ya ajabu kwani killa tupandapo kilima chochote inaweza kuonyesha kilima kina 'feet' fullani. Bassi kilima kile cha kupandia Mpatila kina 'feet' 1000 ukifika juu ya Mpatila. Hivyo tukauanza Mpatila mpaka pa 'porter' ndipo tulipolala safari yote, tukalala tu kwani hatukula kwa kuwa hapana maji tukaweza kupika chakula cha Wazungu tu. Wale Wamakonde waliosema wataleta maji hatukuwaona. Saa a saba za usiku Rev. Cyprian na Hugh na safari yote wakatangulia kusudi wakafike mapema kwenyi maji. Mimi na wapagazi waliomchukua Bwana Askofu tukabaki. Saa a tissa tukatoka tukaenda sana kwani mwendo wa watu wachukua machela ni wa mbio sana, lakini tulitaabika sana kwa giza katika vichaka tukafika kwenyi maji kama saa apili asubui wenzetu waliotangulia walifika mapema sana. Tukapika sana pale, saa saba Rev. Cyprian na mkewe wakatangulia kwenda Miwa, sisi tukatoka saa nane mpaka Chitangali ndiyo Oct. 4, Tukasikitika sana kwani tulizikuta nyumba tu hapana mtu, zayidi tukasikitika kwani

MSIMULIZI. 935

tulilikuta Kanisa likiungua moto. Tukulala asubui mapema tukatoka kuja zetu hapa Newala tukapumzika pa Akumkanga. Hapo tukakutana na jeshi kubwa la manjolinjoli pamoja na Wadachi wawili, mmoja ni Bwana mkubwa wa Lindi. Alasiri tukaja hapa Newala njiani tukawakuta watoto wengi wa Mission na waalimu wao, wakapiga bunduki nyingi sana, ndiyo mwisho wa safari yetu. Ikawa furaha sana kukutana hapa tena na Rev. Cecil Majaliwa, Cyprian, Hugh, kwani walikusanyika kwa mashauri.

Oct. 14, Askofu na mimi tulikwenda Miwa kumweka Cypriani katika kazi yake. Tulipofika tu akawahubiria watu na kuwabariki, asubui akahubiri tena kidogo, baadaye akambariki Cyprian, mbele zao wote, kiisha tukaja zetu Newala. K. E. L.

LIKOMA.

Hatukupata habari nyingi za Nyasa safari hii, lakini tumepata kusikia habari hizi katika barua mbili za Mr. Madan, ya Mwal. Arhur R. Mvenya anasimulia habari za marhemu Atlay, na ya Mwal. William anasimulia habari za kuonekana mayiti ya Bwana Askofu. Siku ya Bartolomayo, Padre Atlay alikwenda kuwinda nyama ng'ambo, Watu wazima watatu na watoto wawili pamoja watu wanane mwenyewe tena

MSIMULIZI. 936

alichukua watoto wawili wa Ng'ambo, huko ikawakuta vita ya Makwangwara, bassi watu wote wakakimbia wakamwacha yeye peke yake. Wallakini watu wawili ndio hawaonekani, ndio Wilfred Zulangeti na mtoto mwingine wa huku jina lake Edward Mnyenga, labda Makwangwara wamewaua hatujui ao wamewachukua, labda wamewauza hatujui vema, wallakini huyo bwana ndiye walimwua wakamzamisha majini kumficha, sisi tukaenda kumtafuta wala hatukumwona hatta kidogo, wakaenda watu wangine baada yetu wasimwone, kumbe wamemficha majini, hatta halafu ndio bwana Johnson akachukua watu akaenda huko na huko kutafuta, wakamkuta ametokea juu, walimzamisha na bunduki yake, bassi wakamkuta papo hapo, wakamtoa majini wakamfunga kwa nguo, na siku hiyo walipomwona ilikuwa siku nane baada yakuuawa kwake wakamleta humu Likoma, tukamzika usiku kwani alilala mno majini. Ndio huzuni tu sisi wote hapa Mission, kupita juma moja baadaye tukasikia Bwana Askofu amekufa na bwana Williams. A. R. M.

KOTAKOTA.

Kweli baba dunia ni hadaa, tazama mwezi Nov. 94, Bwana Maples alipita huko kwenda Ulaya hatta juzi July ao Aug. mliongea naye hapo Unguja, lakini

MSIMULIZI. 937

leo je hayuko yuko wapi? Ati alishika safari yee na Mr Jos. Willams kuja zao hapa Nyasa, hatta kufika pale pa Mponda Fort Johnston wakakuta mashua ileile walioingia wewe mwaka jana, "Sherrifi," wakaingia. Lazima yao ndio wapite "West side of the lake." Na siku hiyo upepo ginsi ulivyokuwa mkubwa ajabu, kusi mkubwa alivuma, hatta killa mtu alijua kama si burre angawa hajapata habari alijua. Kwangu Nyumba yangu iliungua moto lakini nalidiriki kuuzima. Hatta panapo Sept. 3, kasha la bati likaokotwa pande za Chia likaletwa bomani tukaangalia tukajua ni vitu vya Mission, lakini hatukuwa na hakika kama ndio mashua yetu imezama. Hatta panapo Ijumaa Sept. 13, ndipo alifika Ibrahimu Kalambilajinja yule yule wa Msumba pamoja na baharia akafika bomani, marra tukapata habari kama bwana mkubwa Maples na Mr. Williams wamefariki kwa maji. Ah, mambo makubwa hayo. Nao baharia ukiwaangalia wamekonda hatta wamekuwa hali ingine kwa maji ya siku moja tu. Bassi nikapewa ruksa na bwana A. F. Sim kuuliza habari hizi tangu mwanzo hatta mwisho, bassi hauliza hapata, zote hamwarifu bwana, marra pasipo kukawia akaniambia, kesho Sept. 14, nitoke kwenda kutafuta mili ya watu hao wawili. Bassi nami pasipo jambo la kunikawilisha tulitoka tu siku ya Sept. 14, pamoja na Ibrahimu na William na Bilali, Usufu, na jumla yetu watu sitashara. Na kazi yetu ndio kupita pwani kwa pwani hatta Kachuru, hatta ilipopinduka mashua ao hapo walipookokea, bassi

MSIMULIZI. 938

tukatoka pwani kwa pwani, rasi kwa rasi, ncha kwa ncha, mchanga kwa mchanga, siku ya kwanza ya pili ya tatu, hatta panapo Sept. 18 tukafika Kachuru hatta panapo 19 tukatoka tukaenda wee pwani kwa pwani majini kwa majini hatta tukafika Mpika "Rock" hapo walipookokea, akina Ibrahimu. Tukaendelea kidogo hatta rasi ingine, tukakuta mwili wa Bp. Maples kati ya mawe matatu, yee kati kati! Ah, bwana wangu ilikuwa kitu kikubwa sana ajabu kuona mwili huu kati ya mawe. Ati baada ya siku 16. Umeharibika kidogo tu, huko na huko mguu mmoja wa shoto umekatika kabisa toka goti hatta nyayo, lakini viungo vingine vizima vile vile. W. E. K.

BARUA YA ASKOFU MKUU WA KANTEBURI.

Addington Park, Croydon, Oct. 6, 1895.

Mpenzi wangu Mr. Travers,

Sikupata barua yako mpaka jana, wakati nisipokuwapo nyumbani, bassi sikuweza kurudisha jibu. Nalikuwa nikitazamia kusikia kwako kama habari ile ya kuogofya si kweli. Imekuwa kama jambo lisilosadikika kama Askofu Maples ametwaliwa na Bwana wetu toka kazi yake nzuri na ya kutumainisha, naye amepelekwa kati ya ziwa kuliweka wakf kwa kufa kwake. Lakini katika ile tharuba ya ghafula ilioshuka naona katika ziwa, kama ile ya zamani, sina mashaka kama Bwana wetu alikuwa akitembea juu ya maji akamwambia mwanafunzi wake, "Ndimi usiogope." Misiba hii ya ghafula katika kazi yetu ni vigumu kwetu kufahamu, illa Mwenyezi Muungu peke yake, lakini tunayo hazina katika vyombo vya udongo bassi havina buddi kuvunjika marra kwa marra.

MSIMULIZI. 939

Askofu wa Hereford nalimjua sana na kumpenda nilipokuwa nikikaa Cambridge, tena alikuwa mkubwa wangu. Alikuwa na furaha sana, na shukrani, alipoamriwa mwanawe George kwa kazi hii, hatta kufa kwa mtoto huyu, na kumfuata upesi babaye kwenda ulimwengu ujao, naona ni kama jambo lililo karibu nami. Twaweza kusema, "Ole! kwa kazi yetu," Lakini haimkini kusema Ole I kwa kazi ya Masiya.

KIUNGANI.

Safari hii sina maneno mengi ya kuwaarifu, kwani sisi watu wa visiwani hatuna habari nyingi kama watu wa Mrima. Lakini nina habari moja nataka kuwaarifu, ndio habari ya siku kuu yetu ya Andrea Mt.

Mwaka huu siku kuu hii tumefurahi kwa namna nyingine. Kwani miaka hii miwili iliopita furaha ya siku kuu hii ilikuwa kuwaita watu wa zamani waliokaa hapa nyumbani na kuwakaribisha. Lakini mwaka huu ilikuja hivi. Maana siku kuu ilikuja siku ya Jumaa mosi bassi tukafanya kazi Ijuma, na Jumaa mosi ikawa furaha ya siku kuu. Assubui tulishinda papa hapa, na alasiri tukatawanyika kutembea. Na hivyo isitoshe, tukataka kwenda pande za shamba kutembea. Bassi Mr. Madan akaandika barua kwa General Matthews kutaka mashua moja ya moshi ipate kutuchukua. Bassi General Matthews akamwazima meli nzima jina lake,

MSIMULIZI. 940

Barawa, kubwa, swafi, na yenyi wasaa. Bassi tukaona haijuzu tuingie peke yetu, tukawakaribisha jamaa zetu wa Mbweni, na watoto wa Kilimani, jumla tulipata foko watu miteen.

Bassi siku ya Jumaa a nne ndipo tulipoingia. Tukaondoka hapa Kiungani kama saa a pili unussu, tukaenda mpaka mlango mkubwa wa fordha, tukaingia hatta pwani. Tuliuzimwa mashua moja kubwa na mkubwa wa fordha, bassi wakiingia watoto kama arobaini kwa marra moja na kwenda kuwatia katika Barawa.

Tulipokwisha kuingia wote ilikuwa kama saa nne tukaanza kuondoka bandarini. Tukaongoza pande za kaskazini, tukipita pwani kwa pwani, na kuangalia mashamba ya pwani pwani, yakionekana vizuri sana. Nia yetu ilikuwa kwenda mpaka kisiwa Mwana Mwana penyi mnara wa taa, kutia nanga na kushuka pwani. Lakini haikuja kama tulivyotaka. Kwani tangu mjini mpaka Mwana Mwana tulikwenda kwa saa nne, tukafika kama saa nane, tukaona kama tukitia nanga tutachelewa. Bassi tukapindua tukarudi. Ikawa kuja zetu taratibu mpaka tukawasili bandarini, kufika tu bandarini ikapiga saa a thenashara. Bassi wakashuka kwanza wanaake, tena watoto wa Kilimani, na mwisho sisi. Tukafika nyumbani kama saa a pili. Tukafurahi sana siku hiyo, bahari haikuchafuka ilikuwa shwari kwenda na kurudi. Mtg.

MSIMULIZI. 941

MKUTANO.

Nimeona ni wajibu nitie humu habari za mkutano wa Wamasihya wa Bonde uliofanyika siku hizi. Na habari hizi nimetwaa katika Msimulizi wa Bonde na Zigua unaokwitwa Habari za Mwezi, ulioanza mwaka huu.

Itafaa kumjulisha killa mtu mambo tuliyopatana katika mkutano wetu wa kwanza, kwani Wamasihya wote hawakuwapo penyi mkutano, Tumepatana kama mtu yeyote avunjaye maagano haya amekosa naye hana buddi kutengwa katika kanisa kwa kitambo hatta atakapokiri kama kweli amekosa na kukusudia kutubu kwa moyo pamoja na kufanya ahadi kama atajaribu kwa kadri awezavyo kushika amri za Muungu na mapatano ya Wamasihya wenzake, wote twajua hakika ya methali ile inenayo, "mvunja inchi mwana inchi," maana yake avunjaye inchi ni mzalia wa inchi, kwani ajua njia zote za inchi yake na madhehebu na tabia za watu wa inchi yake, vivyo kadhalika na mambo ya desturi za inchi, aliye mzalia wa inchi hujua kanuni kuliko mgeni, mgeni ajapo kaa katika inchi na kujua lugha kama mwenyeji haimkini kujua desturi zote pia wazifanyazo wenyeji wa inchi, kwa hiyo sisi Wamasihya wa Bonde tukafanya shauri kukutana pamoja tutazame desturi zipi ziwezazo kupatana na Dini ya kimasihya, na zipi ziwapasazo wamasihya kuacha wakikusudia kuwa wamasihya kanuni.

MSIMULIZI. 942

Mkutano ulianza saa nne wa robo haukwisha mpaka saa nane.

Tulikusudia kufikiri mambo kama sitashara wallakini hatukuwahi kwisha yote. Tuliyoapatana ni haya:

1 Mmasihiya aliye yote hana ruksa kuoia kibondei wala kuwalazimu watoto wake kushika kawaida hii. Mmasihiya aliye yote akihalifu mapatano haya, amestahili kutengwa katika kanisa na kuhesabiwa kama Mwanafunzi hatta atakapona kama kweli amekosa na kutubia kosa lake.

2 Mmasihiya aliye yote hana ruksa kuingia katika kiwanja ao galo ao kuwa kungwi (shahidi) katika mambo haya akitenda haya amekhalifu maagano ya mkutano, naye kadhalika atatengwa.

3 Mmasihiya aliye yote hana ruksa kuwa kungwi katika harusi ya kishenzi, kwani akiwa kungwi hana buddi kuwafunza na kuwafanyia wengine mambo yale ayakataayo mwenyewe, Awapo kungwi amekuwa mkhalifu, ana lazima kutengwa.

4 Mmasihiya aliye yote hana lazima kushika desturi ya kutoa mimba kwani ni kuvunja amri ya sita ya Muungu atendaye haya ni mkhalifu atatengwa.

5 Mmasihiya aliye yote hana ruksa kuazima nyumba yake kwa watu wakusudio kuvunja amri ya Muungu, kwani akifanya hivi ashariki

MSIMULIZI. 943

dhambi yake, na kupendezwa na watu wajifungao kuvunja amri ya Muungu kusudi, afanyaye jambo hili amekosa, atatengwa.

6 Mmasihiya aliye yote hana ruksa kwisha kilio, kwani hii ni desturi ya kishenzi wala haimzidishi rehema ya Muungu ao wema wa yule aliyefariki. Atendaye haya amekosa ana lazima kutengwa.

7 Fika ya namna yoyote imegombezwa kwa wamasihiya kwani ni kumwomba, na kuamini kama yule aliyefariki ana nguvu za kukupa afya na uzima. Habari za Mwezi.

KWA MPONGA.

Habari za kwa Mponga ni hizi; leo hivi walikuwa watu wawili, mtu na nduguye, nao ni wabwanga wazima mmoja aitwa Semote na mmoja Mwakombo. Bassi hawa walitoka kwenda kukamata nzige, hatta vibuyu vyao vikajaa nzige tele. Mmoja akamwambia mwenzake, twende mtoni tukaoge, hatta walipokaribia mtoni "wakasikia sauti zikinena, watu wa kwa M'ponga mwatida;" Zile nzige zikanena "wache watu wangine watule. Hatta nyinyi watu wa kwa M'ponga mwatida." Bassi watu wale wakatupa zile nzige wakaenda mbio mjini wakawaambia watu

MSIMULIZI. 944

kama nzige wanena. Kwa hiyo mtu yo yote wa kwa M'ponga asile nzige! Kwa sababu mihindi ya kule hailiwi na nzige ndio maana nzige leo wakanena. "Heri watu wa Magila na wengine turathi watule." Bassi watu wa kwa M'ponga wanena hivyo.

Habari za Mwezi.

SAFARI YA BWANA ASKOFU TOKA MASASI HATTA UNGUJA.

Salamu kwa ndugu mtazamiao kusikia killa safari Mtengenezaji analowapasha, akipokea kwao wamleteao habari ziwazo zote.

Bassi Bwana askofu alipofika kule Newala, tukaambiwa kama alipokewa kwa furaha sana, na kilichopunguza furaha yao ndio mfalme mwenyewe mzee Matola alikuwa mgonjwa sana na tukaambiwa alipokuja tu Askofu baada ya siku mbili tatu mfalme huyu akafariki. Nanyi mmesikia katika Msimulizi ulio wa pili wake huu kama alikuwa mgonjwa mno hatta akapata kubatizwa, tena mmejua kama alikawa sana ugonjwani mwake, bassi alifariki na Askofu angaliko kule kule Newala. Lakini zamani za kufariki kwake na kuzikwa, huyu Askofu alikwenda kuangalia Station moja itwayo Miwa, akaapo sasa Rev. Ciprian H. Ch. Mzee huyu aliwaacha watoto wake waliompenda mno, alipojua kama amekuja yule atakayekuwa baba wa watoto wangu, ndivyo ilivyokuwa kwa maneno machache juu ya kufa kwake.

MSIMULIZI. 946

Bassi askofu akiisha kuwaangalia wenzetu kule, kwa siku nyingi kidogo akawa na nia ya kufunga safari yake ya kuja pande za kwetu Masasi. Na Askofu alipokuwa na nia hiyo na kule Masasi tunamtazamia sana, hatta padre akatupeleka sisi wawili kwenda kupata hakika ya kutokea kwake, mimi na Benedicto K. N. Nasi tulitoka Oct. 23 kwenda Newala tukafika mnamo Oct. 24, naye akatupa barua ya kunena nakuja baada ya juma mosi, naswi ikatupasa kurudi na kumpa habari padre Carnon aliyetupeka kusikia habari zako huyu Askofu. Tukafika Masasi Oct. 28,

Kwa juhudi nyingi tukamtazamia Bwana Askofu zayidi ya siku 8. Bassi mwisho kunako Nov. 4, Tukapata habari kama atatoka kesho Newala, nayo ni kweli alitoka November 8, kule Newala, kumbe ilikuwa pamoja na Shemasi wake padre Daudi M. Bassi zamani za kukaribia kule njiani karibu na nyumba (hiyo) ya Mission. Tukawaona kwa kuwastukia tu kwani si njia tuliyokichunguza kwa juhudi na furaha. Bassi mwajua sisi kuamkiana kwetu kama tukiwa tukifurahia jambo kubwa lazima bunduki. Tukamwamkia kwa bunduki mpaka nyumba yake kwa baruti tu kuichoma moto. Na watu wakaja ghafula hiyo zayidi ya mia mbili. Tukaamrisha michezo, watu waliokuja. Ah! walicheza kwa nguvu na furaha nyingi mno. Na bunduki zile tukapiga mpaka saa sita urobo, zilianza saa tatu, nayo saa sita tuliacha maana tuwe na nafasi ya kupata chakula.

MSIMULIZI. 947

Mnamo saa nane zikaanza vile vile pamoja na michezo, kwenyi saa kumi tukapumzika, lakini wale waliopenda kuwa na furaha zayidi, tukanena heri mje mnamo saa a kwanza ya usiku (jioni), kweli nao wakaja wengi, tukaanza kucheza na bunduki pia zinalia mumo kwa mumo mpaka saa a nne ya usiku tukatawanyika kwenda killa mmoja nyumbani kwake.

November 13, walitiwa mikono Wamasihya wa Chiwata na Mwiti kwani ndiko wakaako sasa, kule Chitangali mzee Barnaba Nakaam ametoka, bassi anakaa Chiwata na nduguze wanakaa mahali pamoja panaitwa Mwiti. Kwani wakaja kupewa pande za Masasi Sacramenti ya Kipa imara? Sababu mahali pale wakaapo wamekuja siku hizi hizi bassi hawajadiriki bado kujenga kanisa walikuwa hawana buddi mwaka huu kuja kule Masasi maana kuna kanisa, twatumaini mwaka mgine hawatakuwa watu wa kwenda pangine kwa kusudi hili.

Nov. 15, Mwalimu Klement M. alisafiri kwenda pande za Lilulu kwa babaye kutafuta chakula, nathani wote mnajua kama pande za huko Masasi na Newala, njaa kubwa imeingia mno sana, isiyokuwa na mahali pa kutafutia chakula kabisa, bassi tulipata habari kama kule kipo chakula ndio maana Padre akaona vema aende Mwalimu Klement maana kwa babaye atakwenda pata msunje - Uji kidogo, wapone watoto wa Mission. Alikaa kama siku tatu akarudi na mizigo miwili tu, nguo zikarudishwa zingine

MSIMULIZI. 948

kwani nako waliikuta njaa, wanacho cha kuponea wenyewe tu bassi akatufikia hapa Nov. 18,

Nov. 20, walitiwa mikono hapa watu wazima na watoto wa Mission jumla watu 45 pamoja.

Nov. 24, tulikuwa na furaha mno sana kumwona Mwalimu. Klement akipewa "Uso maji" baada ya kufanyiza kazi yake kule Masasi; napo ndio siku ya kuaga sisi ulimwengu ule wa Masasi, kwani panapo Juma a tatu yake ndio tukatoka kuja Unguja ndio Nov. 25, pamoja na huyu Mwalimu Klement. M. anakuja kusoma hapa tayari kwa kazi ya Ushemasi.

Tulipotoka kule Masasi ilikuwa juma a tatu tukaenda mwendo wa saa 4 tukafika Mwiti mahali anapokaa sasa Padre Cecil na pale tukakutana na Mwenyi Barnaba Nakaam akienda pande za kwetu Masasi kutengeneza uthia wa vita tuliokwisha kusikia katika Msimulizi uliopita. Bassi wakaamkiana wote, watoto, Padre, Mzee Barnaba, na Askofu, tulikaa pamoja nao kwa saa 4 kamili. Tena yule Padre Daudi, tukamkuta pale pale Mwiti maana alitangulia kutoka kule Masasi mwezi Nov. 21, Bassi kwenyi saa kumi tukatoka sisi kwenda kulala Chiwata mji wa mfalme Barnaba, lakini mwenyewe ndiye yule tuliyepitana naye Mwiti, bassi tulimkuta mtoto wake tu, Mwalimu Gilbert Y. M. akatukaribisha vizuri sana, assubuhi Nov. 26 tukaagana naye na kusema sala zetu pamoja tukaenda weeee ah! njia ya taabu sana, marra

MSIMULIZI. 949

twapanda, panginge twashuka, hatta Askofu akatuuliza, "who made this path?" Tukaambiwa kama mtu huyu alikuwa akienda kwa rafiki yake, bassi akafanyiza njia hii illi akawasili upesi kwa rafiki yake asiuthike kuzunguka, akastaajabu sana Askofu na sisi pia, kwani siyo mahali pa kuangusha mzigo ukauokota hatta ungejaa vitu gani, hautamaniki tena, ilikuwa kama nussu ya siku ile tukitaabika tu na vilima hivi. Tukaenda kupikia mto mmoja unaitwa Mbwinji. Maji yake mazuri sana. Tukatoka tukaenda kidogo tukapumzika akanywa 'cocoa'. Askofu na sisi pia tukapika tena, sababu tulikiingia jangwa kuu lisilo na maji ndio maana tukala mapema, tulikwenda sana, lakini kwa nguvu za pale, mpaka saa a kwanza jioni ndio tukafikia kijiji, jumbe wake aitwa Makuwango tukatia hapa hema na kulala na assubuhi kama saa a kwanza, Nov. 27 tukaenda zetu mpaka kwa Satia tukapita, tukaenda kupikia miji yake ya mwisho, Pa Nmmaogo na tukatoka kama saa 7 kwenda kidogo ikatukuta mvua, tukakimbilia majumbani, na tulipotoka hapa ndio mpaka Lukuredi tukalala.

Nov. 28, tukatoka pale mpaka kwa Martin Liwengwa, tukapikia tukienda zetu Mtua kulalia tulifika kama saa kenda hivi.

Assubui Nov. 28, tukatoka pale mpaka kwa Mbaruku, tukala chakula chetu, na kusikia kama Lindi kwema hakuna uthia.

Tukatoka saa 8 tukafika kwa Silim saa kumi

MSIMULIZI. 950

kasorobo. Lakini mwenyewe hatukumkuta illa mtoto wake tu Abdallah naye angetukaribisha bali tulitoka upesi tu, na wapagazi wakarudi zao kwenda kupita barabarani, sisi tukaingia ndani ya mashua ya Sagara, maana Askofu aliagiza itukute kwa Silim, nayo ikatukuta kweli. Tulikwenda kwa taabu sana hapakuwa na upepo, bassi tukaingia Lindi saa tatu ya usiku. Na wapagazi waliopita njia ya mlima hawakuweza kufika siku ile ile maana walichoka lakini nussu wakafika kama wakati ule tuliofika sisi mnamo saa a tatu za usiku. Mwalimu Harry Mnubi hatukumkuta (maana alikuwapo pale akijenga nyumba ya Mission kufikia wazungu wasafirio, na kufikia safari zitokazo pande za kwetu kuchukua mizigo ya Mission) Kwani hatukumkuta? Ah jambo hili la huzuni lilikuwa kwetu, maana meli yetu ilituacha, ilitangulia kutoka pale Lindi, tungesafiri pamoja na huyo Mwalimu kufika hapa Unguja. Bassi tukawa watu wa kukaa tu pale Lindi, baada ya siku 4 Askofu akamwendea Bwana mkubwa wa Madachi; Major von Wissman, kumwamkia na kumwarifu haya, bassi kwa wema wake akasema nasafiri kesho kutwa kwenda Dar-es-Salaam heri tufuatane pamoja. Bassi pale Lindi tulikaa kwa siku sita tukaja zetu tukaingia ndani ya Steamer, lakini Bwana Askofu alikuwa mgonjwa wa kifua siku zote tulizokaa Lindi, na tulipoingia katika 'Steamer' akauthika sana, tukaenda siku ile

MSIMULIZI. 951

mpaka Kiswele, Askofu akashuka kulala pwani nasi tukamfuata tukaenda kulala kule kule pwani. Assubui mapema ndio Dec. 8, tukapanda, ikang'oa nanga mpaka tukawasili Kilwa mnamo saa tano, tukakaa kwa saa tatu, na saa nane tukang'oa naaga, mnamo saa a kwanza ya usiku 'Steamer' ikatia nanga penyi kisiwa chaitwa Chore. Tukalala mpaka saa a thenashara assubui. Na Dec. 9, ndio tukafika Dar-es-Salaam. Na Herr von Wissman, alimkaribisha sana Askofu kama alivyoweza. Sisi sote tuliokisafiri na Askofu tukawa tukilishwa kule kule. Ah kufayidi tu katika majumba ya watu wazima. Tukakaa kule tukungoja meli tuingie kuja hapa Unguja.

Watoto wengi waliotoka pande za kwetu wako kule Dar-es-Salaam bassi tukaongea sana nao, nao wote hawajambo, na wenyi afya zao, wakatukaribisha sana.

Baada ya siku mbili tukaona marekebu moja ya Waingreza inakuja, Tuchunguze ni H. M. S. Barrosa, ilikwenda kule kasidi kuwachukua Maofsari kwenda kumwamkia Governor von Wissim an. Bassi kwa bahati ndio ikatukuta kule. Bwana Askofu akaenda kumwamkia 'Captain' mwenyewe Mr. Startin na kumwambia kama naenda Unguja bassi wakatukaribisha kwa furaha sana. Tukatoka panapo Dec. 12, kule Dar-es-Salaam, siku ile ile tukafika Unguja mnamo saa a thenashara kasorobo, tukashuka. Tungefika mapema lakini tulitoka kule kama saa 5 hivi, ndio habari. I. F. M.

MSIMULIZI. 952

HABARI ZA MACHEMBA.

Ulipokuwa Lindi Bwana Askofu na sisi watatu, Klement, Isaya, Benedict. Kunako Dec. 4, Bwana Wissman alikusanya kombania zote za askari wa Dar-es-Salam na Kilwa na Lindi pia kutaka kwenda kwa Machemba bin Mchakama, kusudi kumpiga. Maana mmeisha sikia habari za Myao huyu ginsi alivyofanya uthia njia ya kwenda pwani washenzi hawapiti kabisa illa kwa shidda sana. Wengi wao wakinyang'anywa mali zao. Bassi kwa uthia huu Bwana Wissman amekasirika kabisa, hatta anaona haya kabisa kwa sababu marra ya kwanza Wadoicha walipokwenda kupigana naye zamani, Wadoicha walishindwa. Na sasa Bwana Wissman hataki kabisa kushindwa naye.

Bassi hawa askari wengi sana sana, 'Steamers' mbili "Rovuma" na "Rufiji." Zikajaa askari wenu, na wangingeo wakapita inchi kavu wakakutana Sudi. Bassi Machemba alipopata habari kama Dachi anakuja kukupiga, akaona vimoto safari hii, kushindwa tu. Bassi akafanya shauri na mawaziri wake lipi watakalolitenda? kwani pana mawili, "Ukali wana ililo, woga wana iseko." Tafsiri yake ndio, Ukali huleta huzuni, na woga huleta furaha." Naye huyu Machemba akachagua, la pili ndio 'woga' illi apate furaha. Kwani anamfikiri rafiki yake mmoja ndiye Makunganya alichagua lile la kwanza la 'Ukali' kwa

MSIMULIZI. 953

sababu hiyo amepata hasara kubwa sana.

Watu wake wengi wengi wameuawa, naye mwenyewe akasongwa ndiyo mwisho wake. Bassi Mchemba akifikiri hayo anaona heri kuwa mwoga kuliko kupata hasara kama ile ya rafiki yake. Bassi wakuu wake naye mwenyewe pia wakatoka waende kumlaki Mdachi kutaka kupatana. Bassi naye Mdachi akakubali kupatana naye. Tena Mchemba akatoa vitu vingi sana na pembe pia ishara ya kupatana. Lakini Mdachi alikataa kupokea zawadi ile. Illa Dachini akamwambia sharti ukitaka kupatana na sisi ulete bunduki na selaha zote za vita, na tena ukubali bandera ya Kidachi. Bass akakubali zikaletwa bunduki 50 na pipa 5 za baruti. Akapokea Dachini. Akampa bandera ya Kidachi akamwambia "Sasa amani, nikisikia haifanyi uthia tena kwa watu nitakurudishia bunduki zako na tutapatana kabisa." Bassi sasa Mmasaniga huyu yuko chini ya Dachini. Baada ya kutengeneza haya askari walio wengi wakarudi Lindi. Tena Bwana Wssiman na askari kama settini hivyo na wazungu wa sita wakaenda kwenda Masasi. Na walipofika kule watu wengi wakakimbilia milimani wakithani ndio vita. Lakini siyo vita walikwenda kwa amani tu. Bass wakakaa kwa siku chache tu wakaenda Newala. Wakatoka Newala hatta Mikindani kurudi zao Lindi na Dar-es-Salam. Ndio habari. K. M.